

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 23 Aprili, 2020**

*(Bunge lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tukae. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani Na:-

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MHE. JORAM I. HONGOLI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 133

**Hitaji la Watumishi Hospitali ya Wilaya ya Ludewa**

**MHE. NEEMA W. MGAYA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya upungufu wa watumishi Hospitali ya Wilaya ya Ludewa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAMISEMI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2016 hadi Machi, 2020, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepeleka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa jumla ya watumishi 108 wa kada mbalimbali za Afya ambapo watumishi 25 kati ya hao walipangwa kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Aidha, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepata kibali cha kuajiri madaktari wengine 610 ambao watapangwa kufanya kazi kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya nchini vyenye upungufu mkubwa wa watumishi.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri toka Wizarani, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa bado kuna changamoto kwenye Zahanati karibu Wilaya zote nne ndani ya Mkoa wa Njombe, kwa maana ya Ludewa, Njombe, Waging'ombe na Makete: Je, ni lini Serikali itatupatia watumishi katika Zahanati zote?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inaendelea kuomba vibali vya ajira UTUMISHI ili kutatua tatizo la upungufu wa Watumishi wa kada ya Afya uliopo nchi nzima wa takribani asilimia 52. Ni ngumu kutimiza mahitaji ya watumishi kwenye Vituo vyote vya kutolea huduma kwenye Mkoa wa Njombe kwa wakati mmoja. Kwa kawaida vibali vya ajira vinapo patikana, Halmashauri hupelekewa mgao wa watumishi kwa mgawanyo unaozingatia uhitaji kwa kila Halmashauri, ambapo Halmashauri huwapangia watumishi hao Vituo vya kazi kuenda na mahitaji yaliyopo ndani ya Halmashauri.

Na. 134

#### **Uanzishwaji wa Maktaba Mashuleni**

**MHE. MARIA N. KANGOYE** aliuliza:-

Shule nyingi za Sekondari na Msingi hususan za Serikali zimekuwa hazina Maktaba:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali juu ya uanzishwaji wa Maktaba Mashuleni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ndila Kangoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuititia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (*EP4R*) imekamilisha ujenzi wa majengo ya maktaba 39 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.95.

Aidha, shule ambazo hazina maktaba zimetenga vyumba maalum ambavyo vinatumika kama maktaba kwa ajili ya kutunza nyaraka mbalimbali za shule na wanafunzi kujisomea. Serikali inaendelea na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ya shule ikiwemo ujenzi wa maktaba ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu Mazuri ya Serikali juu ya swali langu Na. 134 kuhusu uanzishwaji wa maktaba mashulenii, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maktaba zilizoanzishwa na Serikali ni chache sana kulingana na uhitaji; na kwa kuzingatia uhaba wa maktaba ndani ya shule za Mkoa wa Mwanza, napenda kujua ni mkakati gani hasa Serikali imepanga juu ya kuhakikisha kwamba licha ya shule kutenga vyumba kwa ajili ya maktaba, zinapata vitabu vya kutosha?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kupeleka vitabu vya kiada kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini ambapo mpaka sasa wastani ni kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu kwa mikoa yote nchini. Lengo ni kufikia wastani wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja. Serikali itaendelea kupeleka vitabu vya kiada mashulenii na inawakaribisha wadau wa elimu kuendela kuchangia vitabu kwenye maeneo mbalimbali nchini ili kufikia lengo kuu.

Na.135

**Ujenzi wa Bwawa – Kijiji cha Ichemba**

**MHE. JOHN P. KADUTU** aliuliza:-

Hivi karibuni wataalam wa maji walifika katika Kijiji cha Ichemba Ulyankulu kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bwawa.

Je, ni lini sasa mchakato huo utakamilika ili wananchi wa eneo hilo wapate maji?

**WAZIRI WA MAJI** aliibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Ichemba litakapokamiliika litakuwa na uwezo wa kuhifadhi maji kiasi kinachokadiriwa kuwa lita bilioni 3.6 kwa mwaka ambazo zitahudumia wakazi zaidi ya 143,473 waishio katika Kata tisa zenye vijiji 28 katika Tarafa ya Ulyankulu. Kata hizo ni Ichemba, Kanoge, Mwongozo, Nhwande, Makingi, Sasu, Kamindo, Milambo na Igombemkulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umeanza kwa kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwaa kuanza na kukamiliika katika mwaka wa fedha wa 2020/2021.

Na. 136

**Fidia ya kipande cha Barabara ya Ardhi – Makongo**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Je, ni lini fidia ya kipande cha barabara ya Chuo cha Ardhi – Makongo italipwa ili kukamilisha ujenzi wa barabara ya Ardhi – Makongo – Goba?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
aliibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ardhi – Makongo – Goba iko chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijiji (*TARURA*) chini ya TAMISEMI. Barabara hii ni moja ya barabara zilizokasimishwa *TANROADS* kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hii umechelewa kukamilika kutokana na mali nydingi kuwa kwenye eneo la ujenzi. Hata hivyo, uthamini umekamilika na sasa uhakiki wa fidia unaendelea chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Baada ya uhakiki kukamilika fidia ya kipande cha Barabara ya Chuo cha Ardhi – Makongo italipwa ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo.

Na.137

### **Hitaji la Mawasiliano Jimbo la Igalula**

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI** aliuliza:-

Katika Jimbo la Igalula, Kata ya Memale na Vijiji vyake vyote havina Mawasiliano ya simu, pia Kata ya Loya Vijiji vya Migongwa na Mugulyati na Kata ya Tura Vijiji vyote Nkongwa na Mmunyu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
aliibusu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swala la Mheshimiwa Mussa Rashidi Ntimizi, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hitaji la mawasiliano katika Jimbo la Igalula hususan katika vijiji vilivyopo kwenye Kata za Memale, Loya na Tura ambapo kupitia Mfuko

wa Mawasiliano kwa Wote maeneo hayo yameingizwa kwenye orodha ya maeneo yanayohitaji huduma za mawasiliano kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Vijiji vya Magulyati na Migongwa katika Kata ya Loya viliingizwa katika mradi wa Mawasiliano Vijijini, Awamu ya kwanza ambao ulishakamilishwa kuitia mzabuni - Kampuni ya Mawasiliano ya Tigo mnamo tarehe 8 Machi, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa vijiji vya Munyu na Nkongwa Kata ya Tura, tayari Kampuni ya Mawasiliano ya Airtel imepewa jukumu na utekelezaji wa kufikisha mawasiliano kwenye maeneo hayo ulianza rasmi tarehe 24 Januari, 2020 ambapo utekelezaji unatarajiwa kukamilika ifikapo Oktoba, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umeainisha Vijiji vya Kata ya Mmale kwa ajili ya kupelekewa huduma ya mawasiliano kwenye awamu ya tano itakayoanza mwezi Septemba, 2020.

Na. 138

### **Miradi ya Mchuchuma na Liganga**

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA** aliuliza:-

Je, ni lini miradi ya Mchuchuma na Liganga itaanza?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**, alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu Swalii la Mheshimiwa Deogratias Francis, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya chuma cha Liganga na makaa ya mawe ya Mchuchuma iliyopo katika Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe inalenga kuzalisha na

kuongezea thamani madini ya chuma na uzalishaji wa makaa ya mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo unganishi inajumuisha mgodi wa chuma Liganga wenyewe uwezo wa kuzalisha tani milioni 2.9 kwa mwaka; kiwanda cha kuzalisha bidhaa za chuma Liganga tani milioni 1.1 kwa mwaka; mgodi wa makaa ya mawe huko Mchuchuma wenyewe uwezo wa kuzalisha tani milioni tatu kwa mwaka; kituo cha kufua umeme huko Mchuchuma cha Megawati 600; Msongo wa kusafirisha umeme wa kilovoti 220 katи ya Mchuchuma na Liganga; na barabara kutoka Mchuchuma hadi Liganga (*shortcut route*).

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo pamoja na kuingia mikataba ya ubia, inahitaji fedha nyingi na teknolojia ya kisasa ili kuweza kuzalisha kwa ushindani katika soko la sasa la madini hayo. Kasi ya utekelezaji wa mradi huo umeathiriwa na changamoto ya upatikanaji wa mtaji na gharama za teknolojia ya kuchenjua chuma chenye aina nyingine za madini yenye thamani kubwa (*vanadium na titanium*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sote tunavyofahamu, Serikali tayari ilishaanza jithada za utekelezaji wa miradi hiyo. Hivi sasa Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilipitisha sheria mbili zinazohusu madini na mali za nchi. Kwa mujibu wa sheria hizo, mikataba yote ya awali inahitaji kurejewa upya. Hivyo, Serikali inaendelea na mazungumzo na wawekezaji ili kupata muafaka wenyewe maslahi mapana na kwa kuzingatia sheria za nchi ili kuwezesha hatua nyingine za utekelezaji kuwa tija.

Na. 139

### **Mbuga ya Selous kutokutambuliwa kama Hifadhi ya Taifa**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza: -

Mbuga ya Selous ni miongoni mwa Mbuga kubwa Tanzania, lakini haitambuliki kama Hifadhi ya Taifa kama mbuga nyingine kwa mfano Mikumi -

Je, ni lini Serikali itaipa mbuga hiyo hadhi ya Hifadhi ya Taifa?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifutatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Pori la Akiba Selous lilianzishwa mwaka 1922 na kutambuliwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 275 la mwaka 1974. Pori hilo ni miongoni mwa mapori maarufu na yenye sifa ya kipekee Tanzania, Afrika na duniani. Sifa hizo ni pamoja na ukubwa wa kilometa za mraba 50,000 na wingi wa wanyamapori wa aina mbalimbali wakiwemo tembo, mamba, viboko, nyati na mbwamwitu. Pia, pori hilo linasifikasi kwa kuwa na mito mingi, miinuko na mabonde mbalimbali. Kutokana na upekee huo, Pori la Akiba Selous limeorodheshwa kuwa eneo la Urithi wa Dunia (*World Heritage Site*) tangu mwaka 1982.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mnamo tarehe 29 Novemba, 2019 sehemu ya Pori la Akiba Selous yenye ukubwa wa kilometa za mraba 30,893 ilipandishwa hadhi na kuwa Hifadhi ya Taifa Nyerere kwa Tangazo la Serikali Na. 923 la mwaka 2019. Kifungu Na. 3 cha Sheria ya Hifadhi za Taifa ya mwaka 2003, kinampa mamlaka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzisha na kutangaza eneo lolote la ardhi kuwa hifadhi ya Taifa. Kupandishwa hadhi kwa sehemu ya pori husika kumefanya idadi ya hifadhi za Taifa kuwa 22 na pia kunaifanya Hifadhi ya Taifa Nyerere kuwa hifadhi kubwa ya Taifa Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, Serikali kuititia Wizara imeanza kuweka mikakati mbalimbali ya kuendeleza Hifadhi ya Taifa Nyerere pamoja na sehemu ya Pori la Akiba Selous iliyobaki. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha miundombinu na kuzitangaza kwa nguvu zaidi ili ziweze kukidhi manufaa yaliyotarajiwa.

Na. 140

### **Kujenga Hospitali ya Rufaa – Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa Serikali wa kujenga Hospitali ya kisasa ya Rufaa katika Mkoa wa Morogoro?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro ni mionganini wa Hospitali za Rufaa za Mikoa 28 ambazo zinatoa huduma za ngazi ya Rufaa Mkoa. Hospitali inahudumia wastani wa wagonjwa wa nje 500 hadi 700 kwa siku na kati ya hao, wanaolazwa wagonjwa wapya ni 70 hadi 80 kwa siku. Hospitali ina jumla ya vitanda 365 kati ya vitanda 500 vinavyohitajika kwa ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Hospitali hii ina upungufu wa majengo ya kutosha ambayo yanababishwa na ufinyu wa eneo la kujenga majengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali hii imekuwa ikipokea majeruhi wengi wa ajali (wastani majeruhi 2,414 kwa mwezi). Hii ni kutokana na Mkoa wa Morogoro kuwa ni mapitio ya barabara kuu inayounganisha mikoa mingi ya Tanzania Bara. Aidha, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Morogoro inatoa huduma kama Hospitali ya Wilaya, kwani Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Mvomero hazina Hospitali za Wilaya, hivyo kufanya Hospitali hii kutumika kama Hospitali ya Wilaya kwa Halmashauri hizo tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kufanya upanuzi wa mara kwa mara, bado kumekuwa na changamoto ya majengo kwani majengo mengi katika

Hospitali hiyo yalikuwa yakitumika katika vita kuu ya dunia kama kambi tangu mwaka 1954 na baadaye kutumika kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa sasa kuna uhitaji wa kujenga hospitali kubwa na ya kisasa ya Mkoa ili kukabiliana changamoto zilizolezwa hapo juu. Kwa kutambua umuhimu huo, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Morogoro inaendelea na hatua za kupata eneo la ujenzi wa Hospitali ya Mkoa. Serikali itaanza kutenga fedha za ujenzi baada ya taratibu za umiliki ardhi kukamilika.

Na. 141

### **Kutengeneza Benki ya DNA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, Serikali ina makakati gani wa kutengeneza Benki ya *DNA* kama mkakati wa kupunguza uhalifu, kwa kuwa ni rahisi kupata watuhumiwa kwani Benki ya *DNA* itasaidia *ku-match* na watakaohisiwa?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuititia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni mtekelezaji wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu (*Human DNA Regulation Act No 8, 2009*) kifungu cha 59 (1) na Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (*GCLA Act No. 8, 2016*) kifungu cha 32 (1). Imepewa jukumu la kuanzisha na kusimamia Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali za utambuzi

wa binadamu ikiwemo kubaini wahalifu (mfano: wahusika wa matukio ya ubakaji, mauaji na ujambazi) kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama nchini pamoja na kusaidia utambuzi wa binadamu wasiotambulika baada ya kutokea majanga mbalimbali, mfano ajali za moto, milipuko, ndege, magari na kuzama kwa meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia utekelezaji wa sheria hizo mbili na mkakati wa kupunguza uhalifu nchini, Serikali imeanza mchakato wa uanzishwaji wa mfumo rasmi wa Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu ambapo Wizara kwa kushirikiana na Taasisi nyengine imeandaa andiko la dhana ya uanzishwaji wa Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya Binadamu (*DNA Database Concept Note*) na Mpango Kazi wa Utekelezaji (*Road Map*) kwa kushirikiana na Wataalam Wazalendo wa mifumo ya TEHAMA nchini kutoka Taasisi za Serikali ikiwemo Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Wakala wa Ufilisi na Udhanimi (RITA) na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).

Aidha, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kushirikisha wadau wengine muhimu wakiwemo vyombo vya Ulinzi na Usalama ili kupata maoni yao yatakayosaidia katika uanzishwaji na utekelezaji wa mfumo huo wa Kanzidata ya Taifa ya Vinasaba vya binadamu. Mfumo huu utaanza kutekelezwa baada ya taratibu hizi kukamilika.

Na. 142

**Kuwakamata Watu Wanaojihusisha na  
Vitendo vya Ushoga**

**MHE. KHATIBU SAID HAJI aliuliza:-**

Serikali katika kulinda heshima na utamaduni wa Taifa letu ilitoa tamko kuititia Naibu Waziri wa Afya kuchukua hatua kali kwa kuwakamata na kuwachukulia hatua wale wanaume wanaojihusisha na ushoga.

Je, ni mafanikio yapi yalipatikana katika zoezi hilo na mashoga wangapi wamepatikana na kuchukuliwa hatua?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipambana na vitendo vya ushoga kwa sababu ni kinyume na desturi na tamaduni za Kitanzania kushiriki mapenzi ya jinsia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2017 hadi mwaka huu wa 2020 jumla ya mashoga 39 walikamatwa na mashauri yao yako kwenye hatua mbalimbali za kisheria. Wapo ambao wamehukumiwa miaka 30 jela, wapo walioachiliwa huru kwa kukosekana kwa ushahidi na wengine ambaao upelevaze wa majalada yao umekamilika na majalada yapo kwa wakili wa Serikali (*State Attorney*) kwa ajili ya ushauri au maelekezo ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendea kupambana na vitendo hivyo vinavyodhalilisha utu wa Mtanzania. Nitoe wito kuitia Bunge lako Tukufu kwa wananchi wanaojihusisha na vitendo hivyo kuacha mara moja.

**NAIBU SPIKA: Katibu!**

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita mtoa hoja Mheshimiwa Spika alikuwa ameshatoa pole na kwa mujibu wa kanuni zetu, basi tunalazimika kufuata hicho, lakini Mheshimiwa Waziri pole sana kwa msiba mkubwa uliokupata. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2019/2020 na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2020/2021. Naomba pamoja na muhtasari nitakaousoma wa hotuba yangu, lakini hotuba yangu yote kuhusu taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2020/2021 iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii muhimu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunitfea kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuanzia tarehe 23 mwezi Januari mwaka 2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoiongoza Serikali ya Awamu ya Tano inayotekeleza Ilani ya CCM ambapo mafanikio mengi yamepatikana kutika Sekta mbalimbali. Ni wazi kuwa mafanikio haya yote yamepatikana kwa kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu nchini kupitia utendaji mzuri wa vyombo vyaya ulinzi na usalama. Naomba

nitoe rai kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali itikadi za aina yoyote tuendelee kuyaenzi mafanikio haya makubwa na kuendelea kushirikiana kwa pamoja katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ikiongozwa na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani na wajumbe wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa ushauri wa kuboresha mambo mbalimbali katika Wizara ikiwemo katika kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuwasilisha sasa maelezo ya mapitio ya utekelezaji wa majukumu na kazi za Wizara katika mwaka 2019/2020 na malengo ya mpango na bajeti kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya shilingi bilioni 921.24; kati ya fedha hizo shilingi bilioni 517.04 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 372.26 ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni 31.93 ni fedha za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 fedha zilizopokelewa na Wizara ni jumla ya shilingi bilioni 731.55. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.91 zilikuwa ni za miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 373.61 ni mishahara na shilingi bilioni 350.74 zilikuwa ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Wizara ilikuwa imokusanya jumla ya shilingi bilioni 248.4 ikilinganishwa na lengo la kukusanya shilingi bilioni 471.89 sawa na asilimia 53. Miongoni mwa sababu za kushuka kwa mapato ni upungufu wa vitendea kazi kwa ajili ya ufuatiliaji wa mapato yanayotokana na shughuli za Uhamiaji ambazo zinachangia asilimia 70 ya mapato yote ya Wizara. Ili kuimarisha ukusanyaji wa mpato hayo Serikali katika mwaka 2020/2021 imetenga

shilingi bilioni 1.17 kupitia Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya kununua magari sita na pikipiki 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu ya kazi zilizopangwa mwaka 2019/2020, Wizara imepata mafanikio mbalimbali ikiwemo kusajili na kutambuliwa kwa watu milioni 2,478,448 na hivyo kufanya jumla ya watu wote waliosajiliwa katika mfumo wa *NIDA* kufikia asilimia 86 ya lengo la usajili wa watu 25,237,954; pia tumefanikiwa kuwarejesha kwa hiari wakimbizi 9,875 wa Burundi; kupunguza msongamano Magerezani kwa kuwezesha wafungwa 2,973 kutumikia vifungo vyao nje ya magereza na kuokoa na kuwapa misaada wahanga 196 wa usafirishaji haramu wabinadamu; na kutolewa kwa *Passport* na hati nyininge za safari 395,903.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni kukamilika kwa nyumba 431 za makazi ya Jeshi la Polisi katika mikoa mbalimbali na kukamilika kwa majengo 12 ya ghorofa katika Gereza la Ukonga yenye uwezo wa kuchukua familia 172 za Askari Magereza, lakin pia kukamilika kwa Ofisi ya Idara ya Upenzelezi wa Makosa ya Jinai na Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Jijini Dodoma. Wizara pia imefanikiwa kupandisha vyeo Maafisa Wakaguzi na Askari 2,406 wa Jeshi la Polisi na 3,702 wa Jeshi la Magereza na 169 wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji na 815 wa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi; Jeshi hili kwa hushirikiana na jamii na wadau wengine ili kuhakikisha uhalifu wa aina zozote zile unazibitiwa. Ushirikiano huu umeiwezesha nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu. Katika kudhibiti uhalifu wa matumizi ya silaha, Jeshi la Polisi limefanya operesheni na kukamata silaha za aina mbalimbali 211 na risasi 531. Kupitia operesheni hizo jumla ya watuhumiwa 156 walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kesi zao zinaendelea. Vilevile Jeshi la polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vyao dola vimefanikiwa kukamata nyara za Serikali 1,963 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.97. Watuhumiwa 997

walifkishwa mahakamani na kesi zao zipo kwenye hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama barabarani inaendelea kuimarika kutokana na mikakati iliyowekwa na Jeshi la Polisi ambayo imesaidia kupunguza matukio ya ajali vifo na majeruhi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 matukio makubwa ya ajali barabarani yamepungua kwa asilimia 26 na ajali za kusababisha vifo zimepungua kwa asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa Ofisi na Vituo vya Polisi; Serikali imekamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 400, nyumba hizo zimejengwa katika mikoa mbalimbali na zilizinduliwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika Mkoa wa Geita tarehe 15 Julai, 2019 na Dodoma tarehe 22 Novemba, 2019. Aidha, katika kuunga mkono juhudhi za Mheshimiwa Rais wadau walijitokeza kuchangia ujenzi wa nyumba nyingine 31 katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar Jeshi la Polisi limeshirikiana na wadau katika ujenzi wa nyumba nne za Askari Kaskazini Pemba na nyumba mbili Kusini Pemba. Aidha, Kituo cha Polisi Nungwi, Daraja C kilichopo Kaskazini Unguja kimejengwa upya. Katika mwaka 2020/2021 jeshi la Polisi limepanga kujenga Kituo cha Polisi Mkokotoni, Kaskazini Unguja kitakachogharimu shilingi milioni 500. Ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari Buyekera unaokadiriwa kugharimu shilingi bilioni 1.4 na kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Mbalizi kwa gharama ya shilingi milioni 50 na kukamilisha ujenzi wa nyumba nne za kuishi familia nane za Askari Wilayani Meatu kwa gharama ya shilingi milioni 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi; kuanzia mwezi Agosti mwaka 2019, Shirika lilianza kutoa mafunzo ya umahiri wa utunzaji wa matumizi ya silaha za moto za kiraia kwa kampuni binafsi za ulinzi Jijini Dar es Salaam. Hadi kufikia mwezi Machi 2020 jumla ya Askari 972 wa Kampuni hizo walipata mafunzo hayo. Nichukue fursa hii

kuwataka wamiliki na watunzaji wote wa silaha za moto za kiraia nchini kuwasiliana na Makamanda wa Polisi wa Mikoa ili kupata utaratibu wa kuisajili na kuhudhuria mafunzo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2020/2021, Shirika litajihuisha na kutoa ulinzi katika shughuli za usafirishaji wa fedha na vitu vingine vyatya thamani kwa taasisi za fedha na kampuni za madini. Utekelezaji wa shughuli hizi ni katika kuimarisha usalama na ulinzi katika eneo hili la kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2020 kulikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusu 32,438 katika magereza yote nchini. Kati ya hao wafungwa ni 14,464 na mahabusu ni 17,974 ambaao ni asilimia tisa zaidi ya uwezo uliopo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902. Jeshi la Magereza limeendelea kupunguza msongamano wa wafungwa kwa kutumia taratibu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji wa makazi ya Ofisi na Mabweni ya Wafungwa; Serikali imekamilisha ujenzi wa majengo 12 ya ghorofa katika Gereza la Ukonga lenye uwezo wa kuchukua familia 172 za Askari Magereza na yameanza kutumika. Nyumba hizo zilizinduliwa rasmi tarehe 23 Januari, 2020 na Mheshimiwa Rais. Kwa dhati nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa juhudini kubwa anazotumia katika kuhakikisha kuwa nyumba hizo zinakamilika na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Kiwanda cha Samani Msalato; katika kuendeleza sera ya uchumi wa viwanda Serikali katika mwaka 2019/2020 imetoea shilingi milioni 820.41 kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Samani, Msalato Jijini Dodoma. Kiwanda hicho kitakapokamilika mwezi Julai, 2020 kitatengeneza samani kwa matumizi mbalimbali. Aidha, katika mwaka 2020/2021 Jeshi la Magereza litaanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi hilo Jijini Dodoma ambapo jumla ya shilingi bilioni 13.5 zimetengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Kujitosheleza kwa chakula unaendelea kutekelezwa ambapo katika mwaka 2019/2020 jumla ya hekari 5,608 zimelimwa. Kati ya hizo hekari 4,200 ni za mahindi, hekari 975 za mpunga na hekari 433 ni za maharage. Matarajio ni kuvuna mahindi tani 5,670, mpunga tani 1,463 na maharage tani 217. Kupitia mkakati huo ulioanza kutekelezwa mwaka 2018 umewezesha Magereza ya Arusha, Katai, Kitengule na Songwe kujitosheleza kwa mazao ya mahindi na maharage kwa asilimia 100. Magereza hayo yameweza kulisha pia magereza mengine mengi. Vilevile Gereza la Arusha limelisha kwa miezi sita jumla ya magereza 14 yaliyopo katika Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2021, Wizara kupitia Jeshi la Magereza itaendelea kusimamia utekelezaji wa mkakati huo ili kuhakikisha magereza yanaendelea kutoa chakula kwa wafungwa na mahabusu. Katika msimu wa mwaka 2020/2021, Jeshi la Magereza litalima hekari 9,000 kati ya hizo hekari 5,750 za mpunga, hekari 2000 za mahindi na maharage hekari 1,250. Matarajio ni kuvuna wastani wa tani 7,785 za mahindi na tani 3000 za mpunga na tani 625 za maharage.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Magereza lipo katika hatua za mwisho la ujenzi wa viwanda vitavu vya kampuni ya kutengeneza bidhaa za ngozi, viwanda hivyo vinajengwa katika Gereza la Kalanga Mjini Moshi kwa shilingi bilioni 9.63. Ujenzi huo umepangwa kukamilika kabla ya mwezi Julai, 2020. Vilevile shirika limepata kazi ya ukandarasi ya kujenga majengo ya Kiwanda cha Sukari cha Kampuni Hodhi ya Mkulazi. Shirika pia limepokea jumla ya shilingi bilioni 1.54 kutoka Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia na watu binafsi kwa ajili ya kutengeneza samani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, limefanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto katika maeneo 53,919 na magari 13,128. Kupitia ukaguzi huo shilingi bilioni 5.89 zilikusanywa. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linakamilisha taratibu za ununuzi wa magari matano ya

kuzima moto pamoja na vifaa vya uokoaji katika bajeti ya 2019/2020. Aidha, magari hayo yenye uwezo wa kubeba lita 5,000 za maji kila moja yatanunuliwa kutoka Shirika la Nyumbu Kibaha. Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Zimamoto na Uokoaji Jijini Dodoma umekamilika. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji, Wilaya ya Chato, Mkoani Geita na Chamwino Dodoma unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Uhamiaji. Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji imeendelea kutoa huduma za *Passport*, *VISA* na vibali vya ukaazi kupitia mfumo wa kielektroniki. Aidha, mfumo wa udhibiti wa mipaka wa kielektroniki umeanza kutumika kwenye Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vilivyopo Dar es Salaam, Kilimanjaro, Zanzibar pamoja na vituo vyote vya mipakani vya utoaji wa huduma kwa pamoja. Mfumo huu utasaidia kuimarisha usalama wa mipakani na nchi yetu pamoja na kuongeza udhibiti kwenye ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2021 Idara ya Uhamiaji itaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma na kukamilisha ujenzi wa Ofisi katika Mikoa ya Geita, Lindi, Manyara na Mtwara. Vilevile ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji utaanza katika Wilaya za Chato, Kyerwa, Mlele, Mufindi, Simanjiro na Rarya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Wizara imefanikiwa kuokoa na kusaidia wahanga 196 waliokuwa wakitumikishwa katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka za Vitambulisho vya Taifa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 *NIDA* imefanikiwa kusajili jumla ya wananchi 2,478,448 hivyo kufanya wananchi waliosajiliwa kufikia 21,823,026 kati ya lengo la kusajili watu 25,237,954 ifikapo Juni, 2020. Aidha, *NIDA* imetoa namba za utambulisho wa Taifa kwa watu 17,871,770 na imechapisha pamoja na kugawa kwa wananchi vitambulisho vya Taifa 6,103,222. Vilevile mashine mbili zenyе uwezo wa kuchapisha

vitambulisho 144,000 kwa siku zimenunuliwa na tayari zimefungwa. Mashine hizo zitasaidia kufikia lengo la Serikali la kuwapa wananchi vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za wakimbizi. Hadi kufikia Machi, 2020 Tanzania ilikuwa inahifadhi wakimbizi wapatao 293,710 kati ya hao, Warundi walikuwa ni 216,000; Wakongo 76,384; na 426 kutoka nchi nydingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako, naomba kutumia fursa hii kukanusha shutuma zinazotolewa na makundi mbalimbali kuwa Serikali ya Tanzania inawarejesha wakimbizi nchini kwao kwa ulazima. Aidha, napenda kuwahakikisha umma wa Watanzania na Jumuiya ya Kimataifa kuwa Serikali ya Tanzania katika kutekeleza zoezi hili imekuwa ikiwarudisha wakimbizi kwa hiari yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani. Nitumie fursa hii kumshukuru Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni kwa ushirikiano anaonipa katika kusimamia majukumu ya Wizara.

Aidha, niwashukuru kwa dhati Katibu Mkuu, Christopher Kadio na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Kailima Ramadhani kwa kusimamia vyema utekelezaji wa kazi za Wizara. Pia, nawashukuru Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Ni dhahiri kuwa, wakuu wa vyombo hivi wametoa mchango mkubwa katika kusimamia maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru familia yangu pamoja na wanangu kwani wamekuwa msaada mkubwa katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kiofisi. Aidha, niwashukuru sana Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe Naibu Spika kwa kunipa ushirikiano katika kipindi kigumu nilichokipitia wakati tulipompoteza baba yetu mpendwa, familia inawashukuru sana. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kutoka kwenye taasisi mbalimbali kwa ushirikiano walionipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru pia Mheshimiwa Rais, viongozi wote wa Kitaifa, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa dini, watumishi wa Serikali, ndugu, jamaa na marafiki na wananchi ambao wameshirikiana na mimi katika kunipa faraja katika msiba mzito wa marehemu baba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Katika mwaka 2020/2021, Wizara inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya Sh.488,569,880,319. Aidha, mapato yanayokusanywa na *NIDA* kuititia ada ya utambulisho yataanza kutolewa taarifa na Msajili wa Hazina badala ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama iliyoyokuwa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe bajeti ya jumla ya Sh.899,170,293,000 kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2020/2021. Kati ya fedha hizi, Sh.863,734,431,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Sh.382,269,678,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Sh.481,504,753,000 ni mishahara. Fedha za Maendeleo ni Sh.35,435,862,000. Kati ya fedha hizo, Sh.34,540,000,000 ni fedha za ndani na Sh.895,862,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE.  
GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE (Mb.), AKIWASILISHA  
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA  
MWAKA 2020/21 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2019/20 na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka 2020/21.

**2. Mheshimiwa Spika**, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuwasilisha

Hotuba hii muhimu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya kipekee kabisa namshukuru Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunitfea kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuanzia tarehe 23 Januari, 2020.

**3. *Mheshimiwa Spika*,** kwa dhati nampongeza Mhe. Rais kwa namna anavyoiongoza Serikali ya Awamu ya Tano inayosimamia utekelezaji wa llani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 - 2020, ambapo mafanikio mengi yamepatikana katika sekta mbalimbali. Mafanikio hayo yameendelea kuitangaza nchi yetu siyo tu katika Bara la Afrika bali Duniani kote. Ni wazi kuwa mafanikio hayo yamepatikana kwa kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu nchini kupitia utendaji mzuri wa Vyombo vyia Ulinzi na Usalama.

**4. *Mheshimiwa Spika*,** ninaomba nitoe Rai kwa wananchi na Waheshimiwa Wabunge wote bila kujali itikadi za aina yoyote, tuendelee kuyaenzi mafanikio haya makubwa na kuendelea kushirikiana kwa pamoja katika kuchangia maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

**5. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ambaao ni Makamu wa Rais, Mhe. Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa hekima kubwa katika kumsaidia Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongoza nchi yetu.

**6. *Mheshimiwa Spika*,** pia, nimshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwani amekuwa mstari wa mbele katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa llani ya CCM na maelekezo mbalimbali ya Mhe. Rais pamoja na kusimamia vema shughuli za Serikali ndani ya Bunge.

**7. Mheshimiwa Spika**, ninakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, akiwemo Kaimu Mwenyeekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Mhe. Salum Mwinyi Rehani (Mb.) na Wajumbe wa Kamati hiyo. Kamati hii imefanya kazi nzuri na kutoa ushauri wa kuboresha mambo mbalimbali ikiwemo kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2020/21.

#### **B. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA KAZI ZA WIZARA KATIKA MWAKA 2019/20 NA MALENGO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21**

##### **Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2019/20**

**8. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya **Shilingi 921,247,033,279** kati ya fedha hizo **Shilingi 517,040,341,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 372,268,278,000** ni za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 31,938,414,279** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo **Shilingi 21,500,000,000** zilikuwa ni fedha za ndani na **Shilingi 10,438,414,279** zilikuwa ni fedha za nje.

**9. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 fedha zilizopokelewa ni jumla ya **Shilingi 731,555,762,841.15**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 7,915,138,039.76** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 373,614,129,528.65** ni Mishahara na **Shilingi 350,026,495,272.74** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**10. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya mapato ya **Shilingi 471,893,927,000**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya **Shilingi 248,408,973,341.17** zilikuwa zimekusanywa sawa na **asilimia 53** ya lengo. Mionganini mwa sababu ya kushuka kwa ukusanyaji wa mapato ni upungufu wa vitendea kazi, hususan magari na pikipiki kwa ajili ya ufuatiliaji wa mapato yanayotokana na shughuli za uhamiaji, ambazo zinachangia

asilia 70 ya mapato yote yanayokusanywa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**11. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa mapato kutokana na shughuli za uhamiaji unaimarishwa, Serikali imeongeza fedha za Matumizi Mengineyo za Idara ya Uhamiaji kutoka **Shilingi 5,637,492,000** mwaka 2019/20 hadi **Shilingi 7,644,400,000** mwaka 2020/21. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,176,000,000** zitatumika kwa ajili ya kununua magari sita (6) na pilkipiki 20.

### **Mafanikio ya Wizara**

**12. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepata mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kusajiliwa na kutambuliwa kwa watu 2,478,448 na hivyo kufanya jumla ya watu wote wallosajiliwa katika mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kufikia 21,823,026; kuwarejesha kwa hiari yao Wakimbizi 9,875 wa Burundi; kupunguza msongamano magerezani kwa kuwezesha wafungwa 2,973 kutumikia vifungo vyao nje ya magereza; kuokoa na kuwapa misaada wahanga 196 wa usafirishaji haramu wa binadamu; na kutolewa kwa pasipoti na hati nytingine za safari 395,903 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali.

**13. Mheshimiwa Spika**, mafanikio mengine ni kukamilika kwa nyumba 431 za makazi ya Maafisa na Askari wa Jeshi la Polisi katika mikoa mbalimbali nchini; kukamilika kwa ujenzi wa maghorofa 12 katika Gereza Ukonga yenye uwezo wa kuchukua familia 172 za Askari Magereza; kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai Jijini Dodoma; na kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Jijini Dodoma.

**14. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imefanikiwa kuwapandisha vyeo Maafisa, Wakaguzi na Askari 2,406 wa Jeshi la Polisi, 3,702 wa Jeshi la Magereza, 169 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 815 wa Idara ya Uhamiaji. Aidha, mafunzo mbalimbali yametolewa ndani na nje ya nchi. Jumla ya Maafisa,

Wakaguzi, Askari na Watumishi Raia 5,470 wa Jeshi la Polisi; 1,593 wa Jeshi la Magereza, 372 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 838 wa Idara ya Uhamiaji.

### **Maeneo ya Kipaumbele kwa Mwaka 2020/2021**

**15. *Mheshimiwa Spika*,** maeneo ya vipaumbele ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2020/21 ni pamoja na: kudumisha usalama wa raia na mali zao; kuhakikisha uchaguzi mkuu unafanyika kwa amani na utulivu; kutoa mafunzo kwa Maafisa, Askari na Watumishi Raia na kuwapandisha vyeo katika ngazi mbalimbali; kununua vitendea kazi muhimu hususan magari; kuendelea na ujenzi wa makazi ya Askari na ofisi ikiwemo kuanza ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Magereza Jijini Dodoma.

**16. *Mheshimiwa Spika*,** maeneo mengine ya kipaumbele ni: kuendelea na usajili na utambuzi kwa lengo la kufikia idadi ya wananchi 27,796,983; kuandaa Sera ya Taifa ya Zimamoto na Uokoaji na Sera ya Taifa ya Uhamiaji na Uraia; kufanya marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Jumuiya, Sheria ya Zimamoto na Uokoaji na Sheria ya Uraia; kuendelea kupunguza msongamano magerezani kuititia taratibu na Sheria mbalimbali; kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kujitosheleza kwa Chakula wa Jeshi la Magereza; na kusimamia utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na mashirika ya uzalishaji mali ya Jeshi la Polisi na Magereza ili yatimize malengo ya uanzishwaji wake.

### **JESHI LA POLISI**

#### **Hali ya Usalama Nchini**

**17. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Polisi lina jukumu la kuhakikisha usalama wa watu na mali zao. Katika kutekeleza jukumu hili Jeshi la Polisi hushirikiana na jamii na wadau wengine ili kuhakikisha uhalifu wa aina zote unadhibitiwa. Ushirikiano huu umewezesha nchi yetu kuendelea kuwa katika hali ya amani na utulivu.

**18. *Mheshimiwa Spika*,** uhalifu wa makosa makubwa ya jinai yanayojumuisha makosa dhidi ya binadamu, maadili ya jamii

na kuwania mali umepungua. Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya makosa makubwa ya jinai 44,277 yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi nchini ikilinganishwa na makosa 45,574 yaliyopotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19, ambapo makosa 1,297 yamepungua sawa na **asilimia 2.8**.

**19. Mheshimiwa Spika**, kati ya makosa makubwa ya jinai 44,227 yaliyopotiwa kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya kesi 12,736 upelelezi wake ulikamilika na watuhumiwa walifikishwa mahakamani ambapo kesi 2,783 zilishinda, kesi 478 zilishindwa, kesi 113 ziliondolewa, kesi 9,362 bado zipo mahakamani. Aidha, kesi 2,476 hazikufikishwa mahakamani zilifungwa katika Vituo vya Polisi.

**20. Mheshimiwa Spika**, kesi 29,062 zipo katika hatua mbalimbali za upelelezi katika Vituo vya Polisi. Mionganini mwa kesi hizo kuna kesi kubwa zenye mahabusu 1,819 ikilinganishwa na kesi kubwa zenye mahabusu 5,788 kwa mwaka 2018/19. Hivyo, jumla ya kesi kubwa zenye mahabusu 3,969 zimepungua sawa na **asilimia 68.5**.

**21. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2018/19 kesi kubwa zenye mahabusu 5,788 ikilinganishwa na kesi kubwa zenye mahabusu 1,819 kuanzia Julai, 2019 hadi mwezi Machi, 2020. Hivyo, jumla ya kesi kubwa zenye mahabusu 3,969 zimepungua sawa na **asilimia 68.5**.

**22. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kesi zinapelelezwa kwa haraka, Jeshi la Polisi katika mwaka 2020/21 litaendelea kutoa mafunzo kwa wapelelezi, kuongeza idadi ya wapelelezi kwa kuangalia ikama ya Askari waliopo pamoja na kuongeza vitendea kazi vya kisasa.

**23. Mheshimiwa Spika**, ili kukamilisha usajili wa Maabara ya Uchunguzi wa Vinasaba (DNA), Kemikali na Sumu, Jeshi limewapeleka mafunzoni watumishi 15 katika masuala ya uendeshaji wa Maabara. Kati ya hao, tisa (9) ni Maafisa wa Jeshi la Polisi na sita (6) ni watumishi raia. Mafunzo ya ndani yalitolewa na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Pia, *Standard*

*Operating Procedures* mpya za Maabara husika zimeandaliwa na zimeanza kutumika.

**24. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Maabara inahitaji kuwa na vyumba vikubwa vya kutosha kwa ajili ya uchunguzi (*Sorting Screening, Extraction Amplification and Detection Rooms*). Utaratibu unaendelea kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maabara ili ifanye kazi kwa ufanisi zaidi.

**25. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara kuititia Jeshi la Polisi itaongeza vitendea kazi vya Maabara zote za Uchunguzi wa Kisayansi vikiwemo mitambo, magari, vitendanishi (*Reagents*), vifaa vya ukaguzi wa matukio (*Crime scene Kits*), vifaa vya kujikinga, pamoja na vifaa viwezeshejaji. Aidha, mafunzo ya ndani na nje ya nchi yatatolewa kwa ajili ya kuwajengea uwezo watendaji wa maabara ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

#### **Operesheni za Polisi za Kitaifa na Kimataifa za Kupambana na Uhali**

**26. Mheshimiwa Spika**, matukio ya uzagaaji wa silaha za moto hapa nchini yamekuwa ni kichocheo kikubwa cha uhali, hususan katika mikoa iliyopo pembezoni mwa nchi na ile inayozunguka hifadhi za Taifa. Sababu kubwa zinazochangia kuongezeka kwa matukio hayo ni wahamiaji haramu wanaoingia nchini wakiwa na silaha pamoja na uwindaji haramu unaoshawishi watu kujitengenezea silaha za kienyeji. Ili kukabiliana na tatizo hili Jeshi la Polisi limeendelea na mikakati mbalimbali pamoja na kuishirikisha jamii katika kutoa taarifa, kutumia taarifa za ki-intelijensia na kufanya operesheni maalum.

**27. Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uhali wa matumizi ya silaha, operesheni mbalimbali zimefanyika hapa nchini, ambapo silaha za aina mbalimbali 211 na risasi 531 zilikamatwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ikilinganishwa na silaha 351 na risasi 4,844 zilizokamatwa kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Silaha zilizokamatwa ni AK 47 (24), Shortgun (19), Rifle (8), Pistol (14), Uzigen (1), G3 (1)

na Magobole (144). Kupitia operesheni hizo, jumla ya watuhumiwa 156 walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kesi zao zinaendelea.

**28. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Vyombo Vingine vya Dola lilitanikiwa kukamata nyara za Serikali 1,963 za aina mbalimbali. Nyara zote zilizokamatwa ziliikuwa na uzitowa kilo 21,314 na gramu 457 zikiwa na thamani ya **Shilingi 3,973,405,567**. Makosa hayo yalihusisha watuhumiwa 997, katika yao wanaume 926 na wanawake 71. Watuhumiwa wote walifikishwa mahakamani na kesi zao zipo kwenye hatua mbalimbali.

**29. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) lilitanya operesheni iitwayo Usalama VI nchi nzima. Katika operesheni hiyo, pikipiki 6 na magari 10 yaliyobainika kuwa ni ya wizi yalikamatwa. Vilevile, vitu mbalimbali vilikamatwa vikiwemo: madini aina ya Carbon Kilo 275.6; dawa za kulevyta aina ya *Heroin* kete 160, *Cocaine* kete 13, Bhangi kilo 98.33 na Mirungi kilo 50.2. Jumla ya watuhimiwa 187 walikamatwa katika operesheni hiyo.

### **Hali ya Usalama Barabarani**

**30. Mheshimiwa Spika**, hali ya usalama barabarani imeendelea kuimarika kutokana na mikakati mbalimbali ya kudhibiti ajali iliyowekwa na Jeshi la Polisi. Hii inadhihirisha kuwa utii wa Sheria bila shuruti umeongezeka kwa madereva na makundi mengine ya watumiaji wa barabara hali iliyosababisha kupungua kwa matukio ya ajali, vifo na majeruhi.

**31. Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha matukio makubwa ya ajali za barabarani 1,920 yaliripotiwa kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ikilinganishwa na matukio 2,593 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/19. Hivyo, matukio 673 yamepungua sawa na **asilimia**

**26.** Aidha, ajali zilizosababisha vifo zilikuwa 850 ikilinganishwa na ajali 941 zilizotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19.

**32. Mheshimiwa Spika**, watu waliopoteza maisha kwa ajali za barabarani hadi kufikia mwezi Machi, 2020 walikuwa 1,084 ikilinganishwa na watu 1,216 mwaka 2018/19 sawa na **asilimia 11**. Vilevile, watu waliojeruhiwa katika ajali za barabarani walipungua kutoka 2,639 mwaka 2018/19 hadi 2,129 mwaka 2019/20 sawa na **asilimia 19.3**.

**33. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi limeanzisha Kampeni ya "Utatu" inayohusisha Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU) na Jamii inayolenga kudhibiti vitendo vya rushwa na kuongeza uadilifu wa Askari wa usalama barabarani. Vilevile, elimu kwa jamii imetolewa kwa njia mbalimbali juu ya matumizi sahihi ya barabara na madhara yatokanayo na kutotii Sheria za Usalama Barabarani.

**34. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi kuititia Kikosi cha Usalama Barabarani liliendesha operesheni mbalimbali za kusimamia Sheria za Usalama Barabarani. Kuititia operesheni hizo hatua kali zilichukuliwa kwa madereva waliokamatwa kwa makosa hatarishi kama vile ulevi, mwendo kasi, uendeshaji wa hatari na wanaosababisha ajali za vifo kwa kuwafungia leseni na kuwapeleka mahakamani.

**35. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 madereva 189 walifungiwa leseni wakiwemo madereva wa magari madogo ya binafsi 72, magari ya Serikali 8, magari ya abiria 83 na magari ya mizigo 26. Aidha, mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani yanashubiri ridhaa ya Serikali na baada ya hatua hiyo muswada husika utawasilishwa Bungeni.

**36. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara kuititia Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na Jeshi la Polisi itaendelea kudhibiti ajali za barabarani kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri

Ardhini na Mabalozi wa Usalama Barabarani. Vilevile, Baraza na Jeshi la Polisi wataendelea kutoa elimu kwa umma juu ya matumizi sahihi ya barabara na utii wa Sheria bila shuruti ili kuhakikisha barabara na watumiaji wanakuwa salama muda wote.

### **Mafunzo na Ajira katika Jeshi la Polisi**

**37. Mheshimiwa Spika**, mafunzo yametolewa ndani na nje ya nchi ili kuimarisha utendaji kazi wa watumishi wa Jeshi la Polisi. Jumla ya Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi Raia 5,470 wamepata mafunzo mbalimbali, kati ya hao 5,461 walipata mafunzo ndani ya nchi na 9 walipata mafunzo nje ya nchi. Aidha, Wakaguzi na Askari 1,821 wamepata mafunzo ya upandishwaji vyeo katika ngazi mbalimbali. Idadi hiyo ni kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020.

**38. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi limepanga kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari 9,465 pamoja na Watumishi Raia 25. Kati ya hao 9,051 watapata mafunzo ndani ya nchi kupitia Vyuo vya Polisi na 414 nje ya nchi kwa udhamini wa taasisi na nchi mbalimbali. Aidha, Jeshi la Polisi linatarajia kuajiri Askari 2,725.

### **Miradi ya Ujenzi wa Makazi, Ofisi na Vituo vya Polisi**

**39. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha Askari wanaishi katika mazingira bora, Jeshi la Polisi limekamilisha mradi wa ujenzi wa nyumba 400. Nyumba hizo zimejengwa katika mikoa mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar kwa gharama ya **Shilingi bilioni 10** zilizotolewa na Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Mhe. Rais alizindua nyumba hizo katika Mkoa wa Geita tarehe 15 Julai, 2019 na Dodoma tarehe 22 Novemba, 2019 katika eneo la Nzuguni.

**40. Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika kuunga mkono juhudzi za Mhe. Rais, wadau mbalimbali walijitokeza kuchangia ujenzi wa nyumba nyingine 31 ambazo zimekamilika. Nyumba hizi

zipo katika mikoa ya Lindi mbili (2), Manyara mbili (2), Mbeya nne (4), Morogoro tatu (3), Mtwara mbili (2), Mwanza sita (6), Pwani sita (6), Simiyu nne (4), Shinyanga moja (1) pamoja na Songwe moja (1) na zilijengwa kwa utaratibu wa Nguvu Kazi (*Force Account*).

**41. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Polisi kwa kutumia Mfuko wa Tuzo na Tozo limekamilisha ujenzi wa nyumba 31 za kuishi Askari mkoani Dodoma. Nyumba 30 zimejengwa eneo la Medeli East na nyumba moja (1) ya kuishi Inspeksa Jenerali wa Polisi imejengwa eneo la Uzunguni. Pia, kwa kutumia mfuko huo Jeshi la Polisi limekamilisha ujenzi wa ofisi ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai Jijini Dodoma.

**42. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, Jeshi la Polisi limekamilisha ujenzi wa majengo mawili (2) ya ghorofa tatu (3) kila moja ya kuishi familia 12 za Askari mjini Musoma mkoani Mara. Aidha, kazi za umaliziaji wa majengo mawili (2) ya kuhudumia familia 24 za Askari eneo la Mabatini Jijini Mwanza zinaendelea.

**43. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Polisi kwa upande wa Zanzibar pia limeendelea kushirikiana na wadau katika ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Jeshi limeendelea na ujenzi wa nyumba nne (4) Kaskazini Pemba na nyumba mbili (2) Kusini Pemba ambazo zimezekwa na kazi za umaliziaji zinaendelea.

**44. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, Jeshi la Polisi linaendelea na ujenzi wa nyumba tatu (3) za kuishi familia sita (6) za Askari ambazo zipo katika hatua mbalimbali katika maeneo ya: Mitwelo mkoani Lindi moja (1); Kisaki mkoani Morogoro moja (1); na Mtambaswala Mkoani Mtwara moja (1). Aidha, ukarabati wa nyumba tano (5) za kuishi familia 10 za Askari Mjini Morogoro umekamilika.

**45. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi hicho pia Jeshi limeendelea na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya Polisi Daraja "C". Vituo hivyo vinajengwa katika maeneo ya Kisaki Mkoa wa Morogoro, Lizaboni Mkoa wa Ruvuma na Majohhe Mkoa wa Dar es Salaam. Vilevile, Kituo cha Polisi Nungwi Daraja "C"

kilichopo Kaskazini Unguja kimejengwa upya. Ni matarajio ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa wadau wataendelea kusaidia ujenzi wa nyumba za kuishi Askari, Vituo vya Polisi na ofisi ili kupambana na uhalifu kikamilifu.

**46. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na UN – Women, UNFPA na UNICEF kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 limejenga ofisi 11 kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Dawati la Jinsia. Ofisi hizo ni Kawe (Dar es Salaam), Bunda, Butiama, Kiabakari na Serengeti (Mara), Buhigwe, Kakonko, Kibondo, Kigoma Mjini, Manyovu na Uvinza (Kigoma). Kati ya ofisi hizo, ofisi nane (8) zimezinduliwa na ofisi tatu (3) za Buhigwe, Manyovu na Uvinza uzinduzi utafanyika hivi karibuni. Aidha, ili kuendana na ujenzi wa Ofisi ya Dawati la Jinsia, UNFPA imejenga Kituo cha Polisi Buhigwe Daraja "C" kilichopo Mkoa wa Kigoma.

#### **Miradi ya Kipaumbele kwa mwaka 2020/21**

**47. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi limepanga kutekeleza miradi minne (4) ya kipaumbele ambayo ni: kumalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi Mkokotoni (Kaskazini Unguja) utakaogharimu **Shilingi 500,000,000**; ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari Buyekera (Kagera) unaokadiriwa kugharimu **Shilingi 1,400,000,000**; kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Mbalizi (Mbeya) kwa gharama ya **Shilingi 50,000,000**; na kukamilisha ujenzi wa nyumba nne (4) zenye uwezo wa kuhudumia familia nane (8) za Askari wilayani Meatu (Simiyu) kwa gharama ya **Shilingi 50,000,000**.

**48. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na wadau katika ujenzi wa nyumba nane (8) Kaskazini Pemba na 12 Kusini Pemba. Aidha, Jeshi kwa kushirikiana na wadau litakamilisha ujenzi wa nyumba ya kuishi Mkuu wa Polisi Wilaya ya Tabora, nyumba ya kuishi Mkuu wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Uyui, ujenzi wa vituo viwili (2) vya Polisi Daraja 'C' Wilaya ya Sikonge (Tabora) na Wilaya ya Tanganyika (Katavi).

**49. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Mgodi wa Uchimbaji wa Madini ya Dhahabu wa Geita (GGML) utajenga nyumba tano (5) zenye uwezo wa kuhudumia familia 10 za Askari. Pia, Mgodi huo utaanza ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita ikiwa ni utekelezaji wa makubaliano ya ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na mgodi huo.

#### **Ukarabati wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam**

**50. Mheshimiwa Spika**, ukarabati wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Dar es Salaam umekamilika kwa gharama ya **Shilingi 700,000,000** zilizotolewa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa bweni la ghorofa tatu la kuishi wanafunzi 180, jengo la ghorofa moja kwa ajili ya madarasa ya wanafunzi 140, ofisi za walimu na stoo moja ya kuhifadhiya vifaa mbalimbali. Kazi hizo zimefanyika kwa utaratibu wa *Force Account*.

#### **Kuungeza Rasilimali Fedha katika Jeshi la Polisi**

**51. Mheshimiwa Spika**, naishukuru Serikali kwa kulipatia Jeshi la Polisi fedha kiasi cha **Shilingi 71,070,773,423** nje ya bajeti, ambapo **Shilingi 69,570,773,423** zimetumika kulipa deni la wazabuni na watoa huduma, kugharamia mikutano ya *Eastern Africa Police Chiefs Co-operation Organization* (EAPCCO) na **Shilingi 1,000,000,000** zitatumika katika shughuli za operesheni za Jeshi la Polisi.

**52. Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imelipa jumla ya **Shilingi 457,800,000** zikiwa ni fidia kwa Askari 85 walioumia wakiwa kazini pamoja na wasimamizi wa mirathi kwa Askari nane (8) waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu ya Jeshi. Fedha hizo zimelipwa kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo.

#### **Upatikanaji wa Vitendea Kazi kwa Jeshi la Polisi**

**53. Mheshimiwa Spika**, Wizara imepata gari moja (1) kutoka Ofisi ya Rais Ikulu na pia inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kulipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi. Katika

kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020, Jeshi limepata msaada wa magari 19. Magari hayo yaliyotolewa na Kamati ya Usalama Barabarani magari manne (4), Ubalizi wa Ujerumani mawili (2), Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority – TRA) sita (6), Ubalizi wa Marekani matano (5) na watu binafsi mawili (2). Aidha, Jeshi limepokea pikipiki 24 kutoka kwa wadau mbalimbali. Vyombo hivyo vyaa usafiri vimesaidia kuimarisha utoaji huduma kwa wananchi.

### **Kushiriki katika Kuimarisha Ulinzi na Amani katika Nchi Mbalimbali**

**54. *Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi linaendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika kupeleka Askari kushiriki katika kuimarisha ulinzi na amani kwenye nchi mbalimbali. Ushirikiano huu unawezesha Jeshi la Polisi kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani.

**55. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya Maafisa, Wakaguzi na Askari 54 wamepelekwa kushiriki ulinzi wa amani katika nchi zifuatazo: Sudan (*United Nations Mission in Darfur – UNAMID*) Askari 20; Sudan Kusini (*United Nations Mission in South Sudan – UNMISS*) 16; Sudan – Abyei (*United Nations Interim Security Force for Abyei – UNISFA*) tisa (9); Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (*United Nations Organization Stabilization Mission in the Democratic Republic of Congo – MONUSCO*) watano (5); na Maafisa wanne (4) wanafanya kazi kwa muda maalum (*Secondment*) UN ambapo Abyei – Sudan (2), Ethiopia mmoja pamoja na Sudan – Khartoum mmoja (1).

**56. *Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi limeendelea kushiriki kwenye Jumuiya za Polisi za Kikanda na Kimataifa (*EAPCCO* na *SAPCCO*). Katika mwaka 2019/20 Jeshi lilikuwa mwenyeji wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Shirikisho la Wakuu wa Majeshi ya Polisi Ukanda wa Afrika Mashariki (*EAPCCO*) uliofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 22 hadi 25 Septemba, 2019.

**57. *Mheshimiwa Spika***, malengo ya Mkutano wa EAPCCO yalikuwa ni: kuimarisha ushirikiano wa pamoja baina ya

wanachama katika kupambana na uhalifu unaovuka mipaka; kutathmini na kuitisha utekelezaji wa maazimio ya pamoja katika kupambana na kupeleleza makosa yote yanayovuka mipaka (wizi wa magari, ugaidi na usafirishaji haramu wa binadamu); na nchi wanachama kuwa na operesheni na mafunzo ya pamoja kwa lengo la kupambana na uhalifu unaovuka mipaka.

**Usimamizi wa Nidhamu katika Jeshi la Polisi**

**58. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi linaendelea kuwatambua Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi Raia wanaotekeleza majukumu yao kwa nidhamu na ufanisi kwa kuwapa tuzo na zawadi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya Askari 84 walipewa tuzo na zawadi kwa utendaji mzuri na kuliletea sifa Jeshi la Polisi katika nyanja mbalimbali. Kati ya hao, Askari wanne (4) walipewa barua za pongezi, 56 walipewa vyeti na 24 walipandishwa vyeo mbalimbali.

**59. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Jeshi la Polisi limechukua hatua za kinidhamu kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari waliokiuwa Sheria ya Maadili ya Jeshi la Polisi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya watumishi wa Jeshi la Polisi 410 wa vyeo mbalimbali wamechukuliwa hatua za kinidhamu. Kati ya hao, Maafisa, Wakaguzi na Askari 78 wamefukuzwa kazi na 332 wamechukulia hatua na Mamlaka zao za kinidhamu ikiwemo kupewa barua ya onyo, barua ya tahadhari na kukatwa mshahara.

**60. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara itaendelea kusimamia maadili na kuchukua hatua za kinidhamu kwa Askari watakaokwenda kinyume na mwenendo mwema wa Jeshi la Polisi. Aidha, Askari watakaofanya kazi kwa ubora na uadilifu wataendelea kutambuliwa na kupongezwa kwa namna mbalimbali.

**SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA JESHI LA POLISI**

**61. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi kuititia Shirika lake la Uzalishaji Mali (Tanzania Police Force Corporation Sole - TPFCs)

linaendelea kujiimarisha kwa kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mapato. Katika mwaka 2019/20 Shirika lilianza kutoa mafunzo ya umahiri wa utunzaji na matumizi ya silaha za moto za kiraia kwa majoribio katika Jiji la Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Askari wa Kampuni Binafsi za ulinzi kuanzia mwezi Agosti, 2019. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya Askari 972 wa Kampuni hizo walipata mafunzo hayo.

**62. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika linakamilisha taratibu za kutoa mafunzo hayo nchi nzima kwa kuandaa miundombini wezeshi pamoja na kukamilisha mfumo wa TEHAMA utakaotumika kuratibu mafunzo hayo nchini. **Hivyo, nichukue fursa hii kuwataka Wamiliki na Watumiaji wote wa silaha za moto za kiraia nchini kuwasiliana na Makamanda wa Polisi wa Mikoa ili kupata utaratibu wa kujisajili na kuhudhuria mafunzo katika maeneo yao.**

**63. *Mheshimiwa Spika*,** mafunzo haya hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Silaha za Moto ya mwaka 2015 (*Firearms and Ammunition Control Act No. 02 of 2015*). Hivyo, kutohudhuria mafunzo hayo ni ukiukwaji wa Sheria na hufanya mmiliki kukosa sifa ya utumiaji wa silaha hizo. Aidha, wamiliki na watumiaji wa silaha za moto za kiraia wasiozingatia sheria husika, hawataruhusiwa kuhuisha vibali vyta umiliki na leseni za biashara zinazohusisha matumizi ya silaha hizo.

**64. *Mheshimiwa Spika*,** natumia fursa hii pia **kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kuwa Serikali kuititia Jeshi la Polisi itaanza kufanya ukaguzi wa vyeti vyta umahiri kwa wamiliki wote wa silaha za moto za kiraia nchini kuanzia mwaka 2020/21.**

**65. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika pia linamiliki Kampuni ya Ujenzi Daraja la IV, ambapo leseni ya biashara ya Kampuni hiyo imehuishwa kwa ajili ya kushiriki katika miradi ya ujenzi. Wizara inaamini kuwa Kampuni hiyo itashiriki vyema katika zabuni za ujenzi kwa kuwa itatumia wataalam wenye uzoefu wa kutosha wa Jeshi la Polisi ambao wameshiriki katika miradi mbalimbali ikiwemo ujenzi wa nyumba 400 za Jeshi la Polisi,

nyumba za kuishi familia 32 za Askari wa Jeshi la Polisi mkoani Arusha na Vituo vya Polisi (Chato, Kondoa, Manyoni, Nachingwea, Nyakato na Nungwi).

**66. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Shirika litajihusisha na kutoa ulinzi katika shughuli za usafirishaji wa fedha na vitu vingine vya thamani kwa Taasisi za Fedha na Kampuni za Madini. Utekelezaji wa shughuli hizi ni katika kusaidia (compliment) jukumu la msingi la Jeshi la Polisi la ulinzi wa watu na mali zao na hivyo kuimarisha usalama na ulinzi katika eneo hili la kiuchumi.

#### **JESHI LA MAGEREZA**

##### **Hali ya Ulinzi na Usalama Magerezani**

**67. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 kulikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusu 32,438 katika magereza yote nchini. Kati ya hao, wafungwa ni 14,464 na mahabusu 17,974 ambapo ni **asilimia 9** zaidi ya uwezo uliopo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902.

**68. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani, Jeshi la Magereza limeendelea kutumia utaratibu wa Parole ambapo wafungwa 92 waliachiwa huru. Pia, wafungwa 695 walitolewa magerezani kwa ajili ya kutumikia kifungo cha nje kwa utaratibu wa *Extra Mural Labour*. Aidha, wafungwa 5,533 waliachiwa huru kwa Msamaha wa Mhe. Rais na hivyo kufanya jumla ya wafungwa wote walioachiliwa huru hadi mwezi Machi, 2020 kufikia wafungwa 6,320.

#### **PROGRAMU YA ADHABU MBADALA YA KIFUNGO CHA GEREZANI**

**69. Mheshimiwa Spika**, Programu ya Adhabu Mbadala ya Kifungo cha Gerezani husaidia kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani na kuzipatia Taasisi za Serikali nguvukazi ya wafungwa badala ya kuajiri vibarua. Programu hii inasimamiwa na Wizara kuititia Idara ya Huduma za Uangalizi.

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 uchunguzi wa kijamii (*Social enquiries*) ulifanyika na taarifa 3,175 ziliwasilishwa mahakamani kwa ajili ya maamuzi ya kuwaweka wafungwa kwenye vifungo nya nje. Kupitia taarifa hizo, jumla ya wafungwa 2,186 walinufaika na programu ya adhabu mbadala ya kifungo cha gerezani ambapo wanaume walikuwa 1,760 na wanawake 426.

**70. Mheshimiwa Spika**, uwepo wa wafungwa hao nje ya magereza umefanikisha kuokoa jumla ya **Shilingi 1,128,600,000** ambazo zingetumika kwa chakula, kwa wastani wa **Shilingi 2,500** kwa mfungwa kwa siku moja. Aidha, wafungwa hao kufanya kazi kwenye Taasisi za Umma kumeokoa jumla ya **Shilingi 1,751,360,000** ambazo zingetumika kuwalipa vibarua kwa kufanya kazi hizo kwa malipo ya **Shilingi 4,000** kwa kibarua kwa siku. Pia, wafungwa 2,106 walimaliza kutumikia vifungo vyao nje ya magereza na kuwa rala wema.

**71. Mheshimiwa Spika**, vilevile, elimu ilitolewa kuhusu Sheria ya Probesheni na Ujenzi wa Tabia, Sura 247 na Sheria ya Huduma kwa Jamii, Sura 291 katika Mikoa ya Arusha, Geita, Iringa, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Mtwara, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora na Tanga.

**72. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepanga kuwasimamia na kuwafuatilia wafungwa 5,000 wanaotarajiwa kutumikia vifungo vyao nje ya magereza. Katika kutimiza jukumu hilo, Wizara itatembelea Mahakama na Magereza kwa ajili ya kusaili wafungwa wenye sifa na kuwapangia wafungwa hao kutekeleza adhabu zao kwenye Taasisi za Umma.

**73. Mheshimiwa Spika**, kazi nyininge ambazo zitafanyika ni kuandaa taarifa za Uchunguzi wa Kijamii, kuandaa programu za urekebishaji, kufanya ukaguzi kwenye Taasisi wanazofanya kazi wafungwa wanaotumikia adhabu zao nje ya magereza, kukagua utekelezaji wa shughuli za huduma za uangalizi katika mikoa mbalimbali na kutoa mafunzo kwa wadau muhimu wa Wizara pamoja na kufanya vikao nya Kamati ya

Kitaifa ya Huduma kwa Jamii. Kazi hizo zinatarajiwa kugharimu kiasi cha **Shilingi 1,245,586,000**.

### **Kuboresha Makazi ya Watumishi wa Jeshi la Magereza na Mabweni ya Wafungwa**

**74. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imekamilisha ujenzi wa maghorofa 12 katika Gereza Ukonga yenyewe uwezo wa kuchukua familia 172 za Askari Magereza na yameanza kutumika. Nyumba hizo zilizinduliwa rasmi tarehe 23 Januari, 2020 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kwa dhati nimshukuru Mhe. Rais kwa juhudini kubwa alizozitumia katika kuhakikisha kuwa nyumba hizo zinakamilika na kuanza kutumika.

**75. *Mheshimiwa Spika***, vilevile, Jeshi la Magereza linaendelea na ujenzi wa nyumba 482 kwa kutumia rasilimali zinazopatikana maeneo ya magereza unaendelea katika magereza yote nchini na upo katika hatua mbalimbali. Aidha, Jeshi la Magereza limejenga bweni moja (1) katika Gereza Kwitanga na kukamilisha mabweni manne (4) ya kulala wafungwa katika Gereza Segerea. Hivyo, kuongeza jumla ya nafasi 246 za kuhifadhi wafungwa. Aidha, Jeshi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali linaendelea na ujenzi wa mabweni 10 yenyewe uwezo wa kuhifadhi jumla ya wafungwa 865 katika magereza ya Kwitanga moja (1), Geita matatu (3), Sumbawanga matatu (3), Chunya moja (1), Kyela moja (1) na Kambi Mkwaluni mkoani Songwe moja (1). Ujenzi huo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

### **Kuimarisha Shughuli za Viwanda**

**76. *Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza sera ya uchumi wa viwanda, Serikali katika mwaka 2019/20 imetoea **Shilingi 820,410,355.88** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kiwanda cha Samani Msalato Jijini Dodoma. Ujenzi wa Kiwanda hicho unaendelea na kitakapokamilika mwaka 2020/21 kitatengeneza samani kwa matumizi ya ofisi, maeneo ya biashara na nyumba za makazi. Ujenzi huo unatarajiwa kukamilika baada ya miezi minne tangu ulipoanza tarehe 3 Machi, 2020.

## **Ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi la Magereza**

**77. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Magereza litaanza ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Jeshi hilo Jijini Dodoma. Ujenzi huo ni utekelezaji wa agizo la Serikali la kuhamia Dodoma. Jumla ya **Shilingi 13,500,000,000** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya ujenzi huo.

### **Kujitosheleza kwa Chakula cha Wafungwa na Mahabusu**

**78. Mheshimiwa Spika**, katika kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kujitosheleza kwa Chakula cha wafungwa na mahabusu kwa mwaka 2019/20 jumla ya ekari 5,608 za mazao makuu ya chakula zimelimwa. Kati ya hizo, ekari 4,200 ni za mahindi, ekari 975 za mpunga na ekari 433 ni za maharage. Matarajio ni kuvuna mahindi tani 5,670, mpunga tani 1,463 na maharage tani 217.

**79. Mheshimiwa Spika** kupitia juhudzi za kujitosheleza kwa chakula zilizoanza mwaka 2018 zimewesha Magereza ya Arusha (Arusha), Kitai (Ruvuma), Kitengule (Kagera) na Songwe (Mbeya) kujitosheleza kwa mazao ya mahindi na maharage kwa **asilimia 100**. Magereza hayo yameweza kuzalisha ziada na kulisha magereza mengine, ambapo Gereza Arusha limelisha kwa miezi sita (6) magereza matatu (3) yaliyopo mkoa huo, magereza manne (4) ya Mkoa wa Kilimanjaro na magereza nane (8) Mkoa wa Tanga.

**80. Mheshimiwa Spika**, Gereza Kitai limelisha magereza sita (6) ya Mkao wa Ruvuma, Magereza matano (5) ya Mkao wa Lindi na Magereza matano (5) ya Mkao wa Mtwara. Gereza Kitengule limelisha Magereza nane (8) ya Mkao wa Kagera, Magereza manne (4) ya Mkao wa Geita na Magereza mawili (2) Mkao wa Shinyanga. Gereza Songwe limelisha Magereza matano (5) ya Mkao wa Mbeya na Magereza matatu (3) ya Mkao wa Songwe.

**81. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Gereza Mollo liliopo Mkao wa Rukwa limeweza kujitosheleza kwa zao la mahindi kwa **asilimia 100** na ziada kulisha Magereza matatu (3) yaliyopo Mkao huo na Magereza mawili (2) yaliyopo Mkao wa Katavi.

Magereza ya Isupilo (Iringa) na Ludewa (Njombe) yamezalisha mahindi na kujitosheleza kwa **asilimia 100** na kulisha magereza mengine matano (5) yaliyopo ndani ya mikoa hiyo. Aidha, Magereza ya Idete na Kiberege yameweza kujitosheleza kwa zao la mpunga kwa **asilimia 100**.

**82. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuititia Jeshi la Magereza itaendelea kusimamia utekelezaji wa mkakati huo ili kuhakikisha lengo la kujitosheleza kwa chakula cha wafungwa na mahabusu katika magereza yote linafikiwa. Aidha, matrektta mapya 26 yalinunuliwa na mawili (2) yalitolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Matrektta hayo yatasaidia kuongeza uwezo wa kulima katika magereza mbalimbali.

**83. Mheshimiwa Spika**, katika msimu wa 2020/21 Jeshi la Magereza litalima ekari 9,000 za mazao mbalimbali. Ekari hizo zitalimwa mahindi ekari 5,750, mpunga ekari 2,000 na maharage ekari 1,250. Matarajio ni kuvuna mahindi tani 7,785, mpunga tani 3,000 na maharage tani 625.

**84. Mheshimiwa Spika**, shughuli za kuendeleza kilimo cha zao la chikichi katika Gereza Kwitanga, mkoani Kigoma zinaendelea. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya ekari 600 zimeandaliwa na miche 23,000 iliyopo kwenye kitalu inatarajiwa kupandwa ifikapo mwezi Oktoba, 2020. Miche mingine inaendelea kuandaliwa na itapandwa kwenye eneo la ekari 6,000. Katika bajeti ya mwaka 2020/21 Serikali imetenga **Shilingi 31,600,000** kwa ajili ya kuhudumia vitalu hivyo na kuwezesha upandaji wa miche kwenye shamba.

#### **Mafunzo na Ajira kwa Watumishi wa Jeshi la Magereza**

**85. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya Maafisa na Askari 1,537 walipata mafunzo ya uongozi wa kijeshi katika Vyuo vya Magereza na watumishi 951 walihitimu mafunzo ya taaluma mbalimbali katika vyuo vya ndani na nje ya Jeshi.

**86. Mheshimiwa Spika**, Jeshi linatarajia kuajiri askari 685 wenyе fani mbalimbali watakaopatiwa mafunzo ya awali katika Chuo cha Magereza Kiwira (Mbeya). Pia, Jeshi linatarajia kutoa mafunzo ya uendeshaji wa Magereza na Taaluma ya Urekebishaji kwa Maafisa na Askari 3,270 katika ngazi mbalimbali za uongozi.

**Ushiriki wa Ulinzi wa Amani chini ya Umoja wa Mataifa na Mahusiano ya Kikanda**

**87. Mheshimiwa Spika**, jumla ya Askari 17 wa Jeshila Magereza wako nchini Seychelles kwa ajili ya kushirikiana na kubadilishana uzoefu katika masuala ya kikazi. Aidha, Askari wawili (2) wapo nje ya nchi wakitekeleza jukumu la kulinda amani katika nchi za Sudan Kusini na Sudan (Darfur).

**Kuboresha upatikanaji wa Vitendea Kazi kwa Jeshi la Magereza**

**88. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utendaji, Jeshi la Magereza linatarajia kununua magari sita (6) kwa ajili ya shughuli za utawala. Jumla ya **Shilingi 1,350,000,000** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya ununuzi wa magari hayo.

**SHIRIKA LA MAGEREZA**

**89. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Magereza (Prisons Corporation Sole – PCS) lipo katika hatua za mwisho za ujenzi wa viwanda vitatu (3) vya Kampuni ya Kutengeneza Bidhaa za Ngozi (Karanga Leather Industries Company Limited). Viwanda hivyo vinajengwa katika eneo la Gereza Karanga Mjini Moshi kwa gharama ya **Shilingi 9,637,282,548.00**. Ujenzi huo umepangwa kukamilika kabla ya mwezi Juni, 2020. Aidha, Shirika limepata zabuni ya ujenzi wa Kiwanda cha Kuchakata Ngozi ambacho ni sehemu ya Viwanda vya Kampuni hiyo. Gharama za ujenzi zinakadirwa kufikia **Shilingi 18,181,915,215.50**. Ujenzi utaanza mwezi Aprili, 2020 na utakamilika baada ya miezi nane (8).

**90. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Shirika la Magereza limepata kandarasi ya kujenga majengo mbalimbali ya Kiwanda cha Sukari cha Kampuni Hodhi ya Mkulazi. Ujenzi huo unaendelea

katika eneo la Gereza Mbigiri na unahusisha ujenzi wa majengo ya utawala, nyumba za makazi, zahanati na uzio. Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa majengo hayo ni kama ifuatavyo: Zahanati imefikia hatua ya kuezeka; na majengo ya utawala na nyumba za makazi yapo katika hatua ya kujenga ukuta. Zabuni hiyo ina thamani ya **Shilingi 2,345,356,633.65** na kazi za ujenzi zinatarajiwaa kukamilika mwezi Juni, 2020.

#### **Viwanda vya Samani**

**91. Mheshimiwa Spika**, Shirika pia limepokea jumla ya **Shilingi 1,548,046,829** kutoka Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia na watu binafsi kwa ajili ya kutengeneza samani za aina mbalimbali. Samani hizo zimetengenezwa katika viwanda vilivyopo katika Magereza ya Ukonga (Dar es Salaam), Uyui (Tabora) na Arusha (Arusha) na kukabidhiwa kwa wahusika. Katika mwaka 2020/21 Shirika litaendelea kutengeneza samani zenye ubora wa hali ya juu kwa ajili ya wadau mbalimbali.

#### **Viwanda vya Chumvi**

**92. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Magereza limefanikiwa kujenga Kiwanda cha Kuchakata Chumvi katika Mradi wa Chumvi Bagamoyo mkoani Pwani. Kiwanda hicho kimegharimu **Shilingi 30,890,000** ikiwa ni gharama za ujenzi na kununua mashine mbalimbali. Taratibu za ununuza wa mashine ya kukausha chumvi zinaendelea sambamba na kukamilisha usajili katika Mamlaka za Udhibiti. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 720 za chumvi kwa mwaka.

**93. Mheshimiwa Spika**, shughuli za uzalishaji wa chumvi zinaendelea katika Gereza Lilungu Mkoani Mtwara. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya tani 309 zilizalishwa na kuuzwa, ambapo mapato ya **Shilingi 30,900,000** yalipatikana. Matarajio kwa mwaka 2020/21 ni kuzalisha tani 640 zenye thamani ya **Shilingi 68,500,000**.

#### **Kiwanda cha Kuchakata Maziwa**

**94. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeanza ujenzi wa Kiwanda cha kuchakata maziwa katika mradi wa ng'ombe wa

maziwa (Kingolwira Prison Farm - KPF) uliopo Gereza Mtego wa Simba mkoani Morogoro. Jengo la kiwanda limefikia **asilimia 80**. Shughuli za ujenzi zinatarajia kugharimu kiasi cha **Shilingi 122,906,200**. Lengo ni Kiwanda hicho kuanza uzalishaji mwaka 2020/21.

### **Karakana ya Kutengeneza Magari**

**95. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Magereza limefanikiwa kusajili karakana ya kutengeneza magari iliyopo Ukonga Jijini Dar es Salaam. Karakana hiyo imejumuishwa kwenye miradi ya Shirika kwa Tangazo la Serikali Na. 680 la tarehe 16 Agosti, 2019. Kazi za utengenezaji magari zilianza mwezi Disemba, 2019. Shirika lipo katika majadiliano na Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) kwa ajili ya kutengeneza magari ya Shirika hilo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

### **Kazi za Kutumia Nguvu Kazi**

**96. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Magereza limepata usajili kutoka Bodi ya Usajili wa Wakandarasi wa kufanya shughuli zinazohusisha matumizi ya nguvu kazi katika barabara (*Labour Based Road Works*). Kazi hizo ni pamoja na kusafisha barabara, kukata miti, kufyeka nyasi na kuzibua mitaro ya barabarani. Huduma hiyo inatolewa nchi nzima kuititia Ofisi za Wakuu wa Magereza.

### **Usajili wa Kampuni ya Ulinzi**

**97. Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha usalama katika miradi mikubwa, Shirika linakamilisha taratibu za usajili wa Kampuni ya Ulinzi itakayojulikana kwa jina la SHIMA GUARD. Hatua iliyofikiwa sasa ni kufanya usajili wa kampuni ya ulinzi na kuandaa mpango wa biashara. Kazi hizo zinatarajiwaa kukamilika mwezi Juni, 2020. Kampuni hiyo pia itatoa huduma za ulinzi kwa Taasisi, Mashirika na Watu Binafsi.

### **Udhhibitii wa Makusanyo**

**98. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Magereza limefanikiwa kuingiza miradi yake yote kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Mapato ya Serikali (*Government Electronic Payment Gateway - GePG*). Aidha, Shirika limeanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kihasibu unaojulikana kwa jina la "Prisons

*Corporation Sole Accounting System".* Mfumo huo unawezesha upatikanaji wa taarifa za mapato kutoka katika miradi yote ya Shirika. **Natoa rai kwa wateja wanaopata huduma katika Miradi ya Shirika kuhakikisha wanapewa stakabadhi za malipo za kielektroniki kwa kutumia mfumo huo.**

### **JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**99. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuokoa maisha ya watu na mali zao. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Jeshi limefanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto katika maeneo 53,919 na magari 13,128. Kupitia ukaguzi huo, kiasi cha **Shilingi 5,892,180,000** kilikusanywa kutokana na tozo za majengo na magari.

**100. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na majanga, Jeshi limeshiriki kuzima moto na kufanya uokoaji katika matukio 2,204 ambayo kama yasingedhibitiwa yangeweza kuleta madhara makubwa kwa jamii. Baadhi ya matukio hayo ni moto ulitokea katika: lori la mafuta eneo la Msamu mkoani Morogoro; matanki ya mafuta ya Lake Oil eneo la Kigamboni Jijini Dar es Salaam; pamoja na Masoko yaliyopo maeneo ya Makoroboi Jijini Mwanza, Tegeta Nyuki Jijini Dar es Salaam na Samunge Jijini Arusha.

**101. Mheshimiwa Spika,** ili kupunguza matukio ya moto nchini, katika mwaka 2019/20 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na utoaji elimu kwa umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo vipindi vya luninga 36 na vipindi vya redio 306. Pia, elimu hiyo imekuwa ikitolewa katika maeneo mbalimbali yenye mkusanyiko mkubwa wa watu. Aidha, katika kukabiliana na matukio ya moto kwenye shule za msingi na sekondari, Jeshi limefanikiwa kufungua Klabu za Zimamoto katika shule 431. Elimu kwa umma itaendelea kutolewa katika mwaka 2020/21 kwa lengo la kuongeza uelewa zaidi kuhusu tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga mengine.

### **Kuboresha Upatikanaji wa Vitendea Kazi**

**102. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linakamilisha taratibu za ununuzi wa magari matano (5) ya kuzima moto pamoja na vifaa vya uokoaji kupitia bajeti ya mwaka 2019/20. Magari hayo yenye uwezo wa kubeba lita 5,000 za maji kila moja yatanunuliwa kutoka Shirika la Nyumbu Kibaha (Tanzania Automotive Technology Centre – TATC). Katika mwaka 2020/21 Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imepanga kununua magari matatu (3) ya kuzima moto kwa gharama ya **Shilingi 2,250,000,000**.

**103. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Shirika hilo limekamilisha matengenezo ya magari manne (4) ya kuzima moto yaliyokuwa yameharibika. Aidha, katika mwaka 2020/21 kupitia Shirika hilo, magari ya kuzima moto 23 kutoka mikoa mbalimbali yatatengenezwa. Kukamilika kwa matengenezo ya magari hayo kutasaidia kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji nchini. Vilevile, Jeshi hilo limepata msaada wa boti moja (1) ya uokoaji na vifaa mbalimbali vya kuzima moto na uokoaji kutoka Serikali ya Ujerumani.

### **Ujenzi wa Ofisi na Vituo vya Zimamoto na Uokoaji**

**104. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekamilisha ujenzi wa Jengo la Makao Makuu Jijini Dodoma. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Chato mkoani Geita upo katika hatua za ukamilishaji. Katika mwaka 2020/21 Jeshi limetenga kiasi cha **Shilingi 1,250,000,000** kwa ajili ya kujenga Kituo cha Zimamoto na Uokoaji wilayani Chamwino mkoani Dodoma.

### **Mafunzo, Ajira na Upandishwaji Vyeo kwa Watumishi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**105. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20 Maafisa na Askari 372 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wamepatiwa mafunzo ya uzimaji moto na uokoaji ndani na nje ya nchi. Kati ya hao Maafisa na Askari 369 wamepata mafunzo ndani ya nchi na Maafisa watatu (3) wamepata mafunzo katika nchi za Ujerumani (2) na Uganda (1). Vilevile, Jeshi limefanikiwa kuwapandisha vyeo Maafisa na Askari 169 katika ngazi mbalimbali.

**106. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimaliwatu, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kuwapandisha vyeo Maafisa na Askari 1,311 na kuajiri askari wapya 501 katika mwaka 2020/21. Askari hao watakaoajiriwa watapatiwa mafunzo ya awali ya kuzima moto na uokoji katika Chuo cha Zimamoto na Uokoaji kilichopo Chogo (Handeni) mkoani Tanga.

#### **IDARA YA UHAMIAJI**

#### **Utekelezaji wa Mradi wa Uhamiaji Mtandao**

**107. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuitia Idara ya Uhamiaji inaendelea kutoa huduma kuitia mfumo wa kielektroniki (*e-Immigration*). Kuitia mfumo huo huduma za pasipoti, viza na vibali vya ukaazi zinaendelea kutolewa. Aidha, Mfumo wa Udhhibit wa Mipaka wa Kielektroniki (*e-Border Management Control System*) umeanza kutumika kwenye Viwanja vya Ndege vya Kimataifa vilivypopo Dar es Salaam, Kilimanjaro na Zanzibar pamoja na Vituo vyote vya Mipakani vya Utoaji Huduma kwa Pamoja (*One Stop Border Posts – OSBPs*). Mfumo huu unasaidia kuimarisha usalama wa mipaka ya nchi yetu pamoja na kuongeza udhibiti kwenye ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**108. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara itaendelea kutumia mifumo ya kielektroniki kutoa huduma zake zote za kiuhamiaji. Mifumo hiyo imeunganishwa na Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji Mapato ya Serikali (GePG) na itasaidia kudhibiti ukusanyaji wa mapato yatokanayo na huduma hizo.

#### **Hali ya Usalama Mipakani**

**109. Mheshimiwa Spika**, Wizara kuitia Idara ya Uhamiaji imeendelea kuwawezesha wageni kuingia na kutoka nchini. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 wageni 1,158,022 waliingia nchini na Wageni 1,048,149 walitoka nchini. Aidha, jumla ya wageni 361 walizuiliwa kuingia nchini kutoptana na sababu za kiusalama na kutokidhi vigezo mbalimbali vya kiuhamiaji.

### **Misako, Doria na Ukaguzi**

**110. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Idara ya Uhamiaji iliendelea kufanya misako, doria na ukaguzi katika sehemu mbalimbali kwa lengo la kudhibiti wahamiaji haramu. Kupitia zoezi hilo, jumla ya wahamiaji haramu 11,187 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikiwemo kuondolewa nchini kwa wahamiaji haramu 7,825.

**111. *Mheshimiwa Spika*,** kati ya wahamiaji haramu hao 1,389 ni Waethiopia waliorudishwa nchini kwao baada ya kumaliza vifungo katika Magereza mbalimbali. Zoezi la kuwarudisha nchini mwao lilifanyika kwa ushirikiano kati ya Serikali, International Organization for Migration (IOM) na Ubalozi wa Ethiopia nchini Tanzania. Aidha, Watanzania 578 waliokwenda nje ya nchi kinyume na taratibu za kiuhamiaji walirudishwa nchini. Zoezi husika litaendelea kufanyika kwa mwaka 2020/21 ili kuhakikisha taratibu za kiuhamiaji zinazingatiwa.

### **Usajili wa Wahamiaji Walowezi**

**112. *Mheshimiwa Spika*,** kumekuwepo na wahamiaji walowezi kutoka nchi jirani waliopo katika maeneo mbalimbali nchini. Walowezi hao wamekuwa wakishiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii kama Raia wa Tanzania. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya Walowezi 49,502 walitambuliwa na kusajiliwa na Idara ya Uhamiaji. Katika mwaka 2020/21 zoezi la kuwatambua na kuwasajili wahamiaji walowezi katika mikoa yote nchini litaendelea ili kuwapatia vibali stahiki.

### **Pasipoti na Hati Nyingine za Safari**

**113. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali iliziondoa rasmi pasipoti za zamani kwenye matumizi tarehe 31 Januari, 2020. Lengo ni kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anayehitaji kusafiri nje ya nchi anatumia pasipoti ya kieletroniki. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya Pasipoti 213,035 zilitolewa kwa Watanzania kwa mchanganuo ufuatao: Pasipoti za Kibalozi ni 984; Pasipoti za Kiutumishi ni 248; na Pasipoti za Kawaida ni 211,803. Kati ya hizo, pasipoti 15,598 zilitolewa kupitia ofisi za Balozi zetu nje ya nchi. Idadi ya pasipoti zote

zilizotolewa imeongezeka kwa **asilimia 189** ikilinganishwa na jumla ya pasipoti 73,416 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2018/19.

**114. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji pia ilitoa Hati za Dharura za Safari 182,868 katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ikilinganishwa na Hati za Dharura za Safari 167,793 zilizotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2018/19. Hivyo, Hati za Dharura za Safari 15,075 zimeongezeka sawa na **asilimia 9**. Ongezeko hilo limetokana na kuimarishe kwa Mfumo wa utoaji Hati za Dharura kwa njia ya kielektroniki. Katika mwaka 2020/21 pasipoti na hati nyingine za safari kwa Raia wa Tanzania zitaendelea kutolewa ili kuwawezesha kusafiri nje ya nchi.

#### **Viza na Vibali vya Ukaazi kwa Wageni**

**115. Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya Viza 335,043 zilitolewa kwa Wageni walioingia nchini. Viza hizo ziliikuwa ni kwa ajili ya matembezi 314,474, biashara 20,045 na shughuli za kidiplomasia 524. Aidha, jumla ya vibali vya ukaazi 14,202 (daraja "A" 1,964; daraja "B" 8,644; na daraja "C" 3,594) vilitolewa kwa wageni wakaazi. Pia, jumla ya Hati za Mfuasi 2,078 na Hati za Msamaha 1,624 zilitolewa katika kipindi husika. Katika mwaka 2020/21 viza, vibali na hati husika zitaendelea kutolewa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za uhamiaji.

#### **Wageni Walioomba na Kupewa Uraia wa Tanzania**

**116. Mheshimiwa Spika**, Raia wa nchi mbalimbali waliotimiza vigezo vya kisheria wamepewa Uraia wa Tanzania. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya wageni 87 walipewa Uraia wa Tanzania kutoka katika nchi za Afganistan mmoja (1), Afrika Kusini wawili (2), India (46), Italia wawili (2), Kenya (10), Lebanon wawili (2), Pakistan saba (7), Rwanda wawili (2), Somalia mmoja (1), Uganda mmoja (1), Uingereza wanne (4), Yemeni nane (8) na mmoja (1) ambaye hakuwa na uraia wa nchi yoyote (Stateless).

## **Watanzania Waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine**

**117. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya Watanzania 26 waliukana Uraia wa Tanzania baada ya kupata Uraia wa Mataifa mengine. Mataifa hayo ni Botswana mmoja (1), Canada mmoja (1), Hong Kong mmoja (1), India watano (5), Kenya watatu (3), Marekani watano (5), Morocco mmoja (1), Rwanda mmoja (1), Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) mmoja (1), Uganda mmoja (1), Uingereza watatu (3), Ujerumani mmoja (1), Yemen mmoja (1) na Zambia mmoja (1). Hivyo, kupoteza hadhi ya kuwa Raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Sura, 357 Rejeo la 2002.

### **Ujenzi wa Makazi na Ofisi za Uhamiaji**

**118. Mheshimiwa Spika**, Idara ya Uhamiaji inaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Jijini Dodoma. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 ujenzi ulifikia **asilimia 30** na umepangwa kukamilika mwaka 2021. Katika mwaka 2020/21 Idara itaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu na kukamilisha ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Geita, Lindi, Manyara na Mtwara. Vilevile, ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji utaanza katika Wilaya za Chato (Geita), Kyerwa (Kagera), Mlele (Katavi), Mufindi (Iringa), Simanjiro (Manyara) na Rarya (Mara).

**119. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha makazi ya watumishi, Idara ya Uhamiaji itaendelea na ukarabati wa nyumba za watumishi katika eneo la Ibinzamata Mkoani Shinyanga. Aidha, ujenzi wa nyumba ya kuishi Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Jijini Dodoma utaanza katika mwaka 2020/21.

### **Mafunzo, Ajira na Upandishwaji Vyeo kwa Watumishi wa Idara ya Uhamiaji**

**120. Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/20 jumla ya Maafisa na Askari 396 pamoja na watumishi raia 42 walipatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kiutendaji ndani na nje ya nchi. Aidha, Askari 400 walihitimu mafunzo ya awali ya kijeshi na kiuhamiaji na baadae kupangiwa kazi katika mikoa na vituo mbalimbali

vya Uhamiaji. Vilevile, Maafisa na Askari 815 pamoja na watumishi raia 176 walipandishwa vyeo katika ngazi mbalimbali.

**121. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/21 Idara ya Uhamiaji inatarajia kuajiri Askari 495 na kuwapa mafunzo ya awali. Pia, itaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa Maafisa, Askari na watumishi raia ili kuwaongezaa ujuzi wa utendaji kazi kwa ufanisi zaidi.

#### **Upatikanaji wa Vitendea Kazi katika Idara ya Uhamiaji**

**122. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20 Idara ya Uhamiaji imenunua magari matatu (3) kwa ajili ya kuhudumia watumishi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Kambarage Nyerere Terminal III. Magari hayo yamenunuliwa kuititia fedha za bajeti ya mwaka 2018/19. Katika mwaka 2020/21 magari sita (6) na pilkipiki 20 zitanunuliwa. Fedha kiasi cha Shilingi 1,176,000,000 zimetengwa kwa ajili ya upatikanaji wa vitendea kazi hivyo.

#### **VITA DHIDI YA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINADAMU**

**123. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imefanikiwa kuokoa na kuwasaidia Wahanga 196 waliokuwa wakitumikishwa katika maeneo mbalimbali nchini, kama vile kufanyishwa kazi ngumu, kutumikishwa majumbani na kutumikishwa kingono. Kati ya hao, Wahanga 180 walikuwa wakitumikishwa ndani ya nchi na 16 nje ya nchi. Waliotumikishwa nje ya nchi walirudishwa nchini kutoka Uganda mmoja (1), Thailand saba (7), Kenya watano (5), Malaysia mmoja (1) na Iraq wawili (2). Wahanga hao walipewa huduma muhimu kama vile malazi, chakula, matibabu, msaada wa kisaikolojia, elimu ya ujasiriamali, stadi za maisha, ujuzi na kuwaunganisha na familia zao.

**124. *Mheshimiwa Spika***, vilevile, watu na Kampuni zinazojihusisha na mtandao wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu zimeendelea kudhibitiwa, ambapo Wizara iliwasilisha ushauri katika mamlaka husika na Kampuni tisa (9)

zilifutiwa leseni. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na vyombo vingine vyta Ulinzi na Usalama ilifanya operesheni ya kuwasaka na kuwakamata jumla ya watu 102 wanaojihusisha na biashara hiyo na kuwfikisha kwenye Vyombo nya Sheria.

**125. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeshughulikia kesi zinazohusu usafirishaji haramu wa Binadamu kwa kushirikiana na Vyombo nya Ulinzi na Usalama pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP). Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya kesi 44 zimefunguliwa katika Mahakama mbalimbali nchini, ambapo kesi 30 zimetolewa uamuzi na kesi 14 zinaendelea. Katika kipindi hicho jumla ya wahalifu 25 waliokuwa wanajihusisha na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu walihukumiwa kutumikia adhabu ya kifungo gerezani.

**126. Mheshimiwa Spika**, Wizara pia imetoa mafunzo ya utekelezaji wa Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu kwa wadau 802 kutoka Zanzibar pamoja na Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Geita, Iringa, Kagera, Mara, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Tanga. Wadau hao walikuwa Mahakimu, Waendesha Mashtaka, Polisi, Maafisa Uhamiaji, Maafisa Ustawi wa Jamii, Viongozi wa Serikali za Mitaa na watoa huduma kutoka Mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali ambao hutoa hifadhi kwa wahanga wa biashara hii.

**127. Mheshimiwa Spika**, elimu kwa umma juu ya madhara ya biashara hii imetolewa kuitia Vyombo mbalimbali nya Habari pamoja na semina za uhamasishaji kwa Viongozi wa Dini, Viongozi wa Kisiasa, Watendaji wa Serikali za Mitaa na Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

**128. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara kuitia Sekretarieti ya Kupambana na Kudhibiti Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu itaendelea na kazi mbalimbali zikiwemo: kuandaa Mpango Mkakati wa Mapambano dhidi ya Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu; kufanya utafiti juu ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu katika Mikoa 10 ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma,

Iringa, Kigoma, Manyara, Morogoro, Mwanza, Singida na Tanga; na kuandaa na kutoa majarida ya kuelimisha wadau na wananchi dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

**129. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zitakazofanyika ni kufanya uchunguzi, operesheni na kutoa huduma muhimu kwa wahanga wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; kufanya uchunguzi na operesheni kwenye maeneo ya mipaka ya nchi na njia zinazotumiwa na wahalifu wa biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu; kushiriki katika Mikutano ya Kikanda, Kibara, Kijumuiya na Kimataifa; na kutoa mafunzo ya uwezeshaji kwa wadau juu ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa kazi hizo ni **Shilingi 120,913,000**.

#### **KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO DHIDI YA VYOMBO VYA USALAMA CHINI YA WIZARA**

**130. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya malalamiko 561 yalipokelewa na Wizara. Malalamiko hayo kutoka kwa wananchi na baadhi ya watumishi yalihusu utendaji wa Idara na Vyombo vya Usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kati ya malalamiko hayo, 452 yalihusu Jeshi la Polisi, 25 Jeshi la Magereza, matano (5) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 16 Idara ya Uhamiaji, manne (4) Idara ya Huduma kwa Wakimbizi na matano (5) Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Malalamiko 48 yalihusu Taasisi zilizopo nje ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na yaliwasilishwa katika mamlaka husika.

**131. Mheshimiwa Spika**, ufumbuzi wa malalamiko hayo unahitaji kuchukuliwa hatua mbalimbali ikiwemo kufanya uchambuzi na uchunguzi wa kina ambao wakati mwingine huhitaji kufanyika katika mikoa na wilaya mbalimbali nchini. Katika kipindi husika jumla ya malalamiko 130 yalipatiwa ufumbuzi na wahusika kupewa taarifa na mengine 431 yanaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

**132. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2020/21 Wizara itaendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi ili kuongeza imani ya wananchi kwa Vyombo vyta Usalama vilivyopo chini ya Wizara na Serikali kwa ujumla. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara itaendelea kuratibu uimarishaji wa Vitengo vyta Kushughulikia Malalamiko katika ngazi ya Makao Makuu ya Vyombo vyta Usalama na mikoa yote nchini. Aidha, Kanzidata ya ki-eletroniki itakayohifadhi na kuwezesha utoaji wa taarifa za malalamiko na jinsi yalivyoshughulikiwa itaanishwa. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa kazi hizo ni **Shilingi 146,975,000.**

### **MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

**133. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali ya Awamu ya tano imeendelea kutekeleza lengo la Ibara 145 (f) ya llani ya CCM linalohusu kuendelea kuandikisha na kutoa Vitambulisho vya Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imefanikiwa kusajili jumla ya wananchi 2,478,448.

**134. *Mheshimiwa Spika*,** idadi hiyo inafanya wananchi waliosajiliwa tangu kuanza kwa zoezi hilo kufikia 21,823,026 kati ya watu 25,237,954 waliolengwa kusajiliwa ifikapo mwezi Juni, 2020. Aidha, katika kipindi hicho, NIDA imesajili Wageni Wakaazi 26,794. Pia, Mamlaka imetoa Namba za Utambulisho wa Taifa 17,871,770 na imechapisha pamoja na kugawa kwa wananchi Vitambulisho vya Taifa 6,103,225.

**135. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, Mamlaka imesajili jumla ya Wakimbizi 207,644 katika Kambi za Mtendeli, Nduta, Nyarugusu (Kigoma) na katika Makazi ya Katumba, Mishamo (Katavi), Ulyankulu (Tabora) pamoja na Wakimbizi wenye vibali vya kuishi waliopo katika Jiji la Dar es Salaam. Pia, Mamlaka iliendesha zoezi la majoribio (*Pilot exercise*) la usajili wa wafungwa, ambapo wafungwa 380 walisajiliwa katika Magereza ya Bagamoyo (Pwani) na Isanga (Dodoma). Kutokana na zoezi hilo kufanyika kwa ufanisi usajili huo utaendelea katika magereza yote nchini.

**136. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imefanikiwa kununua mashine mbili (2) zenyewe uwezo wa kuchapisha vitambulisho 9,000 kwa saa, sawa na vitambulisho 144,000 kwa siku kwa masaa 16. Mashine hizo tayari zimefungwa na zitasaidia kufikia lengo la Serikali la kuwapatia wananchi wanaostahili Vitambulisho vya Taifa.

**137. Mheshimiwa Spika**, vilevile, kwa kutumia mfumo wa usajili na utambuzi, Kampuni za Simu nchini zimefanikiwa kusajili laini zaidi ya 37,297,930 kwa kutumia alama za vidole. Zoezi hilo limefanikisha utekelezaji wa maagizo ya Serikali ya kusajili laini za simu kwa kutumia Namba za Utambulisho wa Taifa na Vitambulisho vya Taifa. Usajili huo pia umechangia kuongezeka kwa mapato yanayokusanywa na NIDA kutoka lengo la **Shilingi 500,000,000** mwaka 2019/20 hadi kufikia makusanyo halisi ya **Shilingi 1,386,000,000** mwezi Machi, 2020 sawa na **asilimia 177**.

**138. Mheshimiwa Spika**, ninatoa Rai kwa wananchi kuendelea kujisajili na pia nawaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwashamasisha wananchi katika majimbo yao kujisajili na kutumia Namba za Utambulisho wa Taifa katika kupata huduma mbalimbali.

**139. Mheshimiwa Spika**, kupitia Bunge hili nawaomba wananchi, hususan waliopo katika mikoa ya pembezoni na mipaka ya nchi wawe na subira kutokana na kuchelewa kupata Namba za Utambulisho wa Taifa. Hali hii inatokana na kuwepo kwa utaratibu maalumu wa kufanya upukuzi wa maombi yao kwa sababu ya kuwepo kwa mwingiliano mkubwa wa watu kutoka nchi jirani. Upukuzi huo unafanyika kwa nia njema ili vitambulisho vyetu visitolewe kwa watu wasiostahili.

**140. Mheshimiwa Spika**, nawaomba wananchi washiriki ipasavyo katika kutoa taarifa endapo watabaini katika Mtaa, Kijiji, Shehia, Kata, Tarafa, Wilaya au Mkoa wanaoishi, kuna mtu ambaye siyo raia wa nchi yetu anajaribu kujianzikisha ili apate Kitambulisho cha Taifa.

**141. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia NIDA itaendelea na zoezi la usajili na utambuzi katika wilaya na mikoa yote hapa nchini, ambapo jumla ya watu 6,076,666 wanatarajiwa kusajiliwa. Lengo ni kufikia idadi ya wananchi 27,796,983 watakaofikia umri wa miaka 18 mwezi Juni, 2021 kulingana na takwimu za ongezeko la ukuaji wa watu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (*National Bureau of Statistics – NBS*). Sanjari na zoezi hilo la usajili na utambuzi, elimu kwa umma itaendelea kutolewa ili wananchi waendelee kutambua umuhimu wa Kitambulisho cha Taifa.

#### **Kuunganisha Ofisi za NIDA Katika Mkongo wa Taifa**

**142. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/20, NIDA imefanikiwa kuunganisha Wilaya 15 katika mtandao wa mawasiliano unaotumia Mkongo wa Taifa kusafirisha taarifa za usajili na utambuzi wa wananchi moja kwa moja katika kituo cha kuchakata taarifa na uzalishaji wa vitambulisho.

**143. Mheshimiwa Spika**, wilaya zilizounganishwa katika Mkongo wa Taifa ni Bariadi, Bukombe, Ilala, Karatu, Kigamboni, Kondoa, Masasi, Maswa, Mbozi, Meatu, Mkuranga, Monduli, Mvomero, Ubungo na Urambo na kufanya idadi ya wilaya zote zilizounganishwa katika mtandao wa mawasiliano kufikia 134. Katika kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi taasisi 69 za umma na binafsi zimeweza kuunganishwa na mfumo wa usajili na utambuzi wa watu.

**144. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara kupitia NIDA itaunganisha mfumo wa mawasiliano katika wilaya 16 na Makao Makuu ya Mamlaka kupitia Mkongo wa Taifa na hivyo kufikisha lengo la kuunganisha wilaya 150 nchi nzima. Wilaya zitakazounganishwa ni Gairo, Ulanga na Malinyi (Morogoro), Kaskazini A, Kaskazini B na Kusini (Unguja), Mbogwe na Nyang'wale (Geita), Mlele na Tanganyika (Katavi), Ngorongoro (Arusha), Mbulu (Manyara), Kalambo (Rukwa), Serengeti (Mara), Kyerwa (Kagera) na Micheweni (Pemba).

**145. Mheshimiwa Spika**, NIDA pia itaunganisha mfumo wa Vitambulisho vya Taifa pamoja na mifumo ya taasisi 39 za

umma na binafsi na kufikisha idadi ya taasisi 108. Utaratibu huu utaendelea kurahisisha utoaji wa huduma za utambuzi katika taasisi hizo na kutoa huduma kwa haraka na ufanisi kwa wananchi. Aidha, Mamlaka itaanza kutoza tozo kwa taasisi za umma na binafsi zinazotumia taarifa kutoka kwenye mfumo wa usajili na utambuzi kwa kuzingatia mikataba (*Data sharing Agreements*) kati ya taasisi hizo na NIDA.

### **Upatikanaji wa Vitendea Kazi vya NIDA**

**146. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuendelea kuboresha utoaji wa huduma, vitendea kazi muhimu katika zoezi la usajili na utambuzi wa watu vitanunuliwa vikiwemo *Server 20, Computer 70, Router 20* pamoja na magari manne (4). Vilevile, itatoa mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa wataalam sita (6) wa mifumo ya TEHAMA na wanne (4) katika Kitengo cha Uzalishaji wa Vitambulisho.

**147. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma na ofisi 32 za usajili za wilaya utaanza (badala ya 25 zilizokadiriwa kujengwa kabla ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu). Kati ya ofisi hizo 29 zitajengwa Tanzania Bara na tatu (3) zitajengwa Zanzibar (Wilaya ya Micheweni, Wilaya ya Mkoani na Wilaya ya Mjini). Aidha, ujenzi wa ghala la kuhifadhia nyaraka na kufanya matengenezo vifaa vya TEHAMA utaanza katika Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani.

**148. *Mheshimiwa Spika*,** kazi hizo hazikuanza kwa wakati kutokana na kuchelewa kwa majadiliano ya mkopo wa masharti nafuu kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea Kusini. Vilevile, ujenzi wa ofisi ya usajili na utambuzi wa watu katika Wilaya ya Rufiji eneo la Mradi wa Kufua Umeme wa Mwalimu Nyerere utaanza kwa kutumia fedha za ndani. Fedha zilizotengwa kwa mwaka 2020/21 kwa ajili ya kazi husika ni jumla ya **Shilingi 10,861,812,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 10,000,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 861,812,000** ni fedha za nje.

## **USAJILI NA USIMAMIZI WA JUMUIYA ZA KIJAMII NA KIDINI**

**149. Mheshimiwa Spika**, Wizara imendelea kusajili Jumuiya za Kijamii na Kidini, ambapo katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya maombi ya usajili 248 yamepokelewa. Kati ya maombi hayo 156 ni ya Taasisi za Kidini na 92 ni Jumuiya za Kijamii. Jumla ya Jumuiya 71 zimesajiliwa, maombi 174 yanaendelea kushughulikiwa na matatu (3) yamekataliwa kwa kutokutimiza vigezo husika.

**150. Mheshimiwa Spika**, zoezi la uhakiki wa Jumuiya za Kijamii na Kidini lilifanyika katika kanda tatu ambazo ni Kanda ya Kati (Dodoma, Manyara, Morogoro na Singida), Nyanda za Juu Kusini (Iringa, Mbeya, Njombe, Songwe na Rukwa) na Kanda ya Ziwa (Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Simiyu na Shinyanga). Kupitia zoezi hilo, jumla ya Jumuiya 213 zilihakikiwa ambapo 112 ni za Kidini na 101 ni za Kijamii. Zoezi husika liliifanyika ili kuhakikisha jumuiya hizo zinaendeshwa kwa kuzingatia Sheria ya Jumuiya, Sura 337. Vilevile, mfumo wa upokeaji na kushughulikia maombi ya usajili wa jumuiya hizo umeboreshwa na kuwa wa kielektroniki.

**151. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha jumuiya hizo zinaendeshwa kwa kuzingatia sheria husika, elimu kwa wananchi juu ya usajili na masharti ya usajili imeendelea kutolewa kwa wahusika pale wanapofika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya kupata huduma. Aidha, elimu hiyo imetolewa na Ofisi ya Msajili kupitia semina zilizoandalishi na jumuiya husika.

**152. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya itatekeleza kazi mbalimbali zikiwemo: kuendelea na usajili wa Jumuiya za Kijamii na Kidini; kufuatilia utendaji na uendeshaji wa jumuiya hizo; na kushiriki katika utatuzi wa migogoro ya jumuiya. Katika kutekeleza kazi hizo **Shilingi 148,048,000** zimetengwa.

## **HUDUMA KWA WAKIMBIZI**

**153. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imekuwa ikipokea na kuwahifadhi wakimbizi kutoka nchi mbalimbali. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Tanzania ilikuwa inahifadhi waomba hifadhi na wakimbizi

293,710. Kati ya hao, Warundi walikuwa 216,900, Wakongo 76,384 na 426 kutoka nchi za Comoro, Eritrea, Ethiopia, Iran, Kenya, Nigeria, Rwanda, Somalia, Sudani, Sudani Kusini, Syria, Uganda, Uturuki, Yemen na Zimbabwe.

**154. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa tatizo la ukimbizi sio la kudumu, Wizara kwa kushirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNHCR na IOM imeendelea kuwatafutia suluhisho la kudumu wakimbizi wanaohifadhiwa hapa nchini. Miongoni mwa suluhisho ni kuwarudisha katika nchi zao za asili mara baada ya usalama katika nchi hizo kuimarika au kuwahamishia katika nchi ya tatu (*Resettlement*) nafasi zinapopatikana.

**155. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya wakimbizi 9,875 kutoka nchi ya Burundi walirejeshwa nchini kwao kwa hiari yao. Idadi hiyo inafanya wakimbizi waliorejeshwa nchini kwao tangu kuanza kwa zoezi hilo mwezi Septemba, 2017 kufikia 82,299. Aidha, jumla ya wakimbizi 1,901 walihamishiwa katika nchi ya tatu ambazo ni Australia (160), Canada (44), Ireland (3), Marekani (1,689) na Uholanzi (5).

**156. Mheshimiwa Spika**, kuititia Bunge hili, **ninaomba kutumia fursa hii, kukanusha shutuma zinazotolewa na makundi mbalimbali kuwa Serikali ya Tanzania inawarejesha wakimbizi nchini kwao kwa lazima**. Aidha, ninapenda kuuhakikisha umma wa Watanzania na Jumuiya ya Kimataifa kuwa, Serikali ya Tanzania katika kutekeleza zoezi la urejeshaji wakimbizi, imekuwa ikiheshimu uhiari wa wakimbizi katika kuamua kurejea kwenye nchi zao au kuendelea kubaki Tanzania ikiwa wanaona bado hawana uhakika wa usalama nchini kwao.

**157. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyosema hapo awali, zoezi la urejeshaji wakimbizi linatekelezwa na Serikali yetu kwa kushirikiana kikamilifu na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNHCR, IOM na WFP (World Food Program) pamoja na wadau wengine wa kimataifa na ndani ya nchi. Ushiriki wa wadau hao ni ushahidi tosha kuwa zoezi linafanyika kwa

uwazi na kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya Haki za Binadamu.

**158. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Serikali itaendelea kuwashifadhi wakimbizi na kuwatafutia suluhihi la kudumu. Aidha, usalama utaendelea kuimarishwa katika maeneo yote yanayohifadhi Wakimbizi.

#### **Utunzaji wa Mazingira katika Kambi za Wakimbizi**

**159. Mheshimiwa Spika**, ujio wa kundi la wakimbizi nchini umeendelea kusababisha changamoto ya uharibifu wa mazingira ndani ya Kambi za Wakimbizi na maeneo yanayozunguka kambi hizo. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa Kimataifa na wa Ndani ya nchi imeendelea kukabiliana na changamoto hiyo kwa kufanya shughuli mbalimbali.

**160. Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa shughuli hizo ni pamoja na kutengeneza majiko banifu 7,212 na kuyagawa kwa wakimbizi kwa ajili ya kupikia, kupanda miti 784,942 na kufanya doria ndani ya kambi na vijiji jirani vinavyozunguka kambi za wakimbizi kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira. Katika mwaka 2020/21 Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika utunzaji wa mazingira kwenye maeneo ya kambi za wakimbizi na vijiji vinavyozunguka kambi hizo. Kipaumbele kikubwa kitakuwa ni katika kutafuta nishati mbadala ya kupikia badala ya kuendelea na matumizi ya kuni.

#### **SERA NA SHERIA ZINAZOHUSU WIZARA**

**161. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21 Wizara itaandaa Sera ya Taifa ya Zimamoto na Uokoaji (National Fire and Rescue Policy) na Sera ya Taifa ya Uhamiaji na Uraia (National Immigration and Citizenship Policy). Aidha, Wizara itafanya marekebisho ya Sheria ya Jumuiya, Sura ya 337, Sheria ya Zimamoto na Uokoaji, Sura ya 427, Sheria ya Uraia, Sura ya 367 Rejeo la 2002, Sheria ya Kuzuia Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu, Sura ya 433 na Sheria ya Tume ya Polisi, Uhamiaji na Magereza, Sura ya 241. Maandalizi ya Sera na

marekebisho ya Sheria husika yanalenga kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi.

### **Tahadhari Dhidi ya Ugonjwa wa COVID-19**

**162. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19 katika utekelezaji wa majukumu yake. Tahadhari zinachukuliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na wadau wengine muhimu. Miongoni mwa tahadhari zilizochukuliwa ni: kununua vifaa vyta kupima joto na kujikinga na maambukizi; kupunguza msongamano katika mahabusu za Jeshi la Polisi kwa kutoa dhamana kwa watuhumiwa wenyе makosa madogo.

**163. Mheshimiwa Spika**, tahadhari nyingine zilizochukuliwa ni: kuzuia ndugu na jamaa kuwatemebelea wafungwa na mahabusu; na kuhakikisha kuwa wageni na wananchi wanaofika katika ofisi za Wizara na Taasisi zake wanapatiwa huduma kwa kuzingatia tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo.

### **C. SHUKURANI**

**164. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Mhandisi Hamad Masauni (Mb.) kwa ushirikiano anaonipa katika kusimamia majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu Ndugu Christopher D. Kadio na Ndugu Naibu Katibu Mkuu Kailima Ramadhan kwa kusimamia vema utekelezaji wa kazi mbalimbali za Wizara.

**165. Mheshimiwa Spika**, pia, haitakuwa vema bila kuwashukuru Wakuu wa Vyombo vyta Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Inspekte Jenerali wa Jeshi la Polisi, Simon N. Sirro; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Suleiman M. Mzee; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John W. Masunga; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala; na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vyta Taifa, Dkt. Arnold M.

Kihauli. Ni dhahiri kuwa Wakuu wa Vyombo hivi wametoa mchango mkubwa katika kusimamia maeneo yao na kuhakikisha amani na utulivu unaendelea kuwepo nchini.

**166. Mheshimiwa Spika**, vilevile, nawashukuru Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi Prof. Suffian H. Bukurura, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Magereza Meja Jeneralis Mstaafu Raphael M. Muhuga, Makamishna, Makamishna Wasaidizi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Maafisa, Askari na watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutekeleza shughuli za Wizara kwa weledi na ufanisi.

**167. Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninatoa shukrani kwa wadau wa maendeleo wakiwemo Austria, Ubelijiji, China, Misri, Ethiopia, Japan, Morocco, Korea Kusini, Ujeruman, Urusi, Jumuiya ya Ulaya (EU), GGML, HAART, IOM, Nightlight International, RECSA, UNDP, UNHCR, UNICEF na UN – Women.

**168. Mheshimiwa Spika**, vilevile, navishukuru Vyombo vya Habari, Jumuiya za Kijamii na Kidini pamoja na wananchi kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli zake. Aidha, ninaishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia "Press A" kwa kuchapisha vema hotuba hii na kwa wakati.

**169. Mheshimiwa Spika**, mwisho ninaishukuru familia yangu kwani imekuwa msaada mkubwa katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kiofisi. Aidha, ninawashukuru ndugu, marafiki na wananchi wakiwemo wa Jimbo langu la Kibakwe kwa kuendeleza umoja na mshikamano katika kushiriki kwenye maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya jimbo letu.

#### D. HITIMISHO

**170. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza katika utangulizi wa hotuba hii kuwa nchi yetu imepata mafanikio mbalimbali ambayo yamechangiwa na kuwepo kwa amani na

usalama nchini. Hivyo, katika mwaka 2020/21 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itahakikisha kuwa hali hiyo inaendelea kudumishwa ili Serikali na wananchi waendelee na shughuli za kiuchumi na kijamii kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

### **Makadirio ya Ukusanyaaji Mapato kwa Mwaka 2020/21**

**171. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2020/21 Wizara inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 488,569,880,319**. Aidha, mapato yanayokusanya na NIDA kupitia ada ya utambulisho yataanza kutolewa taarifa na Msajili wa Hazina (*Treasury Registrar*) badala ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama ilivyokuwa awali.

### **Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2020/21**

**172. *Mheshimiwa Spika*,** naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Bajeti ya jumla ya **Shilingi 899,170,293,000** kwa ajili ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2020/21. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 863,734,431,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 382,229,678,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 481,504,753,000** ni Mishahara. Fedha za Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 35,435,862,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 34,540,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 895,862,000** ni fedha za nje.

**173. *Mheshimiwa Spika*,** naomba kutoa Hoja.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu. Nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba yake Mheshimiwa Cosato David Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba

Taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama ilivyowasilishwa hapo Mezani.

Awali ya yote, naomba kumpa pole Mheshimiwa Spika na Wabunge wote kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Dkt. Getrude Rwakatare. Aidha, kwa niaba ya Kamati, nampa pole Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufiwa na baba yake mzazi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa jukumu kubwa la Kamati yangu ni kuisimamia Serikali kwa niaba ya Bunge kuhusu masuala yanayohusu usalama wa raia na mali zao, naomba kuanza kwa kutoa pole kwa wananchi wote ambaو wameugua na ambaو wamepoteza ndugu zao kwa ugonjwa hatari wa homa ya mapafu unaosababishwa na virusi vya *Corona*. Aidha, naipongeza Serikali hususani Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa jitihada zao za hali na mali katika kupambana na ugonjwa huu hatari duniani. Tunaamini kuwa kwa jitihada hizo na wote kwa pamoja tukiendelea kuchukua tahadhari kama tunavyoshauriwa na wataalamu na kumuomba Mwenyezi Mungu kwa uaminifu ugonjwa huu utakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu sehemu nne zifuatazo:-

- (i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ambayo inapatikana Ukurasa wa 3 - 10 wa taarifa hii.
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Ukurasa wa 10 - 20.
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo inapatikana ukurasa wa 21-28.
- (iv) Maoni na Ushauri wa Kamati inayopatikana ukurasa 28- 39.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najielekeza katika Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo mitano iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika Mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Kaskazini Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ziara za ukaguzi, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa utekelezaji wa miradi umegawanyika katika makundi matatu yafuatayo:-

(i) Miradi ya muda mrefu ya ujenzi ambayo utekelezaji wake umesimama. Mfano wa Miradi hii ni Mradi Na.6303 wa ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Mkokotoni-Zanzibar. Maelezo yaliyotolewa na Serikali yalibainisha kuwa, katika mwaka wa fedha 2019/2020 mradi huu ilitengewa jumla ya Sh.500,000,000. Hata hivyo, hadi kufikia Machi, 2020 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa. (*Makofi*)

(ii) Miradi ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2019/2020 na imepelekewa fedha hizo ambapo

utekelezaji wake unaendelea. Mfano wa miradi hiyo ni Mradi Na.1201 kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Useremala cha Magereza, Msalato, Dodoma.

(iii) Miradi ambayo kutokana na umuhimu wake, fedha za utekelezaji zilitolewa na Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati inapongeza sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuona umuhimu wa kuwa na Jengo la Makao Makuu ya Uhamiaji na kuimarisha shughuli za Zimamoto na Uokoaji katika Jiji la Dodoma ambalo linakuwa kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, wakati wa ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati yangu ilihoji na kukagua endapo masuala ya jinsia na mazingira yamezingatiwa wakati wa kutekeleza miradi hiyo na kushauri ipasavyo. Kamati ilishauri kuwa, ujenzi wa majengo yanayojengwa yazingatieve mahitaji muhimu ya watu wenye ulemavu. Aidha, uwekwaji wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua uzingatiwe kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo utunzaji wa bustani za maua na miti katika maeneo ya majengo hayo. Matokeo na maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yanapatikana katika ukurasa wa 9 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiasi wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Wakati wa kuchambua utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati ilibaini kuwa makusanyo ya Wizara yameendelea kuongezeka kwa miaka mitatu mfululizo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 na grafu Na. 1 ya taarifa hii. Kamati inapongeza mwenendo huu mzuri wa makusanyo na inaamini kuwa hadi robo ya nne itakapokamilika, lengo la makusanyo lillilowekwa kwa Mafungu yote ya Wizara litakuwa limefikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Wizara hususani fedha za

maendeleo umendelea kuwa changamoto ya muda mrefu. Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo yaani kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019 Kamati iliendelea kuishauri Serikali kuititia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo, utengwaji wa fedha za maendeleo na mtiririko wa upatikanaji wa fedha hizo kwa Wizara hii umeendelea kuwa siyo wa kuridhisha kama inavyofafanuliwa katika ukurasa wa 15-17 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika masuala 18 yaliyotolewa ushauri, yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kuzingatiwa na mengine ambayo hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti kama inavyoonekana katika ukurasa wa 18 hadi 20 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitajielekeza katika uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Taarifa ya uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 unapatikana katika ukurasa wa 21-28 wa taarifa hii. Hata hivyo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fungu 28 -Jeshi la Polisi na Fungu 93-Idara ya Uhamiaji ndio yanayotegemewa kwa asilimia kubwa katika makusanyo ya Wizara hii na kwa miaka mitatu mfululizo mafungu hayo yamekuwa yakikusanya kwa asilimia nyingi zaidi ikillinganishwa na Mafungu mengine. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Mafungu hayo mawili ndiyo ambayo yamekuwa hayapewi kipaumbele katika kutengewa fedha za maendeleo licha ya kuwa yanakusanya zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi. Maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, katika mwaka wa fedha 2020/2021, bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwa

kwa Mafungu yote matano ni Sh.899,170,293,000. Ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa kipitia kasma, vifungu na mafungu yote ya Wizara ikilinganishwa na bajeti iliyo idhinishwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha unaoishia. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo mbalimbali ambayo yamebainishwa katika ukurasa wa 25-28 wa taarifa hii. Baadhi ya masuala hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imepungua kwa Sh.22,076,740,279 ambayo ni pungufu ya asilimia 2.39 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020. Upungufu huu upo katika matumizi ya mishahara kutokana na baadhi ya watumishi kustaafu.

(ii) Bajeti inayoombwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imeongezeka kwa asilimia 10.95 kwa bajeti ya maendeleo, mishahara imepungua kwa asilimia 7.38 na imeongezeka kwa asilimia 2.67 katika matumizi mengineyo ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020.

(iii) Fungu 93-Idara ya Uhamiaji inaombewa Sh.3,309,600,000 kwa ajili ya *package* kwa maafisa na Askari wa Idara, fedha ambayo kwa miaka yote ya nyuma ilikuwa inatolewa kwa Majeshi ya Zimamoto na Uokoaji, Polisi na Magereza. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake ambapo mara kwa imara imekuwa ikishauri kuhusu umuhimu wa kutoa *package* hii kwa Idara ya Uhamiaji ambayo mazingira yake ya kazi yanaendana na ya Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Hii inaonesha kuwa Serikali yetu ni sikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa maoni na ushauri mahsus kwa Fungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa jumla:-

(i) Kamati inashauri Serikali kuptitia Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa watumishi katika Mafungu yote ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutokana na umuhimu wake katika usalama wa raia na mali zao.

(ii) Serikali iweke mpango mkakati wa kununua magari kwa ajili ya Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Idara ya Uhamiaji ili kuwezesha Majeshi hayo na Idara hiyo kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

(iii) Upo umuhimu wa Serikali kuanza mchakato wa kuandaa Sheria ya Kusimamia Makampuni Binafsi ya Ulinzi ili pamoja na mambo mengine, kudhibiti matukio ya kihalifu yanayochangiwa na kutokuwepo kwa sheria inayosimamia makampuni binafsi ya ulinzi. Kamati yangu imekuwa ikishauri mara kwa mara kuhusu suala hilo lakini bado halijapewa uzito unaostahili.

(iv) Upo umuhimu wa Serikali kukamilisha miradi ya mwanzo badala ya kuanzisha miradi mingine mipya. Hii itawezesha uwepo wa miradi michache iliyokamilika na ambayo ina tija kwa Taifa kuliko kuwa na miradi mingi ambayo haikamiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mahsus. Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Zimamoto lilitengewa katika eneo la Mchicha, Wilayani Temeke Jijini Dar es Salaam ambalo ujenzi wake ulisimama tangu mwaka 2013. Kwa mara ya mwisho jengo hili lilitengewa Sh.2,000,000,000 katika mwaka wa fedha 2016/2017, hata hivyo, fedha hizo hazikutolewa.

Ni maoni ya Kamati kuwa upo umuhimu wa kuendeleza jengo hilo ambalo baada ya kukamilika kwake

linaweza kutumika kwa shughuli nyingine muhimu za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Jiji la kibiashara la Dar es Salaam na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua juhudzi za Serikali katika kuliwezesha kivifaa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambapo katika mwaka wa fedha 2019/2020 taratibu za kununua magari matano ya kuzima moto kutoka Shirika la Nyumbu zinaendelea. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika masuala ya maokozi pale yanapotokea majanga mbalimbali na kutokana na uhaba na uchakavu wa magari ya kuzima moto na maokozi, Kamati inashauri Serikali kuwa na mkakati madhubuti wa kuliwezesha kivifaa Jeshi hili kwani ukosefu wa vifaa hivyo utaathiri utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliwezeshe jeshi hili kupata *fire hydrants* za kutosha hususani katika maeneo ya Majiji na Miji ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati ilibaini kuwa mahitaji halisi ya *fire hydrants* ni 285,000 kwa nchi nzima, lakini Jeshi lina *fire hydrants* 2,260 tu ambapo kati ya hizo 1,003 hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 28-Jeshi la Polisi. Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Jeshi hili. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Jeshi la Polisi lilitengewa jumla ya Sh. 5,000,000,000.00 lakini hazikutolewa.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Jeshi hili lilitengewa jumla ya Sh.2,292,924,679 ambapo hadi kufikia Februari 2020 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa. Kutoikutolewa kwa fedha hizo kumeathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali zikiwemo za ujenzi wa vituo vya Polisi na nyumba za Askari na Maafisa wa Jeshi. Kamati inashauri Serikali kutoa fedha hizo hususani za kukamilisha kituo cha Polisi cha Mkokotoni ambapo Ujenzi wake umesimama tangu mwaka 2013 licha ya kuwa mradi huo umetekelizwa kwa asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudzi za Jeshi la Polisi za kutekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya vituo vya polisi na nyumba na za askari kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, bado suala la makazi kwa Askari limeendelea kuwa changamoto ambayo inatakiwa kupewa uzito wa kipekee hasa kwa kuzingatia usalama wa Askari wanapoishi uraiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka 2018/2019 Kamati ilishauri kiasi cha Shilingi 1,400,000,000/= kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari kitolewe ifikapo Juni 30, 2019. Hata hivyo, fedha hizo hazikutolewa na ziliidhinishwa tena katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na hadi kufikia Mwezi Februari, 2020 zilikuwa hazijatolewa. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Askari nchini, ili kuwapa morali ya kazi Askari wetu pamoja na kuwajengea mazingira salama ya utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu kukamilisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani tangu Mwaka 2017, pamoja na hatua nzuri iliyofikiwa katika mchakato huo, Ni rai ya Kamati kuwa mchakato huu ukamilishwe katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la msongamano wa Wafungwa katika Magereza linachangiwa na Magereza machache ya kutunza mahabusu ambao kiidadi ni wengi kuliko wafungwa, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kuwa na Mpango wa kuliwezesha Jeshi la Polisi kuwa na mahabusu zake badala ya kutumia za Jeshi la Magereza ambazo hazitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya kuwezesha mafunzo zaidi kwa Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi wa Jeshi la Polisi ili kuwawezesha kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ambayo yanachangia ongezeko la makosa ya

kimtandao, makosa yanayovuka mipaka, usafirishaji haramu wa binadamu, ugaidi na utakatishaji wa fedha. Aidha, uteuzi wa watumishi watakaoshiriki mafunzo hayo uzingatie masuala ya jinsia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa deni la Jeshi la Polisi linalondelea kukua kutokana na kutokulipwa kwa stahiki mbalimbali za Watumishi, Wastaafu na madeni ya wazabuni na watoa huduma. Hadi kufikia Mwezi Juni, 2019 Deni hilo lilikuwa shilingi 652,831,191,645. Aidha, kipaumbele cha malipo ya madeni hayo kitolewe kwa Askari na Watumishi raia ambao deni lao ni shilingi 54,579,136,558. Kwa kuwa, Ugonjwa unaosababishwa na Virusi vya *Covid -19* umeshaingia nchini, ili kudhibiti maambukizi kwa mahabusu na wafungwa, ni vema Jeshi la Polisi likadhibiti upelekwaji wa mahabusu wanaoshtakiwa kwa kesi ndogo katika Magereza.

Kamati inashauri kuwa watuhumiwa wa makosa madogo madogo wawekewe utaratibu mwingine thabiti ikiwa ni pamoja na kuripoti katika vituo vya Polisi kwa muda wanaopangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu 29 Jeshi la magereza Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwekeza katika kilimo ili liweze kujitosheleza kwa chakula. Katika Mwaka 2018/2019 na 2019/2020 zilitengwa jumla ya shilingi Bilioni tatu kwa kila Mwaka, kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu ya Umwagiliaji katika Gereza la Idete kwa Mwaka 2018/2019, na Gereza la Idete na Kitengule- Kagera kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Lakini fedha hizo hazikuwahi kutolewa, hata hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika Magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya umwagiliaji katika Magereza ili kuliwezesha Jeshi hilo kuwekeza katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali na jiko katika Gereza la Segerea. Kamati imekuwa ikisisitiza tangu Mwaka 2016 kuhusu umuhimu wa kutenga fedha hizo hasa kwa kuzingatia umuhimu wa Hospitali hiyo kwa Magereza ya Segerea. Pamoja na jitihada kubwa za Serikali katika kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza, ikiwa ni pamoja na kuendelea kujenga mabweni ya wafungwa, kutumia utaratibu wa vifungo vya nje, utaratibu wa parole na msamaha wa Rais, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa Kamati za kusukuma kesi zinakutana kwa kufuata utaratibu uliopo ili kuwezesha kesi nydingi zaidi kusikilizwa na kutolewa maamuzi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuliwezesha Jeshi la Magereza kupata magari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu. Hadi mwezi Februari, 2020 Jeshi la Magereza lilikuwa na magari 32 tu kwa ajili ya kusafirisha mahabusu katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Pwani na Dodoma na magari hayo ni mabovu na chakavu kwani yamenunuliwa tangu mwaka 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema suala hili likapewa uzito unaostahili ili kuwawezesha mahabusu kusikiliza kesi zao kwa tarehe walizopangiwa kwani kukosa kusikiliza kesi hizo ni kuwaondolea haki yao na vilevile kuendeleza msongamano katika Magereza. Serikali itoe fedha kwa ajili ya kuwezesha vikao vya Bodi ya Taifa na Bodi za Mikoa za Parole. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 zilitengwa shilingi 241,300,000 lakini hadi kufikia mwezi februari, 2020 Shilingi 44,721,400 tu sawa na asilimia 18.5 tu zilikuwa zimetolewa na kuwezesha kufanyika kwa kikao kimoja tu cha Bodi ya Taifa na Bodi ya Mikoa. Kuwezesha vikao vya Bodi hizi kutasaidia wafungwa wengi zaidi wanaostahili kupewa *parole* kupunguzwa magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, fungu 51 Wizara Serikali ione umuhimu wa kuendelea kuunganisha mifumo ya kijiditali ya

Taasisi nyingine za Serikali na ya *NIDA* ili kuwa na utendaji wenyе tija wa Taasisi zinazoshughulikia masuala yanayohusisha hadhi ya uraia wa wananchi. Aidha, vyombo muhimu vya ulinzi na usalama vishirikishwe katika kuhakikisha usalama wa kumbukumbu zinazotunzwa katika kanzi data ya *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kununua mashine mpya mbili za uchapaji zenyе uwezo wa kuzalisha vitambulisho 4500 kwa saa kwa kila mashine. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi cha shilingi 4,419,000,000 ambazo hazijatolewa kwa ajili ya kufanya usajili na utambuzi wa watu katika Mikoa yote nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali ilitenga shilingi 5,224,000,000/- hata hivyo hadi hufikia mwezi Februari 2020 ni shilingi 805,000,000 sawa na asilimia 14 tu zilitakuwa zimetolewa. Kamati ina maoni kuwa kutokatolewa kwa fedha hizo kutaathiri zoezi la usajili na utambuzi kwa ratiba ya utekelezaji iliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Upo umuhimu kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuitia *NIDA* kuweka mkakati wa kuandikisha na kuwapatia Vitambulisho watoto wenyе umri wa chini ya miaka 18 ili kurahisisha upatikanaji wa Taarifa zao hata wanapokuwa watu wazima. Utaratibu huu utaiondolea mzigo *NIDA* kwa siku za usoni pale inapotakiwa kuandikisha wananchi kwa ajili ya huduma muhimu zinazojitokeza Serikalini kama ilivyotokea kwenye usajili wa namba za simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Usajili na Ukaguzi wa Jumuiya za Kijamii na Kidini katika Mwaka 2019/2020 ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kufanyika. Hadi kufikia mwezi Februari, ni asilimia 40.82 tu ya shilingi 90,918,100 zilizokuwa zimetolewa kwa ajili ya shughuli hiyo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwa na Mkakati madhubuti wa kudhibiti na kuhakiki usajili wa Asasi za kijamii ili kupunguza changamoto ya Asasi zinazoendeshwa kwa maslahi ya mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (*UNHCR*) kuendelea kuhakiki wakimbizi waliopo nchini na kuwatafutia suluhihisho la kudumu ikiwa ni pamoja na kuwarudisha katika nchi zao kwa hiari yao. Aidha, kwa wakimbizi waliopewa uraia, Serikali iendelee kutafuta suluhihisho la kudumu ili kuhakikisha usalama katika maeneo wanayoishi na yale yanayowazunguuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, idara ya uhamiaji fungu 93 Wakati wa kujadili taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka 2017/2018 na 2018/2019 Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuhusu kutoa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Mikoa na Wilaya hususan katika Mikoa ya Lindi na Mtwara lakini fedha hizo zimekuwa hazitolewi. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali haikutenga fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa Idara ya Uhamiaji. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga na kutoa fedha za maendeleo kwa ajili ya Idara hii. Kwa Mwaka wa fedha 2020/2021, Idara hii imetengewa jumla ya shilingi 4,450,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Ni rai ya Kamati kuwa fedha hizo zitakapoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa ukamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. George Boniphace Simbachawene (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Eng. Hamad Masauni (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Christopher Kadio, Naibu Katibu Mkuu Nd. Ramadhan Kailima pamoja na Watendaji

wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI (FUNGU 14, 28, 29, 51 NA 93) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA ILIVYOWASILSHWA MEZANI**

---

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, kwa kuwa jukumu kubwa la Kamati yangu ni kuisimamia Serikali kwa niaba ya Bunge kuhusu masuala yanayohusu Usalama wa Raia na Mali zao, naomba kuanza Taarifa hii kwa kutoa pole kwa wananchi wote ambaao wameugua na ambaao wamepoteza ndugu zao kwa ugonjwa hatari wa homa ya mapafu unaosababishwa na Virusi vya COVID- 19.

Aidha, naipongeza Serikali hususan Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Kasim Majaliwa, Mb Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Ummy Mwalimu, Mb Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa jitihada zao za hali na mali katika kupambana na ugonjwa huu hatari duniani kote. Tunaamini kuwa kwa jitihada hizo, na wote kwa pamoja tukiendelea kuchukua tahadhari kama tunavyoshauri na Wataalamu na kumwomba Mwenyezi Mungi kwa uaminifu ugonjwa huu utakwisha.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya utangulizi huo, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) (c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kinatoa Mamlaka kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia.

Kufuatia majukumu hayo ya Kikanuni, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 24 na 25 Machi, 2020 ili kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, jukumu hili la uchambuzi wa Bajeti lilienda sambamba na jukumu la ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoishia kwa Mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kutokana na utekelezaji wa Jukumu hilo, naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi mitano ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inajumuisha Mafungu matano (5) ya kibajeti yafuatayo:-

- i) Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji,
- ii) Fungu 28- Jeshi la Polisi,
- iii) Fungu 29- Jeshi la Magereza,
- iv) Fungu 51- Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa-NIDA; na
- v) Fungu 93- Idara ya Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu sehemu nne (4) zifuatazo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## **2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

### **2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo mitano (5) iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Ukaguzi wa miradi hiyo ulitekelezwa kuanzia tarehe 12 hadi 18 Machi, 2020, katika Mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam na Kaskazini Unguja-Zanzibar

Miradi iliyokaguliwa ni:-

a) **Fungu 14- Jeshi la Zimamoto**

Mradi Na. 6582 wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto, Dodoma.

b) **Fungu 28- Jeshi la Polisi**

Mradi Na. 6303 kuhusu Ukarabati wa Kituo cha Polisi Mkokotoni, Kaskazini Unguja- Zanzibar.

c) **Fungu 29- Jeshi la Magereza**

Mradi Na. 1201 kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Useremala cha Magereza, Msalato, Dodoma.

d) **Fungu 51- Wizara**

Mradi Na. 6501 kuhusu Ujenzi wa Makao Makuu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

e) **Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji, Dodoma.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mhesimiwa Spika**, baada ya kueleza kuhusu Miradi ya Maendeleo na maeneo yaliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya utekelezaji wa Miradi hiyo.

**Mhesimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako kuwa, tofauti na Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambapo miradi yote iliyotembelewa haikuwa imepelekewa fedha, katika Mwaka wa fedha 2019/2020 mradi mmoja ulipelekewa fedha, miradi mitatu ilipata fedha nje ya Bajeti iliyoidhinishwa na mradi mmoja haukupelekewa fedha kabisa.

**Mhesimiwa Spika**, Mradi ulipelekewa fedha ni wa Fungu 29- Jeshi la Magereza na Mradi ambao haukupelekewa fedha ni wa Fungu 28- Jeshi la Polisi. Vilevile, naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji- Fungu 14 na Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji- Fungu 98 inatekelezwa kwa fedha zilizotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi hiyo. Kamati inampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuona umuhimu wa kutekeleza Miradi hii muhimu hasa katika Kipindi hiki ambapo Serikali imehamia Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)- Fungu 51 unatekelezwa kama sehemu ya mradi wa *The National ID system Expansion (phase II)* unaojumuisha ujenzi wa Ofisi za Usajili za Wilaya Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na uwekaji wa miundombinu wezeshi ya TEHAMA ya kufanikisha usajili na utambuzi wa watu nchini. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya Korea Kusini kupitia *Exim Bank*.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba pia nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Idara ya Uhamiaji haikutengewa fedha zozote za maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Jambo ambalo limesababisha miradi yake ya muda mrefu kuendelea kusimama hasa ile ya Ofisi za Mikoa ya Lindi na Mtwara.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya ukaguzi wa miradi iliyoorodheshwa hapo juu, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa utekelezaji wa Miradi umegawanyika katika makundi matatu kama inavyoelezewa hapa chini.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la kwanza ni Miradi ya muda mrefu ya ujenzi ambayo utekelezaji wake umesimama. Maeleo ya Serikali yalionesha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo hazijatolewa kwa muda mrefu licha ya kuwa kuna umuhimu mkubwa wa utekelezaji wake.

Mfano wa Miradi hii ni Mradi Na. 6303 wa ukarabati wa Kituo cha Polisi cha Mkokotoni- Zanzibar. Maeleo yaliyotolewa na Serikali yalibainisha kuwa katika Mwaka 2019/2020 Mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 500,000,000/=. Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2020 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihoji na kubaini kuwa Ujenzi wa Kituo hicho ulianza mwaka 2012 na kusimama Mwaka 2013 kutokana na kutokupelekewa fedha kwa miaka saba mfululizo (2013/2014-2019/2020), licha ya kuwa Kituo kilichokuwepo awali kiliungua na hivyo kusababisha askari kuendelea kutumia Ofisi zilizo chini ya kiwango.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile wakati wa ukaguzi wa mradi huu, Kamati ilibaini kuwa Mkandarasi wa Jengo hilo alishakamilisha asilimia 60 ya ujenzi na amelazimika kusitisha ujenzi kutokana na kutopewa malipo yake jambo ambalo linaathiri morali ya wakandarasi wazuri kutekeleza miradi ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la pili ni Miradi ambayo ilitengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na imepelekewa fedha hizo ambapo utekelezaji wake unaendelea. Mfano wa miradi hiyo ni Mradi Na. 1201 kuhusu ujenzi wa Kiwanda cha Useremala cha Magereza, Msalato, Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Shilingi Bilioni Mbili (2) zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Kiwanda, uingizaji wa miundombinu ya maji na umeme, na ununuzi wa mashine mbalimbali za uzalishaji. Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Juni, 2019 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia umuhimu wa Mradi huu, na maoni yaliyotolewa na Kamati hii kuhusu umuhimu wa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake, Serikali ilitenga tena Shilingi Bilioni Mbili (2) ambazo ziliidhinishwa na Bunge kwa Mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, hadi Kamati ilipofanya ziara ya ukaguzi Mwezi Machi, 2020, Mradi huu ulikuwa umepelekewa Shilingi 898,256,877.00 sawa na asilimia 45% ya fedha zilizoidhinishwa na utekelezaji wake upo katika hatua za awali ikijumuisha ujenzi wa msingi. Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Mradi huu unatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, kundi la tatu ni Miradi ambayo kutokana na umuhimu wake, fedha za utekelezaji zilitolewa na Mhe.

Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mfano wa Miradi hiyo ni Mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Idara ya Uhamiaji, Jijini Dodoma na Mradi Na. 6582 wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto, Dodoma. Kamati ilielezwa kuwa, Idara ya Uhamiaji ilipewa Shilingi 10,000,000,000.00 na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilipewa Shilingi 2,656,000,000.00

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara yalibainisha kuwa fedha hizo zimekwishatolewa na Kamati ilijiridhisha kuwa hatua za utekelezaji wa Miradi hiyo zimeshaanza ambapo Mradi wa Idara ya Uhamiaji umekamilika kwa asilimia 28 na ule wa Jeshi la Zimamoto umekamilika kwa asilimia 100.

Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuona umuhimu wa kuwa na Jengo la Makao Makuu ya Uhamiaji mapema iwezekanavyo na kuimarisha shughuli za Zimamoto na Uokoaji katika Jiji la Dodoma ambalo linakuwa kwa kasi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, wakati wa ukaguzi wa Miradi hiyo, Kamati yangu ilihoji na kukagua endapo masuala ya jinsia na mazingira yamezingatiwa wakati wa kutekeleza miradi hiyo na kushauri ipasavyo. Kamati ilihoji na kushauri kuwa, ujenzi wa majengo yanayojengwa yazingatie mahitaji muhimu ya watu wenye ulemavu. Aidha, ujenzi uzingatie uwekwaji wa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo utunzaji wa bustani za maua na miti katika maeneo ya majengo hayo.

**2.3 Maoni kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**  
**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kama ilivyobainika wakati wa ziara za ukaguzi, Kamati ina maoni yafuatayo:-

- i) Kutokutolewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati kunaathiri ratiba za utekelezaji wake;

- ii) Mwenendo mzima wa utengaji na utolewaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Mafungu ya Wizara hii, hususan Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 28- Jeshi la Polisi na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji unahitaji kuboreshwa zaidi;
- iii) Manufaa ya Miradi ya Maendeleo inayotekelzwa na Wizara hii yataonekana pale tu Serikali itakapotoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa ukamilifu ili kukamilisha Miradi iliyosimama na inayoendelea kutekelezwa.
- iv) Upo umuhimu wa kukamilisha Miradi ya Maendeleo ambayo utekelezaji wake umesimama kwa muda mrefu kabla ya kuanza kutekeleza Miradi mipya. Hii itasaidia Serikali, pamoja na mambo mengine, kuepusha ongezeko la ghamama za Miradi zitokanazo na tozo ya riba.

### **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

#### **3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipofanya uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ilizingatia makusanyo ya maduhuli ikilinganishwa na lengo lilitokusudiwa, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mafungu yote matano ya Wizara.

Vilevile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi cha kuanzia Agosti 2019 hadi Januari 2020 na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

### **3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara ikijumuisha Mafungu yake yote matano ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **471,894,244,600/=** ikilinganishwa na Shilingi **297,014,614,300/=** zilizokadirwa kukusanya katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.


Kamati ilielezwa kuwa, hadi kufikia Mwezi Februari 2020, kiasi kilichokusanya kilikuwa ni Shilingi **229,811,478,366.1** sawa na asilimia 48.7 ya Makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2019/2020. Aidha makusanyo hayo yameongezeka kwa asilimia 23.9 ikilinganishwa na makusanyo yaliyokusanya katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo yalikuwa Shilingi **185,526,900,792.62**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendelea kuongeza makusanyo yake kila mwaka kwani kwa muda wa miaka mitatu mfululizo fedha za makusanyo zimeongezeka kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 na Grafu Namba 1 hapa chini.

#### **Jedwali Na. 1: MWENENDO WA MAKUSANYO YA WIZARA**

2016/2017	2017/2018	2018/2019	2019/2020
156,543,675,737.91	160,687,217,400	185,526,900,792.62	229,811,478,366.1

**Grafu Na. 1: MWENENDO WA MAKUSANYO YA WIZARA  
2016/2017- 2019/2020**



**Chanzo: Randama za Wizara 2016/2017- 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Makusanyo hayo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 yameongezeka katika Mafungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 51-Wizara na 93- Idara ya Uhamiaji ikilinganishwa na makusanyo ya Mafungu hayo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebainisha mchanganuo wa makusanyo hadi kufikia mwezi Februari, 2020 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2 hapa chini.

### **Jedwali Na. 2: MCHANGANUO WA MAPATO**

#### **Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika mchanganuo huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

- i) Makusanyo ya Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 1.96 lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesa kuwa Fungu 14 limechangia kwa asilimia 2.3 ya kiasi kilichokusanya;
- ii) Makusanyo ya Fungu 28- Jeshi la Polisi, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 26.92 na Taarifa ya Makusanyo ilionesa kuwa Fungu 28 limeshachangia kwa asilimia 25.76 ya kiasi kilichokusanya;
- iii) Makusanyo ya Fungu 29- Jeshi la Magereza, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.4 na Fungu

hilo limechangia kwa asilimia hiyo hiyo 0.4 ya kiasi kilichokusanya;

iv) Makusanyo ya Fungu 51- Wizara, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 0.15 na Taarifa ya Makusanyo ilioneshaa Fungu hilo limechangia kwa asilimia 0.67 ya kiasi kilichokusanya;

v) Makusanyo ya Fungu 93- Jeshi la Uhamiaji, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 70.57 lakini Taarifa ya Makusanyo ilioneshaa kuwa Fungu hilo limeshachangia asilimia 70.83 ya kiasi kilichokusanya.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho huo wa makadirio ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na mapato halisi ya kila fungu, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhulli kwa Mafungu yote ya Wizara ni wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, jambo hili ni la kupongezwa kwani Kamati ilibaini kuwa Mafungu Matatu yaani Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 29- Jeshi la Magereza na Fungu 51- Wizara liliweza kukusanya zaidi ya asilimia 50 ya makadirio ya malengo yaliyowekwa hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati ilihoji sababu za Fungu 28- Jeshi la Polisi na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji kutofikia nusu ya makadirio ya makusanyo yao. Maelezo yaliyotolewa na Serikali yalibainisha yafuatayo:-

i) Kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ya Jeshi la Polisi, pamoja na sababu nyininge, kulichangiwa na kupungua kwa makosa ya usalama barabarani na kuongezeka kwa utii wa Sheria bila shuruti kwa watumiaji wa Vyombo vy'a moto. Hata hivyo, Kamati inaona suala hili ni la kupongezwa kwani ni dhahiri kuwa Jeshi la Polisi limeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utii wa sheria ya barabarani na vilevile watumiaji wa vyombo vy'a moto ambao wengi wao wameonesha kuendelea kutii sheria zilizopo.

ii) Kutofikiwa kwa lengo la makusanyo ya Idara ya Uhamiaji kumechangiwa na ufinyu wa Bajeti hivyo kusababisha operesheni maalamu ya kuwasaka wahamiaji haramu kutofanyika ipasavyo. Ni rai ya Kamati kuwa fedha kwa ajili ya misako ya wahamiaji haramu ziongezwe na kutolewa kwa ukamilifu ili kufanikisha utekelezaji wa jukumu hili muhimu la Idara ya Uhamiaji.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, Kamati inaamini kuwa hadi robo ya nne itakapokamiliika, lengo la makusanyo lilllowekwa kwa Mafungu yote ya Wizara litakuwa limefikiwa kikamiliifu.

### **3.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Wizara hususan fedha za maendeleo umendelea kuwa changamoto ya muda mrefu. Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia Mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019 Kamati iliendelea kuishauri Serikali kuititia Hazina kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Hata hivyo utengwaji wa fedha za maendeleo na mtiririko wa upatikanaji wa fedha hizo kwa Wizara hii umeendelea kuwa si wa kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia changamoto hiyo, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2020. Kupitia uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-


- i) Hadi kufikia mwezi Februari 2020, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 68.3 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara.
- ii) Kati ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari 2020, asilimia 39 ilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo na asilimia 1.48 tu ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

iii) Hadi kufikia mwezi Februari 2020, Wizara ilikuwa imepokea asilimia 55 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo na asilimia 26.4 ya bajeti ya Maendeleo ya Fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

iv) Hadi kufikia mwezi Februari 2020, Mafungu manne ya Wizara yaani Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 28- Jeshi la Polisi, Fungu 29- Jeshi la Magereza na Fungu 51- Wizara yalipokea Fedha za Maendeleo. Fungu 14 lilipokea asilimia 16, Fungu 28<sup>1</sup> lilipokea asilimia 63, Fungu 29 lilipokea asilimia 16.41, na Fungu 51 lilipokea asilimia 32.9, ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa kila Fungu husika. Fungu 93- Idara ya Uhamiaji haikutengewa fedha zozote za Maendeleo kwa Mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, ili kupata picha halisi kuhusu uwiano wa upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Mishahara, Mengineyo na Maendeleo, Kamati ililinganisha Kasma za matumizi hayo kwa Mafungu yote matano ya Wizara hii na kuwianisha kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.

#### **Chati Na. 1: UWIANO WA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020**



#### **Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020**

<sup>1</sup> Fedha zilizotolewa ni za uhamisho wa fedha (reallocation between votes) kwa ajili ya ununuzi wa helicopter za Jeshi. Kiasi cha Shilingi 2,792,924,679 kilichopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo hazikutolewa

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni wa kuridhisha. Hata hivyo, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo umeendelea kuwa si wa kuridhisha hususan kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza.

Kwa miaka mitano mfululizo, Kamati imekuwa ikishauri kuhusu Mafungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 28- Jeshi la Polisi, 29- Jeshi la Magereza na 93- Idara ya Uhamiaji, kupewa kipaumbele katika kupelekewa fedha za maendeleo, lakini ushauri huo umezingatiwa kwa Fungu 14 na 29 tu katika Mwaka huu wa Fedha 2019/2020. Hata hivyo, kiasi kilichotolewa kwa kila Fungu hakikuzidi asilimia 16.5.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha za maendeleo unaathiri Mpango na Ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mafungu hayo, ambayo baadhi yake imesimama kwa muda mrefu.

### **3.2      Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Kamati ilishauri masuala kumi na nane (18)<sup>2</sup> yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo kwa Mafungu yote matano.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika masuala yaliyotolewa ushauri, yapo ambayo yamezingatiwa kikamilifu, baadhi yanaendelea kuzingatiwa na mengine ambayo hayajazingatiwa kikamilifu kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti.

---

<sup>2</sup> Maoni yaliyotolewa yameambatishwa kama kiambatisho Na. 1

**Mheshimiwa Spika**, moja ya ushauri uliozingatiwa kikamilifu na Serikali ulihusu Serikali kuongeza ukomo wa Bajeti kwa Idara ya Uhamiaji (Fungu 93) ili kuwezesha shughuli za misako na doria, kuwezesha kuwaondoa wahamiaji haramu na kununua sare za maafisa na askari ambazo hazijanunuliwa kwa miaka mitatu sasa. Taarifa iliyotolewa na Wizara ilibainisha kuwa kwa mwaka 2020/2021, Fungu 93, imeongezewa Ukomo wa Bajeti ya matumizi mengineyo (OC) kutoka kiasi cha Shingi 14,500,692,000.00 kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 hadi kufikia Shilingi 26,520,292,000.00 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa hapo juu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia iliridhishwa na utekelezaji wa ushauri wake kuhusu Serikali kutoa fedha zilizotengwa kwa ajili ya usimamizi na utekelezaji wa adhabu mbadala kwa wafungwa kupitia Sheria ya probesheni na Huduma kwa Jamii ili kupunguza msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani. Taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati ilionesa kuwa, hadi kufikia Mwezi Juni, 2019, Wizara ilipokea Shilingi 206,269,951.33 sawa na asilimia 90.7 ya Bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizo zilifanikisha jumla ya Wafungwa 4,734 kutumikia adhabu zao chini ya Mpango wa Huduma kwa Jamii na Probesheni.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu ushauri unaoendelea kuzingatiwa, Taarifa iliyowasilishwa ilionesa kuwa Serikali imeendelea kuzingatia ushauri wa Kamati kuhusu kukamilisha mchakato wa Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 iliyorejewa Mwaka 2002.

Kamati ilielezwa kuwa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hiyo yalishawasilishwa na kujadiliwa katika ngazi ya IMTC mwezi Disemba, 2019 na tayari sehemu kubwa ya maoni na maelekezo ya kikao hicho cha IMTC yamefanyiwa kazi na Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kukamilisha baadhi ya masuala yarioshauriwa kabla ya kuwasilisha katika Baraza la Mawaziri. Ni rai ya Kamati kuwa, kutokana na umuhimu wa Sheria hii,

Serikali ichukue juhudzi za makusudi katika kuikamilisha Sheria hii ndani ya Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, ushauri mwingine uliotolewa ulihusu Serikali kutoa Shilingi **596,638,468,000/-** zilizoidhishwa chini ya fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha 2018/2019. Fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa Umma kuhusu masuala ya ukatili wa jinsia, kuanzisha elimu juu ya vitendo vya ukatili kwa kushirikisha dhana ya Polisi Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Serikali yalionesha kuwa hadi kufikia Mwezi Juni, 2019 fedha hizo hazikutolewa. Aidha, Kamati ilielezwu kuwa feha zote zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Fungu 28-Jeshi la Polisi, jumla ya shilingi 5,000,000,000.00 hazikutolewa.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

##### **4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo.

Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

- i) Kulinda usalama wa Raia na mali zao;
- ii) Kusimamia marekebisho ya tabia kwa wafungwa ndani na nje ya Mpagereza na katika maeneo ya Jamii;
- iii) Kutoa huduma za zimamoto na uokoaji;
- iv) Kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji nchini kwa Raia na wagoni; na

v) Kuimarisha na kusimamia Mfumo wa Taifa wa Utambuzi na Usajili wa Watu Nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopitia majukumu hayo kwa kulinganisha na Bajeti inayoombwua, ilibainika kuwa utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu yake utaimarishwa endapo Serikali itatenga fedha za kutosha na kutoa fedha hizo kadri ambavyo zimeidhinishwa na Bunge, kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara.

#### **4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mafungu yote matano inategemea kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi **488,569,880,319/=**. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la asilimia 3.5 ikililinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa Shilingi **471,894,244,600**. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 29 Jeshi la Magereza kwa asilimia 5.65 na Fungu 93- Idara ya Uhaniaji kwa asilimia 4.87.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi kuhusu ongezeko hilo, Kamati ilibaini kuwa mapato yatokanayo na mauzo ya mazao ya kilimo na mifugo yanatarajiwa kuwa Shilingi 1,700,000,000 sawa na asilimia 85 ya makadirio ya makusanyo ya Fungu hilo. Kwa Mwaka 2019/2020, makadirio ya mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa za kilimo yalikuwa Shilingi 1,517,000,000.

Mchanganuo wa lengo la makusanyo unaonekana katika Jedwali Na. 3 hapa chini.

### **Jedwali Na. 3: MAKADIRIO YA MAPATO**

#### **Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini yafuatayo:-

- i) Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linategemewa kukusanya asilimia 1.89 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 2, ki-uwiano ikiwa ni pungufu kwa asilimia 0.11;
- ii) Fungu 28- Jeshi la Polisi linategemewa kukusanya asilimia 26 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 26.9 kiasi ambacho ki-uwiano ni pungufu kwa asilimia 0.9;
- iii) Fungu 29- Jeshi la Magereza linategemewa kukusanya asilimia 0.4 ya makusanyo ambayo ni sawa ki-uwiano ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.4;
- iv) Fungu 51- Wizara linategemewa kukusanya asilimia 0.05 ya makadirio ya makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa

Fedha 2019/2020 ambapo lilitegemewa kukusanya asilimia 0.2; Kiasi hiki ni pungufu katika uwiano kwa asilimia 0.15;

v) Fungu 93- Idara ya Uhamiaji linategemewa kukusanya asilimia 71.65 ya makadirio ya makusanyo ikiwa ni ongezeko katika uwiano kwa asilimia 1.15 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambapo lilitegemewa kukusanya kwa asilimia 70.5.

**Mhesimiwa Spika**, kwa ufanuzi huo, ni dhahiri kuwa Fungu 28- Jeshi la Polisi na Fungu 93- Idara ya Uhamiaji, ndio yanayotegemewa katika makusanyo ya Wizara hii. Kamati imebaini kuwa kwa miaka mitatu mfululizo mafungu hayo yamekuwa yakikusanya kwa asilimia nyingi zaidi ikilinganishwa na Mafungu mengine.

Kamati inapongeza Mafungu hayo kwa kuendelea kuwa na mchango mkubwa na muhimu katika makusanyo. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizi, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Mafungu hayo mawili ndio ambayo yamekuwa hayapewi fedha za maendeleo licha ya kuwa yanakusanya zaidi.

**Mhesimiwa Spika**, ni rai ya Kamati kuwa mafungu hayo yapewe uzito unaostahili katika kutengewa na kupelekewa fedha za maendeleo ili kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za watumishi na askari, pamoja na majengo ya Ofisi na vituo vya Polisi, ambayo baadhi yake imesimama kwa muda mrefu.

#### **4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mhesimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayoombwaa kwa mafungu yote matano ni Shilingi **899,170,293,000/=**. Kati ya fedha hizo Shilingi **481,504,753,000/=** sawa na asilimia **53.5** ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi **382,229,678,000/=** sawa na asilimia **42.50** ni Matumizi Mengineyo na Shilingi **35,435,862,000/=** sawa na asilimia **4** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Aidha, Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, Shilingi **34,540,000,000/=** sawa na asilimia 97.5 ni fedha za ndani na Shilingi **895,862,000/=** sawa na asilimia 2.5 ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma, Vifungu na Mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha unaoishia. Katika uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

- i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imepungua kwa Shilingi **22,076,740,279/=** ambayo ni pungufu ya asilimia 2.39 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020. Upungufu huu upo katika Matumizi ya Mishahara kutokana na baadhi ya watumishi kustaafu.
- ii) Bajeti inayoombwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 imeongezeka kwa asilimia 10.95 kwa Bajeti ya Maendeleo, Mishahara imepungua kwa asilimia 7.38 na imeongezeka kwa asilimia 2.67 katika matumizi mengineyo ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- iii) Fungu 93- Idara ya Uhamiaji inaombewa shilingi 4,450,000,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 haikutengewa fedha zozote.
- iv) Fungu 93- Idara ya Uhamiaji inaombewa shilingi 3,309,600,000/= kwa ajili ya *package* kwa maafisa na askari wa Idara, fedha ambayo kwa miaka yote ya nyuma ilikuwa inatolewa kwa majeshi ya Zimamoto na Uokoaji, Polisi na Magereza. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake ambapo mara kwa imara imekuwa ikishaauri kuhusu umuhimu wa kutoa *package* hii kwa Idara ya Uhamiaji ambayo mazingira yake ya kazi yanaendana na ya Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Hii inaonesh kuwa Serikali yetu ni Sikivu.

- v) Fungu 93- Idara ya Uhamiaji imeongezewa ukomo wa bajeti ya matumizi mengineyo (OC) kutoka kiasi cha Shilingi 14,500,692,000.00 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kiasi cha Shilingi 26,520,292,000.00 zinazoombwa kwa mwaka 2020/2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia 82.88 ili kuwezesha, pamoja na mambo mengine, misako na doria ya kuwabaini wahamiaji haramu pamoja na kununua sare za Maafisa na Askari.
- vi) Fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Maendeleo kwa Fungu 51 upande wa NIDA zimepungua kwa Shilingi Bilioni 8,783,677,600.00 sawa na asilimia 80.86 ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 19,645,489,600 zilizotengwa kwa Mwaka 2019/2020.
- vii) Fedha za Maendeleo kwa ajili ya Fungu 29 zimeongezeka kwa asilimia 191.8 ikilinganishwa na shillingi 5,000,000,000.00 zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 zimetengwa Shilingi 14,590,000,000.00.
- viii) Ukomo wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo kwa Fungu 29 imeongezeka kwa kiasi cha Shilingi 1,895,000,000.00 na bajeti ya Maendeleo kwa kiasi cha Shilingi **9,590,000,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyoainishwa hapo juu yanatokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia na kujadili Randama za Mafungu matano ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mapema leo hii.

## **5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kudumisha usalama, amani na utulivu, Kamati inatoa maoni na ushauri mahsusini kwa kila Fungu kama ifuatavyo:-

### **5.1 Ushauri wa Jumla**

i) Kamati ilipopitia na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilibaini kuwa upungufu wa Rasilimali watu umeendelea kuwa changamoto inayohitaji kupewa umuhimu wa kipekee katika kuishughulikia. Kamati ilibaini kuwa Jeshi la Zimamoto linauhitaji wa Watumishi 4,995; Jeshi la Polisi lina uwiano duni wa askari na wananchi wanaowahudumia ambapo uwiano uliopo ni 1:1,100 badala ya ule wa Kimataifa wa 1:450; Jeshi la Magereza lina uhitaji wa watumishi 12,877; na Idara ya Uhamiaji inauhitaji wa Maafisa na askari 15,431 na watumishi wa kada za kawaida 781.

Kamati inashauri Serikali kuitia Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kulipa uzito wa kipekee suala la uhitaji wa Watumishi katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutokana na Umuhimu wake katika usalama wa Raia na Mali zao.

ii) Serikali iweke mpango mkakati wa kununua magari kwa ajili ya Majeshi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Idara ya Uhamiaji ili kuwzesha Majeshi hayo na Idara hiyo kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

iii) Upo umuhimu wa Serikali kuanza mchakato wa kuanda Sheria ya Kusimamia Makampuni binafsi ya ulinzi ili pamoja na mambo mengine, kudhibiti matukio ya kihalifu yanayochangiwa na kutokuwepo kwa Sheria inayosimamia makampuni binafsi ya ulinzi. Kamati yangu imekuwa ikishauri mara kwa mara kuhusu suala hilo lakini bado halijapewa uzito unaostahili.

iv) Upo umuhimu wa Serikali kukamilisha miradi ya mwanzo badala ya kuanzisha miradi mingine mipyä. Hii itawezesha uwepo wa miradi michache iliyokamilika na ambayo ina tija kwa Taifa kuliko kuwa na miradi mingi ambayo haikamiliki.

## **5.2 Ushauri Mahsus**

### **5.2.1 Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

i) Kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa jengo la Zimamoto lilitengewa Shilingi Bilioni Mbili (2) katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 hata hivyo fedha hizo hazikutolewa.

Ni maoni ya Kamati kuwa upo umuhimu wa kuendeleza jengo hilo ambalo baada ya kukamilika kwake linaweza kutumika kwa shughuli nyingine muhimu za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Jiji la kibiashara la Dar es Salaam na maeneo ya jirani.

ii) Kamati inatambua juhudzi za Serikali katika kuliwezesha kivifaa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambapo katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 taratibu za kununua magari matano ya kuzima moto kutoka Shirika la Nyumbu zinaendelea. Hata hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika masuala ya maokozi pale yanapotokea majanga mbalimbali, na kutokana na uhaba na uchakavu wa magari ya kuzima moto na maokozi, Kamati inashauri Serikali kuwa na Mkakati madhubuti wa kuliwezesha kivifaa Jeshi hili kwani ukosefu wa vifaa hivyo unaathiri utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

iii) Serikali iliwezeshe jeshi hili kupata '*fire hydrants*' za kutosha hususan katika maeneo ya Majiji na Miji ili kuliwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kamati ilibaini kuwa mahitaji halisi ya '*fire hydrants*' ni 285,000 kwa Nchi nzima, lakini Jeshi lina '*fire hydrants*' 2260 tu ambapo kati ya hizo, 1003 hazifanyi kazi.

### **5.2.2 Fungu 28- Jeshi la Polisi**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa Jeshi la Polisi katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa Raia na mali zao, Kamati inashauri yafuatayo:-

i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Jeshi hili. Kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Jeshi la Polisi lilitengewa Jumla ya Shilingi 5,000,000,000.00 lakini hazikutolewa. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Jeshi hili lilitengewa Jumla ya Shilingi 2,292,924,679.00 ambapo hadi kufikia Mwezi Februari 2020 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

Kutokutolewa kwa fedha hizo kumeathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali zikiwemo za ujenzi wa vituo vya Polisi na nyumba za Askari na Maafisa wa Jeshi. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizo hususan za kukamilisha kituo cha Polisi cha Mkokotoni ambapo Ujenzi wake umesimama tangu mwaka 2013 licha ya kuwa mradi huo umetekelizwa kwa asilimia 60.

ii) Pamoja na juhudzi za Jeshi la Polisi za kutekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya vituo vya Polisi na nyumba za Askari kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, bado suala la makazi kwa Askari limeendelea kuwa changamoto ambayo inatakiwa kupewa uzito wa kipekee hasa kwa kuzingatia usalama wa Askari wanapoishi uraiani.

Kwa Mwaka 2018/2019 Kamati ilishauri kiasi cha Shilingi 1,400,000,000/= kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari kitolewe ifikapo Juni 30, 2019. Hata hivyo fedha hizo hazikutolewa na ziliidhinishwa tena katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na hadi kufikia Mwezi Februari, 2020 zilikuwa hazijatolewa.

Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya Askari nchini, ili kuwapa morali ya kazi Askari wetu pamoja na kuwajengea mazingira salama ya utekelezaji wa majukumu yao.

iii) Kwa kuwa Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu kukamilisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Usalalama Barabarani tangu Mwaka 2017, pamoja na hatua nzuri iliyofikiwa katika mchakato huo, Ni rai ya Kamati kuwa mchakato huu ukamilishwe katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

- iv) Kwa kuwa suala la msongamano wa Wafungwa katika Magereza linachangiwa na Magereza machache ya kutunza mahabusu ambao kiiidadi ni wengi kuliko wafungwa, Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kuwa na Mpango wa kuliwezesha Jeshi la Polisi kuwa na mahabusu zake badala ya kutumia za Jeshi la Magereza ambazo hazitoshi.
- v) Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya kuwezesha mafunzo zaidi kwa Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi wa Jeshi la Polisi ili kuwawezesha kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ambayo yanachangia ongezeko la makosa ya kimtandao, makosa yanayovuka mipaka, usafirishaji haramu wa binadamu, ugaidi na utakatishaji wa fedha. Aidha, uteuzi wa watumishi watakaoshiriki mafunzo hayo uzingatie masuala ya jinsia.
- vi) Serikali itoe fedha kwa ajili ya kulipa deni la Jeshi la Polisi linalondelea kukua kutokana na kutokulipwa kwa stahiki mbalimbali za Watumishi, Wastaafu na madeni ya wazabuni na watoa huduma. Hadi kufikia Mwezi Juni, 2019 Deni hilo lilikuwa Shilingi 652,831,191,645.48.
- vii) Aidha, kipaumbele cha malipo ya madeni hayo kitolewe kwa Askari na Watumishi raia ambao deni lao ni shilingi 54,579,136,558.31.
- viii) Kwa kuwa ni dhahiri kuwa Ugonjwa unaosababishwa na Virusi vya COVID-19 umeshaingia nchini, ili kudhibiti maambukizi kwa mahabusu na wafungwa, ni vema Jeshi la Polisi likadhibiti upelekwaji wa mahabusu wanaoshtakiwa kwa kesi ndogo katika Magereza. Kamati inashauri kuwa watuhumiwa wa makosa madogo madogo wawekewe utaratibu mwingine thabiti ikiwa ni pamoja na kuripoti katika vituo vya Polisi kwa muda wanaopangiwa.

### **5.2.3 Fungu 29- Jeshi la Magereza**

- i) Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuliwezesha Jeshi la Magereza kuwekeza katika kilimo ili liweze kujitosheleza kwa chakula. Katika Mwaka 2018/2019 na 2019/2020 zilitengwa jumla ya Shilingi Bilioni tatu (3) kwa kila Mwaka, kwa ajili ya

ukamilishaji wa miundombinu ya Umwagiliaji katika Gereza la Idete kwa Mwaka 2018/2019, na Gereza la Idete na Kitengule- Kagera kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, lakini fedha hizo hazikuwahi kutolewa. Hata hivyo, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika Magereza yetu. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali ione umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya umwagiliaji katika Magereza ili kuliwezesha Jeshi hilo kuwekeza katika kilimo.

ii) Upo umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali na jiko katika Gereza la Segerea. Kamati imekuwa ikisisitiza tangu Mwaka 2016 kuhusu umuhimu wa kutenga fedha hizo hasa kwa kuzingatia umuhimu wa Hospitali hiyo kwa Magereza ya Segerea.

iii) Pamoja na jitihada kubwa za Serikali katika kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza, ikiwa ni pamoja na kuendelea kujenga mabweni ya wafungwa, kutumia utaratibu wa vifungo vyta nje, utaratibu wa parole na msamaha wa Rais, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa Kamati za kusukuma kesi zinakutana kwa kufuata utaratibu uliopo ili kuwezesha kesi nyingi zaidi kusikilizwa na kutolewa maamuzi kwa wakati.

iv) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuliwezesha Jeshi la Magereza kupata magari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu. Hadi mwezi Februari, 2020 Jeshi la Magereza lilikuwa na magari 32 tu kwa ajili ya kusafirisha mahabusu katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Pwani na Dodoma na magari hayo ni mabovu na chakavu kwani yamenunuliwa tangu mwaka 2008. Ni vema suala hili likapewa uzito unaostahili ili kuwawezesha mahabusu kusikiliza kesi zao kwa tarehe wanazopangiwa kwani kukosa kusikiliza kesi hizo ni kuwaondolea haki yao na vilevile kuendeleza msongamano katika Magereza.

v) Serikali itoe fedha kwa ajili ya kuwezesha vikao vyta Bodi ya Taifa na Bodi za Mikoa za Parole. Kwa mwaka wa fedha

2019/2020 zilitengwa shilingi 241,300,000 lakini hadi kufikia mwezi februari, 2020 Shilingi 44,721,400 tu sawa na asilimia 18.5 tu ziliwa zimetolewa na kuwezesha kufanyika kwa kikao kimoja tu cha Bodi ya Taifa na Bodi ya Mikoa. Kuwezesha vikao vya Bodi hizi kutasaidia wafungwa wengi zaidi wanaostahili kupewa *parole* kupunguzwa magerezani.

vi) Upo umuhimu wa Serikali kuliwezesha Jeshi la Magereza kujenga nyumba kwa ajili ya makazi ya Maafisa na Askari. Hadi mwezi Februari, jumla ya watumishi 5027 tu katika watumishi 13,258 ndio waalikuwa wanaishi Kambini hivyo kuwalazimu watumishi 8,231 kuishi nje ya kambi za magereza jambo ambalo si zuri kiusalama.

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hakuna fedha zozote zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo. Hata hivyo, kamati inalipongeza Jeshi la Magereza kwa kuendelea kutekeleza mkakati wa ufyatuaji wa matofali na kujenga nyumba kwenye vituo vyake kwa kutumia nguvu kazi ya wafungwa.

#### **5.2.4 Fungu 51- Wizara**

i) Serikali ione umuhimu wa kuendelea kuunganisha mifumo ya kijiditali ya Taasisi nyingine za Serikali na ya NIDA ili kuwa na utendaji wenye tija wa Taasisi zinazoshughulikia masuala yanayohusisha hadhi ya uraia wa wananchi. Aidha, vyombo muhimu vya ulinzi na usalama vishirikishwe katika kuhakikisha usalama wa kumbukumbu zinazotunzwa katika Kanzi data ya NIDA.

ii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kununua mashine mpya mbili za uchapaji zenyewe uwezo wa kuzalisha vitambulisho 4500 kwa saa kwa kila mashine. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi cha Shilingi 4,419,000,000 ambazo hazijatolewa kwa ajili ya kufanya usajili na utambuzi wa watu katika Mikoa yote nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali ilitenga shilingi 5,224,000,000/- hata hivyo hadi hufikia mwezi Februari 2020 ni shilingi 805,000,000 sawa na asilimia 15.4 tu ziliwa zimetolewa.

Kamati ina maoni kuwa kutokutolewa kwa fedha hizo kutaathiri zoezi la usajili na utambuzi kwa ratiba ya utekelezaji iliyowekwa.

iii) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Upo umuhimu kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuititia NIDA kuweka mkakati wa kuandikisha na kuwapatia Vitambulisho watoto wenyewe umri wa chini ya miaka 18 ili kurahisisha upatikanaji wa Taarifa zao hata wanapokuwa watu wazima. Utaratibu huu utaiondolea mzigo NIDA kwa siku za usoni pale inapotakiwa kuandikisha wananchi kwa ajili ya huduma muhimu zinazojitokeza Serikalini kama ilivyotokea kwenye usajili wa namba za simu.

iv) Serikali itoe fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Usajili na Ukagazi wa Jumuiya za Kijamii na Kidini katika Mwaka 2019/2020 ili kuwzesha utekelezaji wa shughuli zote zilizokuwa zimepangwa kufanyika. Hadi kufikia Mwezi Februari, ni asilimia 40.82 tu ya Shilingi 90,918,100 zilizokuwa zimetolewa kwa ajili ya shughuli hiyo. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuwa na Mkakati madhubuti wa kudhibiti na kuhakiki usajili wa Asasi za kijamii ili kupunguza changamoto ya Asasi zinazoendeshwa kwa maslahi ya mtu.

v) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (UNHCR) kuendelea kuhakiki wakimbizi waliopo nchini na kuwatafutia suluhisho la kudumu ikiwa ni pamoja na kuwarudisha katika nchi zao kwa hiari yao. Aidha, kwa wakimbizi waliopewa uraia, Serikali iendelee kutafuta suluhisho la kudumu ili kuhakikisha usalama katika maeneo wanayoishi na yale yanayowazunguuka.

### **5.2.5 Fungu 93- Idara ya Uhamiaji**

i) Wakati wa kujadili taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka 2017/2018 na 2018/2019 Kamati imekuwa ikishauri Serikali kuhusu kutoa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji za Mikoa na Wilaya hususan katika Mikoa ya Lindi na Mtwara

Iakini fedha hizo zimekuwa hazitolewi. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali haikutenga fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa Idara ya Uhamiaji.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga na kutoa fedha za maendeleo kwa ajili ya Idara hii. Kwa Mwaka wa fedha 2020/2021, Idara hii imetengewa jumla ya Shilingi 4,450,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Ni rai ya Kamati kuwa fedha hizo zitakapoidhinishwa na Bunge zitolewe kwa ukamilifu na kwa wakati.

ii) Pamoja na ushauri wa jumla uliotolewa kuhusu mahitaji ya vyombo vya usafiri kwa Majeshi ya Wizara hii na Idara ya Uhamiaji, kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya boti za doria ambapo kwa mazingira ya sasa Idara inauhitaji mkubwa wa boti na haina boti hizo. Hii itawezesha kuimarisha doria ya wahamiaji haramu katika maeneo ya maziwa na bahari.

## **6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard):-

1. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **M/Mwenyekiti**
2. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
4. Mhe. Prosper J. Mbeni, Mb
5. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
6. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
8. Mhe. Bonnah L. Kamoli, Mb
9. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb
10. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb

11. Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
12. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
13. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
14. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
15. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
16. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
17. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
18. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
19. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
20. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
21. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
22. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb
23. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
24. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
25. Mhe. Dkt. Charles John Tizeba, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. George Boniphace Simbachawene (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Eng. Hamad Masauni (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Christopher Kadio, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ramadhan Kailima pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Salum Mwinyi Rehani, Mb  
**MAKAMU MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO**  
**YA NJE, ULINZI NA USALAMA**  
Aprilii, 2020

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa David Cosato Chumi kwa niaba ya kamati. Waheshimiwa Wabunge ninayo maoni hapa ama hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo ya ndani ya nchi na kama ambavyo miongozo kadhaa imeshatolewa hapa na mwongozo ambao upo mpaka sasa ni kwamba hotuba hizi zitasomwa pale ambapo taarifa iliyoandikwa kwanza inahusu bajeti lakini pia haivunji kanuni zetu.

Sasa ninyi hamjapata hiyo nakala lakini niko na nakala halisi hapa aya mbalimbali ambazo ni nyingi kimsingi kama ningekuwa nazitaja naweza kuzitaja kwa mifano, lakini zina vunja Kanuni zetu za Bunge na zikiondolewa aya hizi kwasababu ziko nyingi muktadha mzima wa hotuba hii unakuwa hauna maana tena ikianzwa kusomwa halafu ikabaki kwenye Taarifa Rasmi za Bunge itaonekana killisomwa kitu ambacho hakikuwa na uhalisia. Kwa namna hiyo hotuba hii ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi haitasomwa leo hapa bungeni.

Kama Mheshimiwa Spika alivyopata kutoa fursa huko nyuma hata hapa kwa idadi ya wachangiaji nilionao, waheshimiwa wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani watapewa dakika zao kwenye uchangiaji.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja...

**NAIBU SPIKA:** Ngoja nataka kujua umesimama kwa hoja gani? Ili ndiyo njue ni kanuni ipi unataka kutumia.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Kwa sababu umesema kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Kanuni kwanza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka mwongozo, mwongozo wako kwa kanuni ya 68(7) kwasababu umeshatoa maelezo hapo sasa nilikuwa nataka utoe mwongozo kutaka kujua ni kanuni zippi ambazo tumezivunja kwenye hotuba hiyo ili Mheshimiwa Spika siku nyingine maana juzi hapa tulikuwa tumeuliza kwamba tumevunja kanuni zippi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatukupata majibu na tulikuwa tunataka tujue ni kanuni zippi ambazo zimevunjwa ili na sisi tuangalie kama kweli tunavunja kanuni basi tuweze kufanya mabadiliko. Lakini sisi tunawasilisha taarifa hii, haya ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani sasa hatuwezi tukawasilisha taarifa ambayo inafanana na taarifa ya Serikali kwa hiyo, tungeweza kujua ni kanuni zippi ambazo tumezivunja kwenye taarifa yetu hiyo ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kanuni uliyosimama nayo hiyo ya 68(7) ndiyo inayozungumzia mwongozo. Lakini, ukisimama kuhusu utaratibu lazima utaje kanuni iliyovunjwa au inayovunjwa. Sasa waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kama nilivyosema awali, maelekezo kama haya yameshatolewa mara kadhaa na mara ya mwisho yakitolewa alisimama *Chief Whip* wa upinzani Mheshimiwa Ester Bulaya, akaeleza nia ya kambi ya kwenda kuonana na Mheshimiwa Spika kuhusu mambo kama haya, ukiuliza ni kanuni gani ninayo hii taarifa hapa kwa hiyo,

naweza kukutajia lakini wewe unafahamu kanuni zile zote lazima uzitilie mkazo unapotayarisha taarifa yako.

Kwa mfano kanuni ya (64) ina mambo ambayo hayaruhusiwi bungeni yametajwa pale, sasa ukitaka niichukue hii taarifa yako nianze kukutajia ukurasa huu umevunja kanuni ya 64 sijui ngapi ngapi, ukurasa huu sijui umevunja kanuni sijui sabini na ngapi? Ukurasa huu umevunja hiyo sasa nitakuwa nasoma hiyo hotuba kimsingi. Hotuba ambayo haipaswi kwa sababu inavunja kanuni.

Kwa hiyo, ni kazi ya kambi kufanya hiyo kazi na ninyi mnao watumishi ambao wanazielewa hizi kanuni na wako ofisini kwenu kwa hiyo, naamini wanaweza kuwaeleza haya vizuri zaidi kuliko hapa nikaanza kutumia muda wa bunge kutoa ufanuzi kwenye jambo ambalo halitakiwi kuingia kwenye taarifa Rasmi za Bunge. Kwa hiyo, kwa mwongozo uliouomba ni kwamba hakuna jambo hapa ambalo haliruhusiwi liliofanyika linaruhusiwa moja.

La pili ili uweze kuomba mwongozo ukiwa unakiombea kiti mwongozo inhabidi utumie kanuni ya 5 huwezi kuomba mwongozo juu uamuzi uliotolewa na huyu aliyekaa hapa kwenye kiti. Unaomba mwongozo kwa jambo ambalo amefanya mtu mwingine ukitaka kujua mtu mwingine kwa maana ya amefanya Mbunge mwingine unataka kujua je, linaruhusiwa ama haliruhusiwi hapa Bungeni.

Lakini maamuzi yanayotolewa na Spika au maamuzi yanayotolewa na kiti huwezi kuyahoji humu ndani kanuni ya 5 inakuongoza vizuri kama hukukubaliana na maamuzi ya kiti au maamuzi ya Spika unatumia kanuni ya 5 kupeleka malalamiko yako kwa Katibu wa Bunge *then* kamati itaitwa kwa ajili ya kuangalia uamuzi uliotolewa na kiti, uwezi kuhoji uwamuzi uliotolewa na mtu aliyekaa hapa mbele.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge ninayo majina hapa ya wachangiaji na tutaanza kwa utaratibu huu na tutaanza na Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, atafuatiwa na Mheshimiwa Salum Mwinyi

Rehani, Mheshimiwa Almas Athuman Maige ajiandae, halafu wale wahudumu wetu wanitazamie nje kama mvua bado ipo ama vipi? Ili nisije nikatuma mtu aelekee Msekwa kwamba atachangia kule lakini kulikuwa na changamoto ya mvua.

Kwa hiyo, nijulishwe hilo ili niweze kuwaelekeza walioko huku wakae na walioko Msekwa pia nilitewe taarifa ili wachangie wakiwa kule kule badala ya watu kutoka hapa mvua ikiwa inanyesha, Mheshimiwa Oliver Semuguruka.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kutoa mchango wangu katika wizara hii, na pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge lako tukufu na ikiwa ni Bunge la mwisho, bajeti ya mwisho la bunge letu na pia nikiwa mchangiaji wa kwanza ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa wetu Rais wetu kipenzi kwa kazi kubwa anazozifanya za kujenga nchi yetu. Na pia nipende kusema katika ugonjwa huu corona viongozi wengi wameshaongea akiwepo mpendwa wetu Rais kikubwa watu wasiendelee kuwa na hofu na pia tukumbuke kumuomba Mungu ili aendelee kutuepusha na ili gonjwa ambalo na imani Mungu atatuepusha nalo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja naombaa njielekeze katika mchango wangu. Kwanza kabisa nianze na changamoto kubwa iliyopo wilaya za mipakani hasa kuhusu upande wa *NIDA* na *passport* za kusafiri. Ninaongea kwa masikitiko makubwa sana katika Wilaya ambazo ziko mpakani kwa mfano kama Kagera Wilaya ya Ngara, Misenyi, Kerwa, Karagwe tunapata changamoto kubwa sana katika vitambulisho hivi vya *NIDA*, mtu anaenda pale akifika pale anaanza kutiliwa mashaka kwamba siyo raia, ningependa kuuliza waziri akija kunijibu aniambie ardhi ya Kagera haiko Tanzania kwa sababu tunapata shida sana katika mambo ya vitambulisho. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kingine nikiangalia upande mwagine ukweli kabisa kuna mwingiliano mkubwa kwenye wilaya za mipakani wa wageni wanaoingia kutoka nchi jirani kwasababu kama Ngara tumepakana na Rwanda, tumepakana na Burundi, Kerwa hivyo hivyo tumepakana na Rwanda, Uganda, tumepakana na Misenyi. Lakini ninachojaribu kujiuliza Serikali ya kijiji wanafanya kazi gani? Kwa nini wasitambue raia wao kuliko raia wanapata shida kwasababu mtu akiingia pale kama siyo raia Serikali ya kijiji inatambua kwamba huyu siyo raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mabalozi kwa nini raia wa upande wa Kagera tunaendelea kupata shida na kibaya zaidi hata watu wa uhamiaji wanatusumbua sana unaenda pale wanaangalia *appearance* yako mfano kama mimi nikienda pale anaangalia nimepanda juu mashalah wanaanza kuleta shida kwa nini watupatie shida hiyo mimi sijajumba kwa kweli naomba waziri akija anipe majibu ya kuridhisha kwasababu hakuna mtu anayependa anayesema naomba nizaliwe sehemu fulani inatokea unazaliwa sehemu fulani na pia ningependa niulize hivi mtu unatembea hivi mtu anasema wewe siyo mtanzania wewe siyo raia, hivi Mtanzania ana rangi gani? Ana sura gani yaani ni mtu wa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tukianza kuangalia kwa maumbo, kuna mipaka mingi ambayo iko Tanzania. Kuna Mara, Arusha, Mbeya kule, Mtwara, Ruvuma na kote ni mipakani. Kwa nini Kagera tuwe katika mashaka kwamba sisi sio raia? Mtu ukitembea, unaambiwa wewe ni Mnyarwanda; wewe ni Mrundi; *why?* Ina maana Serikali haiwezi kufuatilia ikajua huyu sio raia na huyu ni raia!

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie sana sana kwa jicho la huruma...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Semuguruka kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda tu nimpe taarifa kwamba usumbufu anaoupata Kagera, siyo Kagera tu, hata kule kwetu Tarime wengi tunadaiwa kuwa ni watu wa Kenya. Kwa hiyo, labda Serikali iangalie hili kwa umakini zaidi na iweze kutoa vitambulisho ili raia wasisumbuke sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kabisa kwa sababu naye anayeongea yuko mipakani vilevile. Ina maana ni changamoto ambayo ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kule Ng'ara Mnyarwanda akiongea nitamsikia, Muha akiongea nitamsikia, Mrundi akiongea nitamsikia. Sasa, hapo ndipo kwenye changamoto. Kwa hiyo, tusiwe *judged* kwa kuangalia *appearance* ya mtu kwamba huyu ni mkimbizi. Nini maana ya kuwa na Serikali za Kijiji? Nini maana ya kuwa na Balozi? Kwa kweli naomba Serikali iliangalie kwa jicho la huruma. Tunahangaika sana, tunateseka sana wananchi ambaao tuko mipakani. Pia napenda...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, kuna taarifa nydingine.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba *immigration* kuwahoji raia ni takwa la kisheria ambayo sisi Wabunge tumelipitisha. Sasa kuendelea kushambulia taasisi hizi ni kuwaonea. Angekuwa na wazo zuri kama angeleta hoja hapa tukabadilisha, wao wakatoa tu *passport* bila kuhoji mtu yejote. Ni hilo tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, hiyo ninamlinda Mheshimiwa Oliver Semuguruka, hiyo siyo taarifa. Mheshimiwa Oliver Semuguruka, malizia mchango wako. (*Makofii*)

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba niendelee na mchango wangu. Nilikuwa napenda pia kuongelea shida iliyopo katika Mkoa wetu wa Kagera, pia hiyo shida ipo Mkoa wa Kigoma na shida hiyo vile vile inapatikana sana mipakani ambako tulipokea wakimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafanya kazi *UN*, ninajua nini maana ya wakimbizi. Tulipokea wakimbizi wa *genocide* mwaka 1994; waliingia Ng'ara na Kigoma na mpaka leo wakimbizi bado wapo.

Kwa hiyo, hoja yangu ni kuwaambia watu wa Uhamiaji, kabla ya kum-judge mtu amhoji. Sikatai kwamba asihojiwe, ahojiwe, ijulikane anatoka wapi; lakini siyo mtu anaenda pale anaambiwa leta cheti cha kuzaliwa cha babu yako na babu yako. Hicho cheti nakitoa wapi? Kwa kweli inakuwa ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *issue* ya kwamba sisi tulipokea wakimbizi, labda naweza nikasema ndiyo hiyo wanaangalia, labda huku ni mwingiliano wa wakimbizi na nini; lakini Mtwara na Ruvuma walipokea wakimbizi kutoka Msumbiji na Malawi, ina maana wenyewe hawasumbuliwi huko kama tatizo ni kwamba sisi tulipokea wakimbizi wa *genocide* wa Rwanda na Burundi? Kwa hiyo, naomba sana waliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Tanga nao walipokea wakimbizi kutoka Somalia na nafikiri mpaka leo bado wakimbizi wapo Tanga, mbona wenyewe hawatiliwi mashaka? Arusha kuna watu wanafanana zaidi na wale wanaoita ni wakimbizi wa Rwanda au Burundi, lakini hawa watu hawasumbuliwi. Kuna Wamasai wa Kenya kuna Wamasai wa Tanzania; mtu akiwa pale Tarime kwa mfano anaitwa ni mkimbizi, yaani sio Mtanzania. Kwa hiyo, naomba sana Idara ya Uhamiaji ijiridhishe wakati inaangalia huyu ni raia au huyu siyo raia? Naomba sana Serikali yetu iweze kuangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mipaka ya Mbeya, Arusha, Mara kote huko ni mwingiliano kwa watu ambaao wanaweza kuwachukulia kwamba sio raia. Kwa hiyo, naomba sana tusiwe *judged* kwa kuangaliwa wewe ni mrefu, wewe ni mfupi, wewe ni mnene au ni wa namna gani. Kikubwa tuangalie uraia wako ukoje na kama unatia mashaka, Serikali inajua; lakini siyo kusumbua raia, kila anapoenda kwenye kitambulisho cha *NIDA*, hamna kitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *passport* hizi za kusafiria, kuna ndugu yangu mmoja alikuwa anatakiwa kwenda kusoma nje; kwenda kufuatilia *passport*, akakosa kwa sababu ni mrefu, ni maashalah, eti sio Mtanzania. Nikauliza kwa nini usiende kuulizia huko ni kitu gani? Wewe ni Mtanzania au siyo Mtanzania?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa changamoto ambayo...

**SPIKA:** Muda umeisha Mheshimiwa, kengele mbili zimeshagonga.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani. Waheshimiwa Wabunge, nikiita kama mtu yuko Msekwa atanishtua kwa sababu ninaambiwa mvua bado inanyesha nje. Kwa hiyo, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud halafu tutaendelea.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kupata fursa hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kwa dhati kabisa kukushukuru wewe Naibu Spika na Spika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wa karibu kabisa mnaonipa miongozo na maelekezo kuweza kuismamia Wizara hii nyeti ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Ulinzi na Usalama na kuweza kumudu kuwaongoza Wajumbe mbalimbali wa Kamati hii bila kujali vyama vyao na tuseme wazi kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nashukuru viongozi wa Wizara hii; Waziri na Naibu wake pamoja na Makatibu Wakuu, pamoja na Watendaji wote wa vyombo vya Wizara hii ya Mambo ya Ndani kwa ushirikiano ambao tunaweza kupeana maelekezo na miongozo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba mambo ya ulinzi yanakwenda kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia na kutoa ushauri katika maeneo makuu mawili; Moja ni suala zima la *Corona*. Wizara ya Mambo ya Ndani kwa mujibu wa shughuli na kazi inazozifanya, bado nasi tunahusika kuweza kuona kwamba tunashiriki katika kuhakikisha kwamba baadhi ya maeneo yetu tunadhibiti ugonjwa huu wa *Corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali siyo nzuri na kuna maeneo yanaonyesha kwamba ni hatarishi zaidi. Wengi walikuwa wameangalia mahabusu na wafungwa waliyoko

magerezani kwamba ni tishio; kweli ni tishio na wanaweza kupata athari kubwa. *Risk* kubwa iko kwa wale ambao wanakwenda kufuatilia kesi zao Mahakamani; kwenda na kurudi Magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunatakiwa tuwe na uangalifu mkubwa na udhibiti. Hizi *sanitizer* ziwe ni sehemu ya kipaumbele kwa hawa washitakiwa wanaokwenda Mahakamani na kurudi. Sio hao tu, askari wanaosimamia wafungwa na washitakiwa wanaokwenda na kurudi Mahakamani, kuweko na vitendea kazi au mavazi maalum ambayo yataweza kuwalinda wakati wanapokuwa katika maeneo ya kuhudumia wale wafungwa. Vinginevyo, hapa tuna tishio kubwa la kuweza kuambukiza maradhi haya katika Magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia vilevile Magereza hawa wanakabiliwa na tatizo kubwa la magari; na wakati wafungwa au washitakiwa wanapelekwa Magerezani kwa kutumia magari binafsi, lakini magari ya abiria tunawaona, kitu ambacho kwa kweli siyo salama zaidi na inatishia uwezekano wa kuweza kupeleka maradhi haya katika Magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali sasa hivi iwe na mpango mbadala maalum wa kuhakikisha kwamba kunakuwa na vitendea kazi vya kuweza kuwalinda hawa maabusu na washitakiwa ambao wapo katika maeneo yetu mbalimbali hatarishi ili ugonjwa huu usije ukaingia katika Magereza yetu. Ni kitu ambacho kwa kweli kama hatukuchukua tahadhari kubwa kinawezekana kikaingia *time* yoyote na ongezeko la uambukizaji utakuwa ni mkubwa sana na udhibiti utatupa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kulizungumza ni suala zima la vyombo vyetu vya ulinzi hasa vinavyohudumia watu mbalimbali katika mipaka yetu na maeneo mbalimbali tuliyonayo. Wanatakiwa wawe na weledi sasa wa kuelewa na kutambua vitu mbalimbali hasa

hizi *biological weapons* ambazo tunaona ndiyo tishio kubwa sasa hivi duniani kuliko hata vita vya mzinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa ni kuwa na vijana ambao wana weledi, taaluma za kutambua kemikali na *biological* mbalimbali ambazo zinakuwepo katika maeneo yetu kuliko kuwa tu na Askari ambao kazi yao kubwa ni kukaza mguu na kupiga buti, pengine na kupeleka wafungwa na kurudisha. Sasa tuwe na vijana ambao watakuwa na weledi mzuri wa kutambua vitu hivi ambavyo ni hatarishi kwa maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii katika maeneo mbalimbali tukiangalia nchi za wenzetu; Marekani, China na hata Nigeria na Ghana, wanatumia vijana ambao wanatumia *electronic equipments* ambazo zinasaidia sasa utambuzi wa vitu mbalimbali au maradhi mbalimbali katika maeneo yetu ya mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunashuhudia bidhaa mbalimbali zinaingizwa *airport* na katika mipaka yetu mbalimbali. Sasa watu hawa wanakuwa na weledi mdogo, hivyo vitu vile vinaruhusiwa kuingia ndani kwa kukosa tu weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuishauri Serikali kwanza iweke vifaa maalum vya utambuzi katika mipaka yetu yote. Kwa sababu tunavyozungumza, *one stop border* maana yake tunakuwa na *full kits* za kila kitu ambacho kinahitajika kutambulika pale kiweze kutambua kwa uhakika zaidi, kuliko vingine kuchukua labda mpaka *sample*, upeleke kwa mkemia, upeleke huku, kitu ambacho kwa kweli kinapoteza muda na havionyeshi weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba majeshi haya, wale vijana wenye taaluma, tupeleke katika maeneo yetu ya mipakani hasa kwa wakati huu na kuhakikisha kwamba tunadhibiti maambukizi na vitu hatarishi ambavyo vitaingia katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, hata vile vitengo vyetu vya Polisi Marine na wengineo waweze kudhibiti hivyo vitu. Kwa upande wa Jeshi la Uhamiaji, wao wana tatizo la vitendea kazi. Ni sehemu moja ambayo ni muhimu na kunatakiwa kuwepo vijana wenye weledi hasa wanapohudumia maeneo yetu ya mipakani. Hawana magari ya kutosha lakini wengine hawana ofisi za kutosha ambazo zinawawezesha kufanya kazi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona majeshi ya wenzetu, Uhamiaji wanakuwa na *marine boat* ambazo zinawasaidia kutambua watu mbalimbali wanaofanya biashara za haramu lakini kutambua watu mbalimbali ambao wanajiingiza katika misingi ya kupenya kwenye *panya road* za baharini au kwenye maziwa yetu bila kutambulika. Kwa hiyo, nalomba Serikali, pamoja na bajeti iliyonayo lakini tuangalie yale muhimu ambayo yataweza kuleta ufanisi wa utendaji kazi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine naiomba Serikali kwamba bajeti na yale mapendekezo ambayo yaliyotolewa na Kamati yangu tuweze kuyazingatia na kuyatekeleza. Tusipoipa fedha Wizara hii, tusegemee ufanisi jamani. Hawa watu hawawezi kwenda kwa kutumia nguvu tu, wanahitaji fedha wapate vitendea kazi ili waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mwenzangu pale amesoma mapendekezo yale zaidi ya 11 na yote ukiangalia uwezo wake au fedha zilizotolewa ziko chini ya asilimia 25. Kwa hiyo, tuiombe Serikali kwa dhati kabisa iongeze *percent* ya utoaji wa fedha ili kuonyesha na hii Wizara ina ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao. Vinginevyo, wakati mwengine tutakuwa tunaleta lawama ambazo hazistahiki.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tumekuwa tukisema sana hapa *NIDA* kwamba ina *low performance* kutokana na utendaji wake wa kazi, lakini *NIDA* vilevile ukiangalia fedha zilizokwenda hazilingani na utendaji wa kazi walizofanya. Fedha ni kidogo. Sisi ndio tuliojua hali halisi iliyokuwepo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na fedha zile zilizotolewa, hawamudu kuweza kutoa vitambulisho kwa mujibu wa hali halisi ilivyo. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali itoe fedha za kutosha tuhakikishe *NIDA* inaleta mapinduzi, ilete vitambulisho ambavyo ndiyo nguzo na mwelekeo wa Watanzania na ndiyo kitu wanachokihitaji Watanzania na siyo kupata namba tu peke yake.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. SALUM M. REHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicolas Matiko na Mheshimiwa Mwita Getere ajiandae.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, hujaniruka kweli na Almas Maige.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi ya kusimama mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa ya amani na inayoleta maendeleo ya hali ya juu.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar, Makamu wa Pili, Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa

wanayoifanya katika Taifa letu. Nachukua nafasi hii pia kumshukuru /GP na Makamishna wote kwa kazi kubwa wanayoifanya na tumeona mambo mbalimbali yamepata mabadiliko makubwa. Moja, ni madawa ya kulevyia. Hali ya madawa ya kulevyia imepungua sana na hii kwa kweli inabidi tuwapongeze kwa hali ya juu sana. Naomba /GP uendelee kufanya kazi ili kulisaidia Taifa lako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nizungumze suala moja ambalo tumekuwa tukilizungumza ndani ya Bunge kwa karibia miaka minne yote tuliyokaa hapa; suala la upungufu wa magari katika vituo vyetu vya Polisi. Nami nilishawahi kusimama hapa nikasema, basi tufanyiwe *favour* angalau baadhi ya vituo tupatiwe magari kwa ajili ya kutendea kazi. Wenzetu katika Vituo vya Polisi hasa Kituo cha Afya Mfenesini kule Zanzibar kwa karibu miaka minne hakijawahi kupewa gari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukitumia wakati mwingine magari binafsi, haipendezi. Wakati mwingine magari ya Askari wenyewe yanatumika, haipendezi. Naomba sana Serikali itilie mkazo mkubwa katika jambo hili ili wenzetu hawa wapatitive magari kwa ajili ya kufanya kazi zao ili sasa lawama wanazopewa na wananchi ziendelee kupungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwapongeza sana Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya kujenga nyumba za Askari Polisi, lakini bado suala la ukarabati wa Vituo vya Polisi hasa vile vya zamani bado halijapewa uzito wa kutosha. Naomba sana Wizara hii iangalie Vituo vyetu vya Polisi ambavyo kwa kweli hasa kwangu upande wa Kaskazini Unguja karibu yote, ndiyo sehemu kubwa ambayo watalii wetu asilimia 80 wanapita maeneo yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo vizuri vituo vikawa katika hali mbaya. Wakati mwingine vinatuletea sura mbaya na kwa kweli haipendezi. Naomba sana hili Serikali ijithahidi sana kuhakikisha wanawapa fedha Wizara ili waweze kufanya kazi ya ukarabati wa Vituo vya Polisi, lakini pia kuviwekea uzio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Polisi vingi hasa kule kwetu havina uzio jambo ambalo ni hatari sana kwa usalama wa vituo vyetu. Vituo kama hivyo wakati mwingine anaweza akaingia mtu kutoka upande wowote ule na asijulikane akaenda kufanya jambo baya katika kituo. Siyo jambo linalopendeza. Naomba sana Wizara iangalie vizuri haya, lakini baadaye wachukulie hatua kuhakikisha kwamba wanawaweka wenzetu katika hali nzuri ya usalama hasa wa kwao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza sana suala la *Corona* sana tu ndani ya Bunge hata mitaani na viongozi wetu wakuu wamezungumza, lakini naendelea kuwaambia wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani wachukue tahadhari kubwa zaidi. Tunajua mifumo ya kijeshi inavyoendeshwa ndani ya makambi na sehemu nyingine, mikusanyiko foleni zile za ukaguzi na mambo mengine yanaweza yakachangia pia kuleta ugonjwa humo ndani ya makambi. Ni vizuri wabadirilishe mfumo, watafute mfumo ambaeo utakuwa salama zaidi wapiganaji wetu wasije wakapata madhara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna siku nilipata nafasi ya kuhudhuria semina Dar es Salaam ya Usalama Barabarani kuna watu walitoa mada na watu wakachangia sana wakaeleza madhara yanayosababisha ajali nyingi barabarani; wakasema ajali nyingi wakasema ni sababu ya ulevi, wengine mwendokasi, lakini mimi nikawaambia kuna moja halikutajwa na hili ndilo baya zaidi ambalo linaweza likatuathiri hata katika ugonjwa wetu huu wa *Corona*. Dharau kwa baadhi yetu wengi Watanzania madereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sasa hivi tukilipima kwenye *Corona*, watu wakifanya dharau kwa jambo hili, tunaweza tukateketea halafu tukashangaa wenyewe. Naomba sana wananchi wote Watanzania kwa umoja wetu kwa jambo hili tuondoe dharau, tuondoe ubishi, tuwe kitu kimoja kuhakikisha kwamba janga hili tunaliondoa tena kwa kasi kubwa. Bila hivyo hali kwa kweli inaweza ikawa mbaya sana sana. Tubadililike sana. Wapo Watanzania wanasema

bado tuko na ubishi na dharau tunayo. Kwa hiyo, tubadilike Watanzania katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naiomba sana Serikali kuwapatia fedha za kutosha wenzetu wa Mambo ya Ndani katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Bila fedha hawa watu hawawezi wakaenda. Fedha maana yake ni nyenzo. Wakiapata fedha watapata nyenzo za kufanya kazi, lakini vituo vitakuwa bora na mambo mengine yote yataboreshwa. Ni vyema tukaliangalia kwa undani kabisa jambo hili na kuweza kuwasaidia. Wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu, nami nawapongeza sana. Yako mambo tunayoyafahamu, tunayajua kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini pia wanafanya kwa uzalendo. Naomba sana Serikali iendelee kuangalia Wizara hii na kuisaidia kwa hali na mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Esther Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Getere na Mheshimiwa Almas Athumanji Maige, ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye Wizara hii muhimu ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru Watanzania kwa kutulipia faini tukatoka gerezani na sasa niko hapa kuwasemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni Wizara moja nyeti na ambayo inahitaji pia iweze kupata fedha za maendeleo kama ambavyo tunaidhinisha hapa Bungeni. Ametoka kusema Waziri hapa kwamba tuliidhinisha bilioni 31.9, lakini mpaka Machi, mwaka huu wamepata bilioni 7.9 tu za maendeleo. Katika hizo kwa Jeshi

la Polisi tuliidhinisha takribani bilioni 2.79 kwa ajili ya maendeleo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, *lakini zikachukuliwa sijui zingine zilitoka wapi, bilioni 3.5 wakanunua helikopta nje hata ya yale ambayo tulikuwa tumeidhinisha hapa Bungeni*. Kwa hiyo inabidi tunapokuwa tunakaa hapa tunaongelea haya mambo lazima yatekelezwe kama vile ambavyo tunapitisha, sio tunakaa tunapoteza muda na fedha za walipakodi wa Tanzania halafu baadaye watu watatu wanakwenda wanakaa huko nje wanapitisha fedha kinyume na kile ambacho Bunge limepitisha. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea kuchangia mchango wenyewe, nipende tu kuomba...

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimelisikiliza hili jambo kwa muda na ningependa tujielekeze kama Bunge kwamba wanakwenda kukaa watu wachache au zinatolewa pesa mahali pengine nje na zilizopitishwa na Bunge. Naomba kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kupitia Sheria ya Bajeti amepewa mamlaka ya kufanya *reallocation* na pesa yote inayotolewa na Mheshimiwa Rais amabaye anakwenda anaahidi inatolewa, zote hizo zinatoka kwenye bajeti iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu. Kwa hiyo naomba sana Waheshimiwa Wabunge tunapochangia tusije tukawapotosha Watanzania kwamba kuna fedha zinatolewa kutoka kwenye mifuko ambayo haijulikani, hapana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe tunatunza na muda. Wote tunajua hiyo sheria. *Nimezungumza hapa 2.79 hatukutenga hapa kwa ajili ya kununua helikopta lakini yet 3.5, yaani on top of zile 2.79 ambayo ilikuwa imetengwa kwenda kwenye maendeleo mbalimbali ndani ya Jeshi la Polisi imeongezeka on top of that 0.7 billion zikawa 3.5 kwenda kununua helikopta ambayo hatujaidhinisha hapa Bungeni.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, *it has to be 15%,* nisipoteze muda, nina dakika kumi tu...

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Esther Matiko tusaidie illi uliweke vizuri kwa sababu Sheria ya Bajeti ilipompa Waziri yale mamlaka ina mahali pale imemalizia labda, kwa sababu kwenye sheria huwa kuna kitu kinaitwa *proviso*, labda kuna masharti aliyowekewa pale, yaani wewe tueleze tu vizuri ili ikae vizuri kwenye kumbukumbu zetu; tulipompa hayo mamlaka Waziri tulimwekea mipaka kwamba inabidi arudi hapa ndiyo tuidhinishe, ndiyo aweze kufanya hiyo *reallocation* au hapana?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *in a nutshell, we did not budget to buy helicopter here,* naomba nieleweke...

**NAIBU SPIKA:** Ngoja, ngoja...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** ...anafanya *reallocation for the budget...*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, tuelewane vizuri; kama Bunge limepitisha sheria ya kumruhusu Waziri kufanya *reallocation*, kama Bunge limepitisha hiyo sheria ukisisitiza kwamba hatujapitisha hapa na yeye amefanya *reallocation* ni kinyume au ni sawasawa na hiyo sheria ama haruhusiwi kufanya hivyo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kinyume kwa sababu sheria inamwambia afanye *reallocation* kwenye kile kitu ambacho ni *budgeted for*. Amefanya *reallocation* kwenda kwenye kitu ambacho ni *unbudgeted*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni mwanasheria, naomba kuendelea.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango amesimama tena.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Bajeti inaeleza wazi kabisa, tunachotakiwa kufanya Wizara ya Fedha ni *action plan* inayotoka kwenye Wizara husika inaletwa zinazotekelezwa na zinakuwa ni ndani ya Mafungu ya Wizara husika, *activities* zilizopangwa, ndicho kinachofanyika. Kwa hiyo tusitafute maneno mengine ya kuwaaminisha Watanzania. Pesa zote zinazotolewa zinatolewa zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu lakini kwa *activities* ambazo Wizara husika imeweka *prioritization* yake kwamba katika *scale of preference* kwa mwaka huu Jeshi la Polisi linahitaji helikopta, kwa hiyo hizo ziko ndani ya Mafungu husika ya Wizara, hakuna kitu kingine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, nadhani umesikia, tusiendeleze ubishi kwenye hilo tafadhali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijakubali na siwezi kuchukua alichokisema; unapanga mpango halafu unakuja...

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuendelee kama ulivyonipa *guideline* lakini / have not taken whatever she has said.

**NAIBU SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Esther Matiko kwa sababu hizi ni Taarifa Rasmi za Bunge, kwa sababu hiyo, hilo

eneo la kuzungumzia wewe unasema Mheshimiwa amekueleza sheria inachosema na kilichotokea, wewe unasema hukubali, sasa kati yenu hapa kwa sababu mimi sina uwezo sasa hapa nilipo Mezani wa kuipata hiyo ambayo ilitokea na hiki kinachoendelea sasa, sitaki hizo taarifa ambazo mimi nimesimamia kikao zionekane kwamba tunavunja sheria ambayo ni ya kwetu sisi wenyewe tuliyotunga humu ndani.

Kwa namna hiyo Mheshimiwa Esther Matiko, kwenye hilo eneo mimi kama nilivyota maelekezo, hatuendelezi huo ubishi na maelezo yanabaki kama hivyo yalivyo elekezwu, endelea kwenye eneo lingine. Kwa sababu la sivo maana yake tusimamishe niitishe mimi hiyo sheria tuanze hapa kubishana, jambo ambalo sitaki kupoteza muda wa Bunge.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, *I hope* mchango wangu utabaki kama ulivyo na yeze atabaki na maelezo yake kama alivyoyatoa.

**NAIBU SPIKA:** Hautabaki kwa sababu nimeshatoa maelekezo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *that's a biasness thing*, mimi kama Mbunge natakiwa kuchangia ninachokielewa. Niko hapa kuisimamia na kuishauri Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko huwezi kuchangia kitu ambacho kipo kinyume na sheria. Sheria...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe umekiri hujui inavyosema...

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Esther Matiko. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji; Mheshimiwa Mwita Getere, atafuatiwa na

Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara ya Mambo ya Ndani. Cha kwanza, naomba nimshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani, somo yangu, Mheshimiwa Simbachawene; Naibu Waziri ambaye anamsaidia kazi; Makatibu wa Wizara hii, Makamanda wote wa mikoa na hasa Mkoa wa Dodoma ambao Kamanda wake anatalinda hapa kila siku, tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie, nimesoma maeneo mengi humu ndani, nishukuru sasa na Jeshi la Polisi na Magereza sasa wanajielekeza kwenye miradi mikubwa ya kimaendeleo. Kuna wakati fulani nilikuwa najuliza huwa nikitembelea Magereza na MaPolisi walivyo huwa najuliza hivi mishahara ya Magereza huwa ni midogo kuliko ya Polisi au inakuaje? Maana yake unakuta wakati fulani Magereza afya zao hazijakaa vizuri. Hata hivyo, nafikiri kwamba hawa wanajitesa wenyewe, wana maeneo makubwa sana ya uzalishaji na wana rasilimali watu, wanao kule ndani. Kwa hiyo naona sasa ni wakati muafaka wafanye kazi ya kutafuta hela kwenye maeneo yao. Naona miradi mikubwa mikubwa inakuwepo na Polisi nao wamejingiza sasa wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vitengo ambavyo nimeviona wamevipunguza sana makosa wenzetu wa Polisi, lakini kuna jambo moja nalionna wanatakiwa kulifanyia kazi. Mabodaboda wetu kwenye maeneo mengi, ukiangalia kwenye vituo vya Polisi vingi sasa yaani pikipiki zilizoko pale utafikiri ni mtama au mahindi yaliyovunwa kwenda kuweka kwenye maeneo hayo. Unajuliza mara mbilimbili ni kitu gai hiki? Ni jambo gani lifanyike sasa la maana ili kupunguza makosa ya pikipiki haya ya bodaboda *at least* wafanye kazi wale vijana. Kwa sababu bodaboda hawa wanunuua pikipiki kwa ajili ya kufanyi kazi, sasa pikipiki inakamatwa leo anakimbia anaiacha, anakamatwa leo anakimbia anaiacha; hapana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Waziri na Kamanda Sirro lazima wafike wakati sasa walialangalie hili jambo. Kama ni mafunzo yatolewe ya kutosha kwa bodaboda, kama ni makosa ya kawaida tuangalie namna gani tunaachia zile pikipiki. Haiwezekani Vituo vya Polisi vyote sasa vikashindwa kuweka mahabusu sasa mahabusu yaliyoko pale ni pikipiki. Hiki kitu kinaleta walakini, nafikiri kwamba ni bora sasa twende tukaangalie namna gani tunafanya jambo hili liwe zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia suala la *NIDA*; *NIDA* ni tatizo, sasa najiuliza mambo mawili; aidha viongozi walio kwenye sekta ya *NIDA* uwajibikaji wao ni mdogo au kuna walakini pia wa upungufu mwingine waa kifedha kama wanavyosema watu. Nasema hivi kwa sababu, haiwezekani kwa sababu mimi kwenye eneo langu la jimbo, kata zote za kwangu zinalalamika juu ya *NIDA*. Watu leo wanani pigia simu niombee *NIDA* mimi sijapata, simu zimefungwa.

Sasa tunataka kuangalia hili tatizo la *NIDA* likoje; Waziri naomba alifuatilie ili tuweze kuona kwa namna gani tunamaliza tatizo hili, kwa sababu hili jambo ni nyeti sana katika nchi yetu. Kwa hiyo nalo lazima tuangalie namna gani tunalitatu ili vijana wetu na wananchi wetu kwenye maeneo mbalimbali wapate nafasi ya kutumia simu zao vizuri. Wengine wamefungiwa mpaka leo hawajui jambo la kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza kwenye ujenzi wa nyumba za Polisi; kwa kweli wakati fulani huwa najiuliza, Polisi ukimtzama kawaida akikukamata unaweza ukadharau, ukasema huyu naye labda anatafuta hela au anapenda rushwa na nini, lakini ukijuliza hivi leo kama hakuna Polisi katika nchi yetu inakuwaje? Hivi leo mimi naweza nikalala pale au mtu mwingine hata kama nina nguvu kiasi gani mtu ananitukana tu barabarani, naogopa kumpiga kwa sababu Polisi yupo, naogopa kumnyang'anya mali yake kwa sababu Polisi yupo. Kwa hiyo Polisi ni watu muhimu sana katika nchi yoyote duniani hapa. Kwa hiyo cha msingi tuwawekee mazingira mazuri ya kuwajengea nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Polisi analala nje, mazingira yake ni machafu hata maadili yake yanakufa. Kwa hiyo tumshukuru Mheshimiwa Rais kwenye hii Awamu ya Tano kwa kweli hali ya kuwajengea Polisi nyumba za kusihizimekuwa kubwa sana, nimeangalia bajeti hapo inavyoenda vizuri, lakini tuendelee kuhimiza Magereza wapate nyumba, Polisi wapate nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo langu la Bunda kuna Kituo cha Polisi Nyamswa cha miaka hiyo ya Chifu, kingine kinaitwa Mgeta, Naibu Waziri alikuja pale akakiangalia kile kituo, hali yao ni mbaya, akatuahidi atatujengea nyumba pale, akaahidi atatoa hela, sasa nakwenda kumaliza *term* ya Ubunge hela sijaiona. Sasa haya maneno gani tena!

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, Kituo cha Polisi cha Nyamswa na Kituo cha Mgeta wavipelekee hela ili wawewe kujenga Vituo vya Polisi na wenyewe waishi kama Polisi wengine wanavyojengewa nyumba. Kwa hiyo naomba hili nalo tulichukue kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani hatuwezi kuzungumza bila kuzungumzia suala la *corona*, lakini kabla ya *corona* nilikuwa naona dada yangu pale anang'ang'ana na mambo ya helikopta. Helikopta ya Polisi ni sehemu ya ulinzi wa Polisi. Mimi najiuliza, hivi kweli kama sasa Wanchali na Wanchoka wanapigana kule Tarime, hivi Sirro atatokea na gari kutoka Dar es Salaam mpaka Tarime kweli? Hivi haya ni maneno gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, huo mchango umeondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa hiyo ukianza hapo mtu hataelewa ulipoanzia ni wapi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Nilitaka kumpasha tu aelewewe kwamba helikopta siyo ya kutembelea, ni ulinzi ule.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere tuelewane kwanza...

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Nimetoa hayo maneno.

**NAIBU SPIKA:** Hiyo habari unayojibu haipo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa.

Mheshimiwa Niabu Spika, nataka nizungumze suala la *corona*. Nimshukuru Mheshimiwa Rais jana ametoa maelezo, maana yake kulikuwa na maneno kwamba Rais atoke nje atoe maelezo, jana ametoa maelezo ya kutosha. Nimpongeze Rais, kusema kweli kuna watu mnawazawaza humu lakini ukweli niliwahlil kusikia kauli ya Mwalimu Nyerere anasema katika Taifa hili la Tanzania kuna viongozi wazuri kabisa, waadilifu na wenye maono. Nikawa najiuliza, wapo kwelim mbona tumebakina wapiga dili? Kumbe Rais Magufuli naye yumo humu ndani, anafanya kazi ya maono ya kuona mbali, amekwepa mtego wa *lockdown*, mtego ambao umewashinda wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Marekani pamoja na wapambe wake umemshinda, India umemshinda, China umemshinda. Leo Wamarekani wametoka nje, wanasema tunadai uhuru, hatutaki kufungiwa ndani wametoka nje imeshindikana, lakini Rais amekaa na mawazo yake na maono yake ametukinga na *lockdown*. Watanzania wanyonge leo wangefia ndani. Watu wanaofuga kwa mfano maeneo ya kwetu kule ndani sisi hatujafikia kiwango, kuna watu kwenye nyumba moja ndiyo unakaa pembeni yake kuna mbuzi, kuna kuku, kuna nani, unaweka *lockdown* humu ndani, mimi nakufa na ng'ombe wangu humu ndani hivi inakuwaje, ingekuwa hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo *South Africa* Rais Ramaphosa anasema ataongeza Polisi 73,000 walinde watu wa *lockdown*; hivi sisi tunaweza hiyo kazi, kazi hiyo Polisi wa

Tanzania milioni sita wa Dar es Salaam tunaweza? Rais ametuepusha na jambo la *lockdown*, ni Rais mwenye maono, tumpongeze kwa hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanajuliza Madaktari duniani kwamba ni lini *lockdown* itaisha. Watu wanajuliza ni lini virusi va *corona* vitaisha, kama haviishi *lockdown* ni nini? Sasa haya ndio mambo, lakini Rais ameona mbali, watu wameona mbali. Ametuambia habari ya barakoa, tumeona nchi nyingine zinapingga, kwa hiyo amezungumza mambo mazito, tunampongeza Rais kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Getere. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Almas Athumanii Magie, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Khatibu Said Haji, ajiandae.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ili nichangie hii hoja ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2020/2021. Leo nitajikita kwenye taarifa yetu ukurasa wa 29 ulioongelea mambo yanayohusu Sekta ya Ulinzi Binafsi. Kabla ya hapo nimpe pole sana Mheshimiwa Waziri Simbachawene kwa kuondokewa na mzazi wetu, lakini vilevile nikupe pole wewe kwa kuondokewa na mwenzetu Mheshimiwa Mchungaji Getrude Rwakatare.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze pia kumpongeza Mheshimiwa Simbachawene kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na hivyo kukutana na mimi kwenye Kamati yetu ya NUU; karibu sana. Pia nimpongeze Mheshimiwa Zungu aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii, sasa ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo sasa naomba nichangie katika Sekta ya Ulinzi Binafsi, kama ilivyoelezwa katika taarifa ya Kamati yetu ukurasa wa 29, *item*

ya tatu. Sekta ya Ulinzi Binafsi ilianzishwa hapa kwetu mwaka 1980 ikianza na makampuni mawili tu, lakini sasa yapo makampuni 1,230. Sekta hii ilianzishwa kutokana na ombwe lililokuwepo la kulinda mali za watu binafsi ambazo zilikuwa zimetaifishwa na Azimio la Arusha la mwaka 1967. Mali ziliporudishwa ambazo zilikuwa zinalindwa na askari wa mgambo na Polisi, zikabakia patupu. Ndipo /GP alikuwepo bwana Philemon Mgaya akatakiwa kupeleka ufumbuzi wa kulinda mali hizo na ye ye akaomba siku mbili na aliporudi kwa Mheshimiwa aliywemwita kumuelezea akasema anayo *solutionsasa*, analo jibu la kupata ulinzi wa mali hizo na ndipo yakaitwa makampuni mawili hayo ya *Group Fourn Ultimate Security* kutoka nje ya nchi kuja kuanzisha ulinzi huo hapa. Hata hivyo, hapakuwepo na *GN*, sheria wala kanuni iliyoanzisha Sekta ya Ulinzi Binafsi nchini na imekuwa hivyo kwa miaka 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni haya tangu yalipoanzishwa mpaka sasa yameajiri jumla yake karibu askari 2,500 kutoka na kuingia, lakini kwa muda wote askari 350,000 wameajiriwa katika Sekta ya Ulinzi Binafsi. Hii inaonesha umuhimu wa sekta hii hapa nchini, inaonekana kila mahali na tunashukuru sana *SUMA Guard*, wamechukua nafasi kubwa, wana karibu askari 7,000 katika Sekta hii ya Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari yake ya kutokuwa na sheria; makampuni haya yalipoanzishwa yalianzishwa na wataalam wa Jeshi, Majeshi ya Magereza, Majeshi ya Polisi, Majeshi ya Ulinzi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, walioanzisha makampuni haya miaka 40 iliyopita wameshafariki na kama wapo ni wazee kokoro, walikuwa wamestaifu ujue, ndiyo wakaanzisha makampuni haya wakiwa na miaka 50,60 sasa ongeza 40 wana miaka 90 au walifariki. Makampuni haya kwa sasa yanaendeshwa na watu waliorithi makampuni haya ambaao sio askari, ambaao hawana taaluma ya ulinzi, lakini wanaajiri watu ambaao hawana taaluma ya ulinzi, wanaajiri watu tu kuendesha sekta hii nzito yenye umuhimu wake na matokeo yake mmeyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni mmeshuhudia matukio makubwa sana yaliyotokea katika sekta hii. Kwanza alitumwa bwana Kasusura kwenda kuchukua dola milioni mbili, akaondoka nazo kule *airport*. Halafu kulikuwepo na askari waliotumwa kupeleka hela za mishahara katika benki za *NBC* wakavua nguo huko Kawe wakaondoka na hela zote. Halafu kulikuwa na wizi mkubwa, zaidi ya bilioni tano kule Moshi walishiriki walinzi hawa, lakini hivi karibuni mmesikia kumetokea wizi wa trillioni moja na nusu karibu au na zaidi iliyoibiwa. Walitumwa askari hawa walinzi wapeleke hela hizo kwenye benki na wakazichukua. Walipotumwa Polisi na wao nasikia sijui ilitokea nini huko, maana nimesikia tu Polisi nao walikamatwa walioenda kukamata hela ambazo zimeibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni mmesikia kumetokea wizi wa shilingi trillioni moja na nusu au na zaidi. Askari wale walitumwa wapeleke hela hizo benki na wakazichukua. Walipotumwa Polisi na wao nasikia sijui kilitokea nini huko, maana nimesikia tu Polisi nao walikamatwa walioenda kukamata hela ambazo zimeibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, dawa yake ni kutunga sheria ya sekta ya ulinzi nchini. Sheria hiyo ndiyo peke yake itakuwa muarobaini kwani sheria zote zilizopo haifanyi kazi kwenye sekta ya ulinzi. Inapotokea kupotea mali ina maana sheria hiyo tunayodhania ipo ndiyo imepotea na sekta ya ulinzi ikapoteza mali. Kanuni na sheria zote, *Criminal Law*, *Criminal Procedures*, *Penal Code* au Sheria ile ya Ushahidi haifanyi kazi, inafanya kazi baada ya mali kupotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na mambo mabaya sana katika sekta hii. Licha ya mali kupotea ambayo sasa haiwezi kurudishwa katika nchi nyingine ambako sekta hii ilitokea kuna Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi (*Private Security Industry Act*) ambayo pia inaunda Mamlaka ya Sekta ya Ulinzi Binafsi (*Private Security Industry Authority*) ambayo inasimama kama *EWURA* au *LATRA* na kadhalika. Kwa hiyo, waajiri wa sekta ya ulinzi binafsi wanakuwa makini kwa sababu sheria zile zinawahuishwa wao pale ambapo walinzi watafanya makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hapa tunajaribu kutumia *vicarious liability* na Sheria ya Ukaribishwaji wa Muajiri ambapo waajiri wamekuwa wanakwepa, kwa hiyo, haitusaidii sana lakini kama sheria hii ya sekta ya ulinzi binafsi ingekuwepo ingesaidia kurejesha mali ambazo zimeibiwa kwa sababu makampuni yana uwezo wa kurudisha mali iliyopotea. Pia walinzi na raia wamefariki katika sekta hii na hakuna *injury repay au remedy*. Njjia pekee au tunaita muarobaini ni kutunga Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipoingia Bungeni nilipendekeza sheria hiyo na ilichukuliwa na Serikali na Serikali ikasema ingeileta, sasa ni mwaka wa tano mimi naondoka sheria hiyo sioni. Kwa hiyo, napenda Waziri atakapokuja atuambie sheria hii imefikia wapi kwa sababu ni muarobaini muhimu kwa maisha ya raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana Mheshimiwa Almasi Maige. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Anna Lupembe, sijui yuko humu au Msekwa, aah yuko humu ndani, Mheshimiwa Khatib Said Haji atafuatia na Mheshimiwa Ally Hassan King ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi. Vilevile naomba nikupongeze wewe pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kazi kubwa mnayofanya katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutusimamia ili kuweza kufanya kazi zetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa uzima na uhai ambaa anaendelea kunipa. Naomba nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Waziri Mkuu, wanafanya kazi kubwa sana katika nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru na nimpungeze sana Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Naibu Waziri kwa kazikubwa wanayofanya katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Pia nimpungeze *IGP* pamoja na Makamishna wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpungeze sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wetu wa Katavi, Mkuu wetu wa Mkoa Comrade Homela kwa kazikubwa sana anayoifanya ndai ya Mkoa wetu wa Katavi. Alifanya *operation*, alikusanya silaha nyingi sana katika Mkoa wetu wa Katavi na leo hii Mkoa wa Katavi upo shwari kutokana na hali halisi ya usalama. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpungeze sana *RPC* wetu wa Mkoa wa Katavi. Hata hivyo, *RPC* huyu mpaka leo hana ofisi, anatumia Ofisi ya *OCD* wa Mpanda. Sasa *RPC* hana ofisi wala makazi katika eneo analofanya kazi. Naomba sana basi huyu *RPC* aweze kutafutiwa nyumba kwa sababu tayari kiwanja kipo, aletewe pesa aweze kujenga nyumba ya ofisi yake pamoja na nyumba ya makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi jiografia yetu ni ngumu sana, kila siku nazungumza, lakini bajeti tunaletewa ndogo sana kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kipolisi. Ukiangalia asilimia kubwa ya Mkoa wa Katavi ni mapori, kwa mfano, Wilaya ya Mlele *OCD* anakaa Inyonga, Makao Makuu ya Wilaya, lakini changamoto kubwa ziko katika eneo lingine ambalo ni kilometra 80 kutoka Inyonga mpaka Mpimbwe, kule ndio kwenye watu wengi na mambo mengi na matukio mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ina maana *OCD* anatoka Inyonga kila siku kilometra 80 na magari yetu bajeti yake ya mafuta ni ndogo sana, ma-*OCD* wetu wanapata shida sana kutokana na jiografia. Ukiangalia hili Bonde la Mpimbwe lina wakazi wengi sana, naomba Wizara itizame basi katika eneo hili kijengwe kituo kingine kikubwa ambacho kinaweza kuwekwa *OCD* mwengine kwa sababu kuna Halmashauri mbili, kuna Halmashauri ya Mlele na Halmashauri

ya Kavuu. Nashauri na huku nako wapate *OCD* mwingine kwa ajili ya kuweza kufanya kazi vizuri kutokana na jiografia jinsi ilivyokaa vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia jinsi ma-*OCD* wanavyopata shida hata pia katika Wilaya yetu ya Tanganyika. Wilaya ya Tanganyika nayo ina maeneo mbalimbali, huyo *OCD* yuko Makao Makuu ya Wilaya, akitoka pale akienda Mishamo ni kilometra 130, akitoka Makao Makuu ya Wilaya akienda Kalema ni kilometra 130, mafuta bajeti yake ni ndogo sana wanapata shida na bajeti kwa ujumla ya vifaa vya kutengenezea magari nafikiri mnaelewa jinsi gani wanavyofanya *operation*, ukizingatia Mkoa wetu sisi wa Katavi, hususan Wilaya yetu ya Tanganyika imepakana na *border*, imepakana na Kongo, Burundi na Zambia kuna kazi kubwa sana Wakongo wanaingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna *operation* ya ugonjwa wetu huu ambaa umekuja katika dunia wa *corona*. Juzi tu wamekamata wananchi wa Zaire watatu wana ugonjwa wa *Corona* wanaingia nchini kwetu Tanzania, ni shida. Sasa hawa ma-*OCD* wetu au viongozi wetu na maaskari kama hawana vifaa maalum kwa ajili ya kufanya kazi itakuwa shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kuitia Waziri, Wizara hii ni sikivu. Kwanza tunaomba tuwapongeze sana kwa kazi kubwa mnayotufanyia katika Wilaya hii ya Tanganyika, mmetujengea ofisi, wafanyakazi maaskari mmewajengea nyumba nzuri sana, naomba nipongeze sana kwa hilo, lakini tunaomba tuangalie kutokana na jiografia ni ngumu magari yale hata mkileta kwa muda mfupi sana yanapata uharibifu na kupata pesa za vipuri na nini inakuwa shida. Naomba sana msaada ya bajeti wa Mkoa wa Katavi, hususan mkoa mzima iweze kuongezwa ili tuweze kupata unafuu kwa ajili ya mkoa wetu jiografia yake ni ngumu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizungumzie kuhusu Uhamiaji. Kama nilivyosema katika Mkoa wetu wa Katavi tunapakana na Burundi na Zaire. Kwanza naomba

nimpongeze Kamishna wa Uhamiaji alithubutu kuja Katavi na alienda mpaka Kalema. Naomba nimpongeze sana dada Anna kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya katika nchi yetu. Ni mwanamke ambaye ni jasiri sana. Nilivyomuona amekuja Katavi nilibaki nashangaa lakini nilijua wanawake tunaweza na tunapambana. Naomba tuendelee kumpongeza Anna kwa kazi kubwa anayofanya ni kazi nzuri sana. (*Makofj*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini changamoto ya Uhamiaji ndani ya Mkoa wetu wa Katavi hawana vifaa, hususan magari ya kufanya kazi. Wanapata changamoto sana kwa sababu ndani ya Mkoa wetu wa Katavi tuna Ziwa Tanganyika wahamiaji wanaingia kutokea katika maeneo hayo. Naomba tuwatafutie vifaa ili waweze kufanya kazi nzuri zaidi. Ndiyo hao waliokamata hao Wakongo watatu ambao walikuja katika nchi yetu ya Tanzania na *Corona*. Naomba sana tuwasaidie vifaa Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze Idara ya Zimamoto Katavi. Idara hii inafanya kazi nzuri sana lakini nao hawana vifaa. Wanafanya kazi kubwa, kuna kipindi katika maeneo fulani tulipata majanga ya mafuriko, Mkuu wa Zimamoto wa Katavi alifanya kila njia kuwaokoa wananchi wale waliopata mafuriko haya lakini hana vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna majanga mbalimbali ambayo yametokea ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, hususan Wilaya ya Mpanda, soko liliungua, lakini mwanamke huyu alifanya kila jitihada kuweza kuokoa mali za wananchi wa Mkoa wa Katavi, hususan Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene wewe ni msikivu pamoja na Naibu Waziri, naomba sana uje uangalie mazingira yetu ya Mkoa wa Katavi. Pia njoo uangalie watu wako na Mkuu wetu wa Mkoa Comrade Homera kwa kazi kubwa wanayofanya ndani ya Mkoa wetu wa Katavi. Najua Mheshimiwa Waziri amenisikia, bajeti ya Mkoa wa Katavi itaiiongezwa kutokana na hizi changamoto tulizokuvanazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Hassan King, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuweza kusimama na kuongea katika Bunge hili leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nataka nitoe shukrani zangu za dhati pia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jana kutoka akalihutubia Taifa na hotuba yake ilikuwa ni dira ya wapi tunapoelekea katika kipindi hiki kigumu. Kwa kweli, katika hotuba ile nataka nimpongeze kwa mambo mawili, japo mengi ni mazuri ya kupongezwa, lakini nataka nigosie haya mambo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kuziomba taasisi za fedha licha ya kusogeza mbele mikopo bali kuzitaka zisamehe pia madeni yao kwa nchi masikini, hili ni jambo kubwa sana. Mimi naomba taasisi hizo zizingatie maombi ya Rais wetu Mheshimiwa JPM. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo limenivutia sana kwenye hotuba yake Mheshimiwa Rais jana ni namna alivyouona upuuzi uliofanyika Dar-es-Salaam, kwa kweli, nalo ni jambo nimelipongeza sana. Siku ile mimi nilikuwa Dar-es-Salaam niliuona ule usanii uliokuwa ukifanyika, vinapita vi-pick up eti vinapuliza dawa kwa kweli, tukashangaa hii ni nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulikabili janga hili lazima Taifa liwe na sera ya pamoja kuliende. Hawezi kukurupuka Mkuu wa Mkoa mmoja akaanzisha utaratibu ambao kivingine unaweza kutafsirika labda kwamba ana watu maalum katika mkoa wake na wengine hawastahiki

huduma ile. Kama ni huduma ya kuwasaidia Watanzania ni huduma inayostahiki Watanzania wote. Kwa hiyo, nampongeza Rais kwa sababu hauwezi kuwa upuuzi bila kuwepo mpuuzi aliyeufanya, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na vyombo vyetu vimepewa amri naamini vitatekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais kwa haraka sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niongelee kuhusu masuala ambayo yamekuwa yakiendelea Zanzibar. Kumekuwa na matukio ya watu kupigwa, kuna makundi ya watu ambaao wamebandikwa jina lisilo rasmi la Mazombi Zanzibar, wamekuwa wakiendesha uharamia wa kuvamia watu na kuwapiga. Haya matukio yameshasababisha mauwaji, taarifa ziko na mwezi uliopita tu yuko raia mmoja anaitwa Mohamed Omar Makame, Mkazi wa Bububu, alipigwa vibaya sana na mitandao mingi ilimtangaza mtu yule. Hata Mheshimiwa Nalbu Waziri nilimtumla picha ya mtu yule na sulubu alizizipata. Tukio limeripotiwa Polisi Bububu...

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ngoja niivue...

*(Hapa Mheshimiwa Khatib Said Haji alivua barakoa )*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Daah, napumua kwa taabu sana, ngoja nipumue kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tukio limeripotiwa...

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Khatib, kiafya inabidi uitoe kabisa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa eeh?

**NAIBU SPIKA:** Inabidi ufungue kwanza, usiishike hapo unaposhika.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, aah, hii imesha-expire hii.

**NAIBU SPIKA:** Fungua huko nyuma halafu uitoe.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Imesha-expire siigusi tena kwa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tukio limeripotiwa Polisi Bububu lakini imekuwa ni mazoea vyombo vyetu; na hili nataka Mheshimiwa *IGP*kama yupo hapa alisikie kwa umakini sana. Matukio kama haya yamekuwa ni endelevu ambapo si matukio ambayo yanalijengea heshima jeshi letu kwa sababu wananchi wanashindwa kuchukua hatua kukabiliana na watu wa namna ile wanapowavamia kwa kudhani wako nyuma ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana alikufa mtu kwa kuchukuliwa katika mazingira haya akapigwa na watu wa aina hii. Juzi tayari tukio hili ninalolisema raia huyu amepigwa na hadi sasa yuko katika hali mbaya sana. Naomba Mheshimiwa Waziri Simbachawene, Mheshimiwa Naibu Waziri, matukio haya yanapotokea yawe na mrejesho wa kujuwa waliohusika wamefanywa nini maana yamekuwa ni endelevu, ni ya kila siku. Hayaleti heshima kwa nchi iliyostaarabika kama yetu. Naomba sana suala hili lichukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza, leo kwenye Gazeti la Uhuru nimeona taarifa imeandikwa hapa kwamba kuanzia sasa askari Usalama Barabarani ni ruksa kupiga picha za *speed* kwa kujificha. Hili tukio Waziri aliyepita alilikomesha kwa sababu alijua kupiga picha kwa kujificha kuna matukio mengine yanayofanywa, askari wasio waaminifu wanajificha sehemu ambazo hazina *speed limit* na wanatumia mwanya huo kuwabambikizia raia makosa. Kwa hiyo, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni; pamoja na yanayomkabili Mheshimiwa Kangi lakini katika hili aliwatendea haki sana raia. Lengo la kamera zile ni kuelimisha zaidi kuliko kutafuta maslahi ya *fine*. Nadhani hilo limeeleweka litatolewa ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naipongeza sana Kamati hii ya Ulinzi na Usalama kwa kuiona hatari iliyopo katika magereza ya mlundikano wa mahabusu. Naipongeza sana Kamati wametimiza wajibu wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya mlundikano wa mahabusu magerezani ni kushindwa kwa vyombo vyaa upelelezi kutimiza wajibu wao na kwa wakati, hili ni jambo lisilo na shaka. Kama vyombo vyaa upelelezi kabla ya kupeleka mashtaka Mahakama wanajiridhisha na kinachopelekwa yasingetokea matukio haya ya mlundikano wa mahabusu magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunavyozungumza hapa, kesho ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhan tunaanza rasmi, wako washtakiwa, Mashekhe wa Uamsho Zanzibar wanaalngia mwaka wa nane, upelelezi haujakamilika. Mwaka wa nane tunakwenda, tunahesabu na suala hili nimekuwa nikilisema kila mwaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mashtaka yao hakuna ushahidi iangaliwe namna nyingine, tunaipa Mahakama lawama isiyostahiki. Mahakama ni *industry, raw material* ya Mahakama ni upelelezi uliokamilika na unaosheheni ukweli ndiyo inaweza kuamua. Sasa watu mnawarundika ndani hamuapelekei ushahidi Mahakama mnategemea nini? Leo mwaka wa nane Mashekhe wa Uamsho wanaendelea kusota magerezani, ni lini mtapata ushahidi wa wazee wale? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Rais anayo mamlaka ya kuwasamehe wafungwa walioko magerezani. Kwa huruma ya Mheshimiwa Rais naamini wale wamekuwa wametendewa haki hata wangestahili kufungwa, nina hakika kama alivyowahurumia wengine na wale wangefaidika na msamaha wa Mheshimiwa Rais. Kwa nini tunaendelea kuwaweka watu wale magerezani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri hebu toeni majibu. Familia zile zinalalamika, watoto wao wanataka

mapenzi ya kuwaona wazee wao lakini si kosa kuwashtaki, kosa ni kutokupeleka ushahidi wakapewa haki yao inayostahiki ambayo ni hukumu ya haki. Hebu fanyeni haki katika Mwezi huu wa Ramadhan. Lioneni hili wale ni binadamu wanaumia, wanateseka, mnataka nini? Mungu atatuhurumia vipi sisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka rehema ya Mungu wakati sisi hatuhurumiani? Hebu kwanza tuanze kuwahurumia wanadamu wenzetu, Watanzania wenzetu, raia wetu katika kuwatendea haki ili tutegemee rehema ya Mwenyezi Mungu *otherwise*, acha *Corona*, yatazuka zaidi ya *Corona* kwa dhuluma wanayofanyiwa watu hawa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khatib, hayo uliyomalizia mwisho, vigogo wa dini wa nchi hii walikusanyika jana Dar es Salaam na wewe naamini ni kati ya watu waliokuwa wanaomba Ijumaa, Jumamosi na Jumapili iliyopita. Kwa hiyo, corona haitashuka kwa *style* hiyo ambayo umeiombea hapo mwisho. (*Makofi*)

Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa nilimtaja pia Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kupata hii nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya maendeleo kwa ajili ya Jeshi la Polisi na Mambo ya Ndani na Idara zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai pamoja na kutuweka kuwa wazima tukahudhuria hapa tukachangia bajeti hii. Cha kwanza napenda kuishukuru Serikali kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani hasa hasa kwenye Jeshi la Polisi kwa sababu kule tayari kumefanyika mambo ya makazi, kwa askari wetu katika mikoa takriban yote ya Zanzibar na mambo mengine yanaendelea pamoja na Mkoa wangu wa Mjini, majengo pale Fuoni tayari ujenzi umeshaanza. Pia wametupatia ile adha iliyokuwa ikiwakera wakazi wengi wa

ziwani polisi. Hivi sasa kule kuna choo kimejengwa cha mfano na kizuri tu kinaendelea kujengwa na kingine nafikiri tunaweza tukaja tukakifufua kikaendelea vizuri. Hizo ni pongezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, rasmi kabisa katika siku ya leo nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kufanya kitu kimoja ambacho ni kikubwa sana katika hii dunia. Kitu ambacho aliyewahi kufanya ni mtu mmoja tu, aliyewahi kufanya Mfalme ambaye alioteshwa ndoto, akamtafuta Nabii Yusuf aaulizwa Nabii Yusuf kujibu ndoto ile ya kwamba akasema limeni, itakuja miaka shida, baadaye vingine viacheni kwenye mashuke. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndoto ile ya yule mfalme ni sawasawa na Rais wetu ambaye ndiyo mkuu wa nchi hii naye amepewa ilhamu hiyo hiyo, akatuambia limeni! Kule katika Surat Yusuf anaweza kusoma Maulamah kama mimi kuanzia Aya 46 mpaka 49, mkienda Surat Yusuf mtaikuta. Anaambiwa; Yusuf *Ayyuha Swiddiq, aatwina Fiihy, Sabbi dakaratisimali, yaakuluhunna – Sabuunijaa wasabuu – Sumulati hudhur wasabuuyaamisati laalliy – ardhi ilannasi laalahum – yaalumun*, Yusuf tuambie katika mambo haya, Yusuf akatoa pale na baadaye chakula katika nchi ile kikafurika na watu nchi za jirani wote walitegemea nchi ile na mimi naamini katika Ilham ambayo ameisema Rais wetu, nchi nyingine zitatutegemea kwa chakula. Kwa hiyo Watanzania tulime. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine nije katika Idara ya Vitambulisho, nina takwimu nyingi sana katika Idara ya Vitambulisho. Vitambulisho ambavyo vilivyotarajiwa kwa mujibu wa *NBS* vilikuwa ni milioni 27 *point something*, lakini vitambulisho ambavyo vimeshuka ni milioni 6, ni sawa na asilimia 21.9.

Kwa hiyo, hapa tunaonekana kwamba vitambulisho hatujafanya vizuri. Lakini sitaki kwenda huko, nakwenda kwa sababu raia waliojisajili kwenye simu bila kitambulisho, waliambiwa wana makosa na watafuatiliwa, hili ndilo

ninalolitaka, ndiyo lengo langu. Kwenye Idara hii ya vitambulisho, vitambulisho vilivyotumika kusajili simu au *line*, milioni 37, ni vitambulisho milioni 11.5 or point 6.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukitazama kwamba Watanzania ukigawa hapa kwamba kila mwenye kitambulisho kimoja amesajili *line* tatu na hiki kitu sio kweli. Watu wamesajili *line* kwa sababu wengine hawana vitambulisho lakini wamewatumia watu kuwasajilia, kosa ni la nani? Kosa ni la Idara ya Vitambulisho. Idara ya Vitambulisho, tumesema kwenye Serikali kwamba watu wakasajili simu kwa kutumia vitambulisho wakati vitambulisho vilivyotoka ni milioni 6. Je, milioni 50 au milioni 43 watu waliokuwa na *line*, milioni 43 kwa mujibu wa TCRA, ni lazima watu watafanya kosa, ni sawa sawa na baba nyumbani, amekaa na watoto wake, awaambie, nawapa dakika kumi, kila mmoja aingie kitandani alale. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo wengine wako *mile* 100, hawako pale nyumbani. Je, hawa wa *mile* 100 kwa dakika 10 watafika kulala? Kwa hiyo, watoto waliowahi kuwa nyumbani, wakapanga mito, mashuka na nguo ili wale wenzao wasije wakakutwa na madhara. Kwa hiyo, hii ndiyo kadhia ya vitambulisho, kwa hiyo hawa amba wamesajiliwa *line* ni wale watu ambao wamelaza mashuka, mito, kwa hiyo Idara ya vitambulisho tunaomba wajaribu kulifuatilia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala jingine nazungumzia katika Jeshi la Polisi linaongoza katika usalama barabarani. Viongozi wetu wanapita. Nilishashuhudia, si mara moja wala mbili kwamba misafara inaongozwa kwa simu za mkononi, je likitokea atajibu nani? Zantel, Tigo, TTCL au nani? Sisi tulivyokuwa tunafahamu kwamba polisi wana mfumo wao wa mawasiliano, mfumo wa simu unaona kama sio *reliable* kwa sababu litakapokua kutokezea nani atajibu? Je, mitandao imegoma kama inavyotugomea wakati mwingine, unapiga mwenye *line* hapatikani, jambo gani litatokea? Kwa hiyo, nilikuwa naomba katika jambo hili, Jeshi la Polisi liende vizuri. Kuna shilingi 180,000 ndiyo zilizotengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni ujenzi wa Kituo cha Mkokotoni, najua kuna umuhimu lakini pale Mkokotoni kuna Bandari, Bandari ya Mkokotoni inapitisha vyombo kutoka Pemba, kutoka Mombasa na kunapitishwa mambo mengi sana na kule Kaskazini kwa kwetu sisi pale Unguja ni ukanda wa utalii. Kwa hiyo, kituo kile kikichelewa kujengwa au kama kilivyokuwa *proposed* tokea 2004 mpaka leo hakijajengwa, kuna hasara kubwa sana inaweza ikajitoneza. Kuna hasara kubwa sana inaweza ikajitoneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, Mheshimiwa Waziri alieleza hapa kwamba zimetengwa shilingi milioni 500, ameleeza hiyo katika hotuba yake katika ukurasa wa 25 *paragraph* ya 77. Lakini fedha hizi zilipaswa zitoke kwasababu tokea miaka mingi sana zinapangwa hazitoki, je, na hizi tuamini zitatoka? Hilo ndilo swali langu kwa Mheshimiwa Waziri. Je, hizi tuamini nazo zitatoka? Kwasababu kuna umuhimu. Pale Mkokotoni sasa hivi kuna *combination* kama ilivyokuwa mjini sasahivi, kule Kaskazini iko hivyo. Kule kuna mambo mengi ya utali na kuna vitu vingi sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naomba jambo hili litazamwe kwa umakini zaidi ili athari zisije zikajitoneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBI SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Augustino Holle Vuma ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya miaka mitano chini ya uongozi wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, jambo kubwa ambalo amelifanya kwa Watanzania ni kudumisha amani na utulivu katika nchi yetu, nampongeza sana Mheshimiwa Rais. Lakini amefanya hivyo, kupitia Jeshi la Polisi, sote tunajua ilifika mahali, majambazi ndiyo yalikuwa yanatawala nchi yetu.

Yalikuwa na uwezo wa kwenda benki na kuchukua hela, yalikuwa na uwezo wa kwenda kwenye vituo vya polisi na kunyang'anya silaha lakini mbaya zaidi ni kwamba majambazi haya, ili usafiri kutoka Mwanza, au kutoka Dar es Salaam kutoka Kigoma, lazima Jeshi la Polisi lisindikize mabasi. Vivyo hivyo ukitoka Mwanza kwenda Kagera, lazima Jeshi la Polisi lisindikize mabasi hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo jambo hilo, halipo, niwapongeze sana Makamanda wetu wote Tanzania kwa kazi nzuri sana wanayofanya ya kulinda mali na usalama wa wananchi wake. Nimpongeze sana *IGPSirro*, umefanya kazi nzuri sana, sasa hivi ujambazi hakuna. Labda baadae Mheshimiwa Waziri utatumegea kidogo ili tuju nini siri ya mafanikio hayo kwasababu hapo mwanzo ukitoka tu kidogo unakutana na majambazi, Dar es Salaam pale, majambazi, Mwanza, majambazi, Arusha, majambazi. Leo hakuna majambazi! Siri ya mafanikio hayo ni nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama nilivyosema kwamba ni kwa sabbau tuane jemedari mkuu, Dkt. John Pombe Magufuli, baada ya kuwaelekeza makamanda wote wa mikoa kwamba sitaki kusikia mkoa fulani eti majambazi yanakwenda kuvamia benki, yanakwenda kuvamia vituo vya polisi, sasa hivi Dar es Salaam na maeneo mengine kuko shwari. Kwa hiyo, nimpongeze sana *IGPSirro* kwa kusimamia maelekezo ya Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la pili nipongeze sana vijana wetu, Polisi wa Usalama Barabarani, wanafanya kazi nzuri sana. Wanafanya kazi kwa shida, iwe mvua, ya kwao! Jua, la kwao! Nafikiri iko haja sasa kwetu sisi kuwaangalia hawa wenzetu. Kwa Dar es Salaam na mikoa mingine, wasiposimama barabarani hizo *traffic jam* hatuwezi kufika huku tunakofika. Kwa hiyo, lazima tufike mahali tuwaheshimu sana wenzetu hawa kwasababu wanafanya kazi nzuri sana. Niwapongeze pia *immigration* kwa kazi nzuri sana na nafikiri ni jambo zuri sana, mapungufu hayawezi kukosekana. Nimpongeze sana kiongozi wa *immigration* kwa kazi nzuri sana wanayofanya. Haya matatizo ya hapa na pale

ndiyo changamoto zenyewe. Lazima ziwepo na zitafutiwe fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya nakushukuru. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godbless Lema atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Holle Vuma. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kabla hujazuia hotuba yangu nilikuandikia *ki-memo* kizuri kweli nikakukumbusha kujikinga na corona, nikakuambia uvae na barakoa. Haijaisha dakika tano, ukaniifanyizia! Sasa nimefurahi kwamba hotuba yangu imezuiwa kwasababu hata Yesu angekuwepo leo akahubiri kama wanavyohubiri watumishi wa sasa Herode asingemhukumu. Kwa hiyo, ukiona unaimba mapambio kuzimu halafu shetani hashtuki maana yake mapambio yako hayamtukuzi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka niongee kidogo, nimeomba na Mheshimiwa Rais alivyoita wito wa maombi nilifunga kwa siku tatu na naamini katika maombi na nimefika Bunge hili kwasabbau ya maombi. Lakini nyongeza ya maombi, kikao ambacho viongozi wa dini walikuwa wamekialika jana mgeni rasmi akiwa Waziri Mkuu, wakimtaka Mungu aingilie, sisi watumishi wa kiroho hatukwenda, tulikuwa tunawaangalia kwa mbali. Nilifanya mazungumzo na Roho Mtakatifu akaniambia "mwanangu pale hakuna kitu pale". Kwa sababu imeandikwa watu wangu...

**NAIBU SPIKA:** Lema, ngoja tuwape viongozi wa dini heshima wanayostahili. Wote ni viongozi wa kiroho, hii habari ya kwamba jana hakuna kitu au kilikuwepo, Mungu peke yake ndiye anayejua! Mungu peke yake! Kwa hiyo, tuwaachie wale wanaoamini kwamba kuna jambo limefanyika, tuwaachie hili. Kama wewe huamini, baki nalo mwenyewe kwasababu ndiyo yale yale tunarudi kule kule. Ukihitaji wewe heshima kama mtumishi wa Mungu basi

uwaheshimu wengine kama watumishi wa Mungu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unichungie muda wangu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, neno la Mungu linasema watu wangu wanaangamia kwasababu ya kukosa maarifa. Unakwenda kwenye maombi ya kuzuia ugonjwa unaosambaa kwa kusambazwa, yaani *corona virus* inasambazwa na binadamu, haina miguu!

Wakati unakwenda kukemea pepo la corona linalosambazwa na mtu bar ziko wazi usiku kucha, cluba ziko wazi usiku kucha, disco ziko wazi, casino ziko wazi, watu wanacheza. Tumeona hapa *DC*, wa Dodoma Patrobas Katambi anaingia *club* wakati huu wa *issue za corona virus* ambayo inakuwa *transmitted* na watu na ndijo sababu tunanawa, tunavaa barakoa, anaingia club katikati ya watu, anakuwa *hugged* anakumbatiwa na kadhalika huku anapaka *sanitizer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajiuliza, haya ni maarifa ya aina gani? yaani huyu ni Mungu wa aina gani na atai-intervene viyi kama tunashindwa kutumia maarifa. Wakati Mungu anaumba dunia hakuumba *computer*, gari, aliumba binadamu na akili, akili na maarifa inakusaidia kujua imani bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo ugonjwa, leo tunasikia wagonjwa wengine wametoroka Amana, wamepanda daladala na *DC* wa llala anasema kwamba wameondoka lakini wana *address* zao wanawafutilia, najiuliza mgonjwa aliyetoroka akapanda daladala ya watu 30, ukimfutilia ameambukiza watu wangapi? Tunapokuja kuongelea habari ya corona, Rais apongezwe kwa mambo ya muhimu yote kama anafanya lakini Mheshimiwa Rais ashauriwe na ndijo kazi ya Bunge kumshauri Rais na Bunge likimshauri Rais, Rais hawezi kujisikia vibaya kwasabbau huu ni muhimili ambao kazi yake ni kushauri Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ugonjwa ni hatari kweli, sasa leo tunaongelea Wizara ya Mambo ya Ndani, jana tu Polisi wamekuja kuzua press ya Mwenyekiti. Walipokuja Polisi wako kwenye gari 15 hawana barakoa, ni polisi mmoja tu ana barakoa. Unajiliza, hivi wakiambukizwa Polisi leo, na tunakwenda kwenye hali mbaya ya uchumi, utalii sasa hivi ni asilimia sifuri, *TANAPA* na *KINAPA* kwa siku walikuwa wanatengeneza zaidi ya bilioni moja leo. *Kamati ya Bajeti imesema hawatengenezi milioni 8 kwa siku. Maana yake ni kwamba kuna decline kubwa ya uchumi wa biashara na kukiwa na decline kubwa ya uchumi wa biashara, kutatokea uhalifu.* Maana yake ni kwamba wakati uchumi unashuka, stock market duniani zime-fall, bei ya mafuta leo leo Marekani imekwenda minus 37, hali ni mbaya! Na haya ni Mataifa ambayo...[**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Martha Mlata.

## TAARIFA

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anayeongea anapenda sana kutumia maneno ya Mungu, simlaumu, nampongeza lakini nataka nimpe Taarifa kwa jinsi anavyochangia haonekani kama yeye ni moto au baridi kwasababu yuko vuguvugu. Unazungumza habari ya watu kufanya biashara kwenye *bar* ambako na wewe unakwenda na Serikali inasema kwamba mtu akae mbali, asiende kwenye mikusanyiko na wewe unakwenda.

Leo hii unatoka pale unalaumu watumishi wa Mungu kwamba tunaomba wakati tumeacha *barziko* wazi. Naomba nikupe Taarifa, neno la Mungu linasema ni heri uwe baridi au moto kwasababu ukiwa vuguvugu kinywa cha Bwana kitakutapika. (*Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Ameen!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema unaipokea Taarifa  
hiyo?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina  
tabia hiyo lakini niseme tu kama atanipa *offer* bado  
nitaikataa. Pia mama uko tunakokula kama pale *shoppers*  
namuona na vijana wengi sana. Sasa wale vijana pia isije  
kuwa wanatoka Dar es Salaam wakaja wakamletea  
matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendele...

**MHE JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika,  
taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema kuna taarifa kutoka  
kwa Mheshimiwa Musukuma.

## TAARIFA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika,  
nakushukuru sana. Nimemsikiliza mchangiaji alipokuwa  
akichangia kuhusiana na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma  
kwamba alionekana *club*. Lakini hata yeye Mheshimiwa  
Lema alikuwa na mtoto wa Mwenyekiti wake Mbowe wakati  
anaingia *quarantine*, sasa nina wasiwasi nae na kama vipimo  
viko sahihi angepimwa ili tujue kama alitoka salama au  
alikuwa hayuko salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, endelea na  
mchango wako.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika,  
nakuomba sana unilindie muda wangu, naongea vitu *serious*  
sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa tu taarifa kwamba  
utalii ambao unachangia pesa nyngi sana kwa Pato la Taifa

umeanguka. Biashara *traders*wote waliokuwa wanakwenda China na Vietnam hawaendi. Maana yake ni nini? Maana yake, kuna *decline* kubwa sana ya *purchasing*, biashara zitayumba, nyangi sana. Biashara zikiyumba, hali ya maisha itakuwa ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais jana alisema hakutakuwepo na *lockdown* Dar es Salaam, lakini kutakuwepo na *natural lockdown automatically*, kwa sababu watu wataenda mjini lakini hawana nguvu ya manunuizi. Maana yake ni kwamba utahitaji Askari imara wenye afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema, wakati tunajiandaa na suala la afya ya wagonjwa wa *Corona* tuangalie ulinzi wa ndani ya nchi. Namna ya kuanza kuangalia ulinzi wa ndani ya nchi, Mheshimiwa Waziri upo hapa, Askari wote wanaokuwa kwenye *patrol*, mahabusu zetu zinakuwaje? Ni bora sasa hivi Shule za Msingi zimefungwa, mtumie hizi shule ku-*extend* mahabusu kuliko mtumie mahabusu ndogo watu 20, kwa sababu mahabusu mmoja akiumwa *Corona* anaweza akaambukiza Polisi wote.

Narudia, Polisi akiambulizwa Corona, anaweza akaipeleka kwa *IGP* Sirro; *IGP* anaingia kwenye Vikao vya Kamati vya Ulinzi vya Taifa, anakutana na Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais wanaweza wakaumwa. Ni kwa sababu tupo kwenye vita kubwa, tunahitaji viongozi wenye afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *Corona* haiogopi bunduki. Mwulizeni Borris Johnson kule nanii, haiogopi bunduki! Itapenya halafu utashangaa inawatandika. Sasa mimi maombi yangu, muwe salama kabisa na muwe na afya njema. Kwa hiyo, *measurements* siyo tu ku-*lockdown*; unaweza usi-*lockdown* lakini ma-bar, ma-club na ma-casino yanafanya kazi usiku kucha.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ku-*compare* maisha ya watu na *revenue*. Hela haiwezi kuwa na thamani ya roho

moja hata dakika moja, nanyi mnasema ni Serikali ya wanyonge. Msipochukua *serious measurements*, hawa wanyonge wataisha wote. Tunavyoona huko nje, watu wanakufa 4000, 5000 kwa siku, hayo ni Mataifa yenyeye nguvu ya kitabibu na kiuchumi. Naomba sana, pamoja na maombi na imani, ni lazima Serikali ije na mikakati ya msingi kabisa kwenye miji mikubwa kama Arusha, Dar es Salaam na Mwanza namna gani wanakwenda kuzuia hili tatizo. (*Makofii*)

Suala lingine ni kwamba tunakwenda kwenye uchaguzi keshokutwa. Polisi wowote duniani; awe Marekani, China au Vietnam akishindwa kusimamia misingi ya sheria na haki katika wajibu wake, hao wanakuwa ni kundi la majambazi waliosajiliwa. Popote duniani. Kazi ya Polisi *it is a noble work*, yaani hakuna kazi ya msingi na ya maana kama kazi ya Polisi kwa sababu ni mtu anayechukua *sacrifice* kwa ajili ya maisha ya watu wengine. Kwa hilo, Polisi huyu anayechukua *sacrifice* kwa ajili ya maisha, nidhamu yake inatakuwa iwe sambamba na ya mtumishi wa Mungu ambaye hatiliwi mashaka kwa sababu ni kazi ya *sacrifice*.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi mienendo ya Polisi dhidi ya Vyama vyta Siasa na Siasa ya Vyama Vingi wanafanya Taifa hili linakuwa mahali pabaya sana. Sasa kwa bahati mbaya mnafikiri wanawasaidia ninyi lakini tunajenga *character* ambayo hata kama nyie; mnaweza msiwe nyie; keshokutwa Mheshimiwa Lukvi anaweza asiwe Waziri akawa mtu mwengine, lakini wa CCM vilevile, mtashinda nyie, lakini mkawa mmejenga Polisi wenye *character* ambao wanakuwa na *affiliation* na siasa, mtalikata hili Taifa vipande. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri, ni ngumu lakini Polisi mwenye weledi anaweza akakataa maagizo yanayoharibu hadhi yake na Jeshi la Polisi. Leo Jeshi la Polisi linavyotumika, kama jana tu mfano; anakuja kuzuia mukutano. Tunawaambia huu mukutano una watu nane...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado dakika kama tatu hivi. Tunawaambia bado watu nane, tunamwambia simamieni hapa hizo *standard mnazokata*, Mwenyekiti anakuja kuongea mwenyewe, anasema hakuna, tokeni, la sivyo tukunje viti; watu nane. Sasa unashangaa Polisi anazuia Mkutano wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Waandishi wa Habari wa watu nane...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa. Taarifa huku, Dkt. Mollel huku.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema muda wako umekwisha, nilikuwa nimekupa muda wa nyongeza, sasa simwoni mwenye taarifa sijui yupo Msekwa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Niko huku.

**NAIBU SPIKA:** Aah pole. Hata hivyo muda wake umekwisha. (*Makofi*)

Haya, tunaendelea, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha halafu Mheshimiwa Masoud ajiandae.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe kwa nafasi hii, lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa muda huu nami nichangie kwenye hoja iliyopo mbele yetu kuhusu bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza niunge mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kwa juhudini ambazo zinafanyika na maelekezo thabiti wakati huu ambapo Taifa letu na dunia kwa ujumla tunapitia kipindi kigumu sana. Kimsingi ukiangalia utabiri wa *WHO* ni kwamba kufikia mwezi huu mwishoni tutakuwa na wagonjwa malaki, lakini kwa usimamizi wa Serikali thabiti na maelekezo mahususi ambayo yanatolewa kwetu wananchi, mpaka leo tunaona kwamba maambukizi yapo chini. Natoa rai kwa wananchi waendelee kujikinga

na kufuata maelekezo ya Serikali ili tuendelee kupigana na hii *Corona*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe machungu yangu, ukigusa imani moyo wangu unasononeka mno. Muda siyo mrefu uliopita hapa, viongozi wa dini wamedharaaulika hapa, wamevuliwa nguo kiimani. Neno la Mungu kama sikosei Wakorintho wa Kwanza, Sura ya kwanza, mstari wa 25 unasema: "maana kinachoonekana kuwa ni upumbavu kwa Mungu kina busara kuliko hekima ya kibinadamu na kinachoonekana kuwa ni dhaifu kwa Mungu kina nguvu kuliko nguvu za kibinadamu." (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kuwapa moyo viongozi wa kidini; dini zote ambao jana walikusanyika kwa ajili ya kuombea Taifa letu, kwamba leo hii Mheshimiwa Lema anaona walichofanya ni upumbavu lakini kwa Mungu kina busara kubwa sana. Anaona kwamba walichokifanya ni dhaifu lakini kwa Mungu kina nguvu kubwa sana na Mungu anasikia maombi waliyofanya. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kwamba mwaka 2019 kwenye Bunge liliopita ilikuja hapa hoja ya Mbunge aliyeichana hotuba ya Upinzani. Wakati ule illichanwa, lakini sasa hivi haisomwi kabisa. Maana yake ni nini? Ni kwamba lazima kuna Wizara Vivuli zianze kujitathmini, ziangalie hasa Wizara hii Kivuli ya Mambo ya Ndani ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Lema, kila mwaka ikija hapa ni aidha uondoe mambo mengi ndani yake au isisomwe kabisa. Yaani yeye anajiona ndiyo bora kuliko Mawaziri Vivuli wote wa Upinzani, jambo ambalo siyo sahihi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kwenye Wizara Kivuli ya Madini alisifia sana ame-flow vizuri akaenda vizuri, lakini huyu ambaye anajiita ni Mtumishi wa Mungu, anajiita Nabii, Wizara yake kila siku na kila mwaka imejaa chuki, vurugu na uvunjifu wa amani ya Taifa na pia imelenga kugawanya Taifa. Nabii gani huyu?

**MBUNGE FULANI:** Nabii Tito.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Au ndiyo wale manabii ambao wansemwa siku za mwisho watakuja manabii wa uongo! Neno la Mungu linasema siyo kila alitajaye jina la Mungu ataurithi Ufalme wa Mbingu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tuwe na heshima kidogo na majina. Haya majina ya Nabii na Wachungaji ni majina ambayo yana heshima kubwa sana kwenye jamii zetu, sasa huyu Nabii gani? Labda Nabii Kibwetere au Nabii Tito.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, niachane na hayo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vuma kuna taarifa. Mheshimiwa Lema.

## TAARIFA

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mchangiaji amesema neno la Mungu ambalo alikuwa anajaribu ku-refer michango yangu, nami naomba nisome Mithali 29:20: Je, umemwona mtu mwenye kuhamaki katika maneno? Afadhali kumtumaini mpumbavu kuliko yeye." (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vuma.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kuhusu...

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vuma kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Mollel.

## **TAARIFA**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka tu nimwambie ndugu yangu Mheshimiwa Vuma aendelee na mchango wake *kwa sababu katika route za kijambazi ambazo wizara hii imesimamia kwa miaka hii, mojawapo wa wamiliki wa route hizo ni huyu sasa; na laana ya mambo yaliyotokea huko nyuma ndiyo yanamsumbu na ndio maana amekuwa mtu wa ajabu, anaongea mambo kama aliyechanganyikiwa bila kuelewa.* **[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema kanuni iliyovunjwa.

## **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** 64(1) (f) na (g).

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoa taarifa, Mheshimiwa Mollel ameongea maneno magumu sana na siyo mara ya kwanza anasema kwamba mimi ni jambazi. Ni *very serious accusation*; lakini toka nimezaliwa sijawahi kushitakiwa hata kwa kuiba kijiko isipokuwa kwa kutoa watu kwa shetani kuleta kwa Mungu. Sasa amesema uongo, naomba afute kauli yake ama alete ushahidi wa Kituo cha Polisi mahali popote duniani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Vuma alikuwa akitoa mchango wake hapo na Mheshimiwa Dkt. Mollel akataka kumpa taarifa na kwa mujibu wa kanuni zetu hilo linaruhusiwa, lakini Mheshimiwa Lema wakati taarifa hiyo ikitolewa amesimama akisema Kanuni ya 64(1(f) na (g) inavunjwa na Mheshimiwa Mollel aliyekuwa akitoa taarifa.

Kwa yale aliyoyaeleza Mheshimiwa Dkt. Mollel sikusudii kuyarudia na Mheshimiwa Lema amesimama hapa akiyakana hayo ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Dkt. Mollel kuhusiana na Mheshimiwa Lema. Mheshimiwa Lema

katika kuyakana hayo yaliyozungumzwa, ameashiria kwamba huyu Mheshimiwa Dkt. Mollel aidha afute kauli yake ama alete uthibitisho.

Sasa kwa mujibu wa Kanuni zetu na kwa kuwa taarifa hii Mheshimiwa Lema ameikataa kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 63 kwa maana ya kwamba kama anaikataa maana yake Kanuni ya 63 inasema aliyezungumza maana yake ndio atakuwa alikuwa akitesha uongo. Najaribu kuyaunganisha yote mawili kwa sababu yeye ameshakana na akasema aidha afute kauli yake ama athibitishe.

Sasa Kanuni ya 63 inatupa mwongozo wa namna ya kwenda nalo jambo hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa ajili ya muda Kiti kabla hakijatoa uamuzi wake unashauriwa kama alivyosema Mheshimiwa Lema kwa mujibu wa Kanuni hii ya 63, aidha ufute kauli yako ama nitatoa maelezo mengine.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema ni mtandano na ukweli nina uwezo wa kuuonesha, lakini kwa sababu ya muda, nafuta kauli, lakini Mheshimiwa Lema nina uwezo wa kuunesha hicho unachokisema.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mollel ukishafuta kauli, yote unayoyasema yamefutwa. Kwa hiyo, hakuna kitakachoingia kwenye taarifa Rasmi za Bunge. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Lema alikuwa ameomba ili nitoe utaratibu kwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Mollel ameshafuta hiyo kauli yake, Mheshimiwa Vuma ataendelea na mchango wake.

Mheshimiwa Augustine Holle Vuma.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa unyenyekevu mkubwa sana, unilindie muda wangu. Nije kwenye upande wa Idara ya Uhamiaji. Uhamiaji kwa kweli wapo maafisa ambao ni wazuri sana lakini wapo ambao ni changamoto kama ilivyo kawaida kwenye sehemu

nyingine, hasa maeneo ambayo ni ya mpakani kwa sababu kuna mwingiliano mkubwa. Kwa hiyo, hapo ndipo ambapo wale Maafisa ambaio sio waaminifu wanaonesha makucha yao. Mpaka unaona kila Mbunge wa mpakani akiamka anasema, umekuwa ni mwiba mkali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba tu nitoe ushauri, kaka yangu Mheshimiwa Waziri Simbachawene pamoja na Kamishna wa Uhamiaji, mpange utaratibu wa kuwa mnaenda kutembelea Wilaya ambazo zipo kwenye mipaka. Ukienda kule waite tu. Nenda wilayani, njoo Kasulu pale, ita Wenyeviti wa Vijiji wote waje pale. Awepo Kamishna wa Uhamiaji pale, Viongozi wa Uhamiaji ngazi ya Mkoa na Wilaya halafu wale viongozi wa vijiji wakuletee ma-file ya uonevu ambayo wanafanyiwa na Maafisa wa Uhamiaji ambaio sio waaminifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nendeni Kigoma, Kagera na maeneo mengine ambapo kuna shida hii. Ukifanya hivyo itakusaidia sana kwa sababu hawa kwanza, unapanga ratiba. *For instance unaenda annually labda mwezi wa Saba, kwa hiyo, wanapokuwa wakifanya upuuzi wao wanajua kwamba Waziri na Kamshna wa Uhamiaji watakuja, hawa watakuja kutusema mbele yao, itasaidia sana.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, napenda kuishukuru sana Wizara hii ya Mambo ya Ndani hasa Kitengo cha Wakimbizi kwa uratibu ambaio wanafanya kuratibu mashirika haya yanayohudumia wakimbizi kwenye makambi ya wakimbizi. Ukweli ni kwamba zamani zilikuwa zinakuja pesa nyingi sana kutoka nje ambazo zilikuwa zinapigwa zinaishia kwenye mifuko ya watu, lakini sasa hivi tumeona kuna mabadiliko makubwa sana. Leo hii kuna miradi mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sisi Kigoma tuna mradi unaitwa *Kigoma Joint Programme*, zaidi ya dola milioni 55, ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni 100. Sasa hivi ukienda kuna miradi inaendelea ya maji, barabara, shule na maghala ya vyakula. Kwa hiyo, wananchi sasa wanapewa kama ahsante kwamba mmekaa na wakimbizi kwa muda mrefu,

mmepeata madhara mbalimbali, hamjalipwa lakini hii tunawapa kama ahsante, shukurani ya Mashirika haya ya Umoja wa Mataifa kwa ajili ya kukaa na wakimbizi. *Very good, hongera sana Wizara ya Mambo ya Ndani.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili niongezee kitu kimoja kwamba tujitahidi kuhamasisha au kuwapa nguvu mashirika ambayo ni ya kwetu Tanzania. Zipo faida; Mashirika kama *Red Cross*, napongeza Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushughulikia kuendelea kuwepo kwa *Red Cross* kwenye makambi ya wakimbizi, maana kulikuwepo na mizongwe kidogo wakataka kuondolewa, lakini nashukuru Wizara ilisimama imara na hatimaye *Red Cross* wakaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo faida za kuwa na mashirika haya ya kibinadamu kwenye makambi ya wakimbizi ambayo ni ya Kitanzania, ya kizalendo. Kwanza, mashirika haya ya Kitanzania huwa yanaajiri Watanzania kwa asilimia kubwa. Haya mashirika ya nje huwa yanakuja na wafanyakazi wao kutoka nje huko huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba huwa unafanya mtaji mkubwa, yaani fedha nydingi ambazo zinatoka nje kuja kuhudumia wakimbizi zibaki hapa hapa, kwa sababu mishahara yao hao watumishi inabaki hapa hapa lakini na mambo mengine; *purchase* na vitu vingine wanafanya hapa hapa, ukilinganisha na mashirika ambayo kwao siyo Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja la msingi sana nisisitize, Mheshimiwa Simbachawene ajitahidi sana. Moja ya *legacy* ambayo ataiacha na tutamkumbuka Mkoa wa Kigoma ni kuhakikisha makambi ya wakimbizi yanalishwa na chakula ambacho kinalimwa kutoka kwenye Mkoa wa Kigoma. Kwa nini mkimbizi yupo Nyarubusu ale chakula kutoka Kenya? Yupo Kasulu pale ale chakula kutoka Zambia! Inauma sana. Hawa watu tunawapokea kwa moyo wote; moyo mmoja kabisa, lakini kwa nini wasile chakula? Kwa nini

isiwe soko kwetu sisi kwamba wale chakula ambacho tunalima sisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri sisi Mkoa wa Kigoma hatujawahi kuwa na upungufu wa chakula tangu nchi hii ipate uhuru, tuna chakula cha kutosha. Kwa hiyo, kuna nafasi ya sisi wanatupiga *starter* tu, ooh unajua hiki chakula chenu hakina hadhi; hivi kweli chakula ambacho tunakula, unaona Vuma ana mwili na nguvu hivi unasema hakina hadhi ya kula mkimbizi, kweli! (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vuma.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Aah! Ahsante sana, naunga mkono hoja tena. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha, ahsante sana.

Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud na Mheshimiwa Livingstone Lusinde aijandae.

**MHE. CHACHA R. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru na nimpe pole sana Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Simbachawene kwa kufiwa na baba yake, pole sana. Niwashukuru Wizara nzima kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia kwa kunukuu kifungu cha Biblia kama wengine walivyonkuu; Mithali 29:14 inasema: *"Mfalme awahukumuye maskini kwa uaminifu, kitu chake cha enzi kitathibitika milele. Mfalme awahukumuye masikini kwa uaminifu kitu chake cha enzi kitathibitika milele."* sasa mimi nisiweke pale Mfalme niseme Rais awahukumuye maskini kwa uaminifu kitu chake cha enzi kitathibitika milele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa hotuba yake ya jana aliyoitoa imetoa mwelekeo imeondoa hofu ambayo imejazwa ndani ya mioyo ya Tanzania wengi. Watu kila kona wanaogopa *corona*, yaani watu wanaogopa kila kona kwa sababu ya akina Lema. Mimi niwaulize ni magonjwa mangapi yanaua kuzidi *corona*, leo *corona* tangu ianze Tanzania.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa kuna taarifa Mheshimiwa Godbless Lema

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Hata Rais mwenyewe anayemtaja jana ame-*confess* kwamba hii *pandemic* ni *serious*, kazi yake ya kutoa matumaini kwa watu ndiyo wajibu wa Rais kutoa matumaini Rais haweziku-*confess weakness* kwenye *public*, *he is a President* kwa hiyo hata kama anaona tatizo hizo ndiyo *statement* za Rais, lakini Mheshimiwa magonjwa mengi yanaua, hii ni *pandemic* na humu ndani tayari kuna wagonjwa, inaweza ikala Bunge zima hili umesikia kwa hiyo Mheshimiwa Rais ..

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema nadhani yule unayempa taarifa ameshaelewa na nitamuuliza kikanuni, lakini kimsingi yaani unajua wewe unasoma sana Biblia na Biblia inatufundisha kujuzuia. Mheshimiwa Lema unavyoizungumzia *corona* unatishia kila mtu, hata hapa unasema tutakwisha humu ndani, sisi tunaoamini katika yanayoendelea hatutakwisha nawe, yaani utakwisha mwenyewe kwa ukiri wako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha unapokea taarifa ya Mheshimiwa Lema?

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sipokei kwa sababu roho ya hofu ni roho ya shetani na ukiona

mtu anataka kuogopesha watu, shetani ndiyo kazi yake hiyo. Kwa hiyo mimi nikisikiaga Nabii...

**MHE. JOHN W. HECHE:** kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni iliyovunjwa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Kanuni ya 63.3 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 64(a): "*Mbunge hatatoa Bungeni neno la uongo.*" Corona siyo Lema anayesababisha inatisha watu ni dunia nzima ukifungulia *TV* zote

**NAIBU SPIKA:** Sasa uongo wake hapo uko wapi?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Ndiyo naenda kwenye hoja yangu

**NAIBU SPIKA:** Siwezi kukupa muda kana kwamba unachangia, niongoze vizuri ili niweze kutoa maelezo, wewe si umeomba utaratibu...

Yule amesema Mheshimiwa ana....

Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Heche, siyo wewe peke yako kila mtu anaona, kila mtu anasikia na hayo maneno nimeyazungumza mimi hapa. Tuelewane vizuri, kwa hiyo unapoomba utaratibu unataka mimi nitoe utaratibu, siyo mtu mwingine. Ukipungumza habari za kutisha, wewe mwenyewe umesikia hapo akisema, sasa tukishatishwa humu ndani tukimbia kazi ama? Mheshimiwa Heche, tafadhalii. Mheshimiwa Marwa

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie tu muda maana hata sjafanya chochote. Nilikuwa nasema ukiangalia Tanzania labda na nchi zingine si kwamba *corona* ndiyo ugonjwa pekee unaoua. Leo kwa nchi yetu pekee ukiangalia *malaria* ukapata takwimu kwa siku *malaria* inaongoza kwa kuua. Ukiangalia wanaokufa kwa kansa, wanaokufa kwa kisukari, wanaokufa kwa presha, ni wengi, wanaokufa kwa ajali ni wengi. Naomba nimshukuru

sana Mheshimiwa Rais, amewapa *confidence* Watanzania na ndivyo ilivyo kwa Rais wa nchi, Mfalme yeoyote lazima uwape *confidence* watu wako, lazima uwajengee imani, imani ni kuwa na uhakika huwezi kushinda vita kama huna imani, unaanza...

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako unatunzwa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Nicolaus Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *would you respect* sisi ni Wabunge tunajua kabisa kuhusu hii *pandemic* tukikaa hizi hotuba zetu baadaye zinaenda kwa raia. Mkisema *corona* haitishi ni kwa nini mmefunga shule? Mkisema *corona* haitishi ni kwa nini viongozi wa dini jana wallikuwa wanaliombea Taifa pale Karimjee? Mkisema *corona* haitishi kwanini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameomba *World Bank* wasamehe madeni kwa sababu watu wanataka wa-deal na *pandemic*. Ni kwa nini tumeona Waziri Mkuu akipokea *billions of money* kwa ajili ya ku-deal na *pandemic*, kwa hiyo tusipotoshe. Kwa nini mnavaa mabarako, mnajiweka na ma-sanitizer hapa ndani, *why do you then fumigate this area* kama haitishi, tusiongee uongo kwa raia wanachukua tunayoongea...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko umeomba taarifa, narudia tena, mtu yule ambaye hofu yake inamkimbiza asingekuwa hapa ndani saa hizi. Ambaye ana hofu kiasi hicho asingekuwa hapa ndani sasa. Ugonjwa upo, ugonjwa ni mkubwa, ugonjwa unaua, kila mtu achukue tahadhari, hakuna mtu anaambiwa sasa akae tu hovyo, hapana, kila mtu achukue tahadhari, kila mtu, hamna mtu mwagine wa kumchukulia tahadhari mtu mwagine. Kwa maana hiyo hiyo tusitishane, lakini tujihadhari, wala hakuna unabii kwenye jambo hili limeshatokea, hakuna nabii anazungumza jambo ambalo limeshatokea. Kwa hiyo mtu asitake kuonesha kana kwamba kuna jambo la ziada litatokea, hapana, limeshatokea na lipo na linaendelea. Mheshimiwa Marwa Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unajua ngoja niwaambie, mimi nilikuwa upande ule, hawana hoja saa hizi, hoja iliyobaki ni *corona*, watapiga *corona* mpaka fainali Bunge linavunjwa, hamna *issue*. Wanataka *lockdown* hivi tuulizane sisi hapa; wananchi wetu, mama ntilie wale wanaoenda kufanya vibarua ndo wapate mlo wa siku, tufanye *lockdown*, hiyo ndiyo mnataka nyie upinzani, mimi nikwambie kila nchi ina *model* yake, *model* tulioamua, *model*/ambayo Rais wetu ameamua kuichukua twende nayo ni nzuri, nani asiyeona Marekani wanavyoandamana, nani asiyeona Kenya wanavyoandamana? Nani asiyeona Afrika Kusini, ukawafungie watu wanakula nini? Wanaishije?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ile *ruling* aliyoitoa ndiyo inapaswa, ndiyo tunapaswa kuiendea kwa kulingana na hali halisi ya uchumi wa nchi yetu. Hawa wanataka tufeli, hawa wanataka nchi ikose mapato, tusiendelee, *that is what you need* Lema hakuna kingine, ili mwisho mseme Dkt. Magufuli amefeli, hakuna nini, tulia *brother* hamna.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu ngoja nikwambie kitu, kuna mtu amesema jambazi, jambazi siyo lazima ushike bunduki, hata ukiwakataa viongozi wa dini waliokuwa wanaomba jana wewe jambazi. Majambazi wa kiroho wapo, leo unaweza ukasimama ukapuuza viongozi wetu wa dini, wamesimama kuomba, leo unapinga...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa hebu tuiondoe hiyo habari ya ujambazi.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeondoa, naomba niendelee

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa msemaji ni kweli kabisa kwamba viongozi wa dini wasidharauliwe kwa hayo wanayoyafanya au wanayoutuombea. Hata hivyo, tumesema hapa kwamba kuna viongozi wa dini wako miaka nane sasa hivi wako gerezani. Sasa je, tunaposema kwamba viongozi wa dini dua zao hazikubaliki na tunaposema kwamba viongozi wa dini wako magerezani hawajatolewa, wanawadhalilisha viongozi wa dini ni nani, kati ya sisi tunaosema na ninyi mlioweka ndani nani anadhalilisha viongozi wa dini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bwege umeshasikika Mheshimiwa

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Kuna watu miaka nane kuna mashehe...

**NAIBU SPIKA:** Umeshasikika Mheshimiwa, umeshasikika Mheshimiwa Bungara. Mheshimiwa Marwa endelea na mchango wako.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Rais Dkt. Magufuli, mimi ngoja nikwambie leo, si nilikuwa kule, pale Kibiti wakati watu wa CCM wanaauawa, Polisi wanaauawa, mimi nilikuwa kule tulikuwa tunafurahi kweli, unabisha? Tulikuwa tunafurahi. Sasa nimshukuru Mheshimiwa Rais na nivishukuru vyombo vyaya ulinzi na usalama kufanya kazi yake, viachiwe vyombo vyaya ulinzi na usalama vifanye kazi yake.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha, kengele ya pili imeshagonga.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud atafatiwa na Mheshimiwa Masoud naomba ukae. Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru katika muda mfupi uliopita wakati mchango wa Mheshimiwa Lema unatolewa hapo Bungeni kwako Mheshimiwa Lema alisema Kamati ya Bajeti imetoa taarifa juu ya mambo ya utalii na nini kuathirika kwake kwa sababu ya *corona*. Sasa mimi ni Mwenyezeki wa Kamati sijatoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu, juu ya athari za *corona* katika uchumi wa nchi yetu. Sasa naomba Mwongozo wako jambo hilo linaposemwa wakati hakuna taarifa yoyote na sisi hatujaleta taarifa yoyote mbele zako kama jambo hilo linaruhusiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimeombwa Mwongozo nitautolea maelezo baada ya kumaliza hili zoezi la leo. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salum atachangia, halafu tutamalizia na Mheshimiwa Livingston Lusinde na Mheshimiwa Masauni ajiandae.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala*. Leo ni mwezi 29 Shaaban, matarajio kesho kama mwezi utaandama itakuwa ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo Mashekhe wetu wa Kiislamu uamsho bado wako ndani kwa muda wa miaka nane sasa. Hawa ni viongozi wa dini Serikali ikae iamini na ikubali kwamba mwaka jana wakati tunatoa maelezo haya ya kuwatetea Mashekhe hawa wa Kiislamu wa uamsho aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati huo Mheshimiwa Kabudi alisema tunasubiri *email/kutoka* nje, huu ni mwaka mmoja sasa, *email/haijafika*, hatujui hatma ya viongozi hawa wa dini. Nawaombeni sana Serikali mtuelewe, mwaka 2001 kule Zanzibar tulisema tutafanya maandalaman, tukaambiwa hamtafanya maandalaman, mkiandalama mtapigwa na tulikubali kufa na wako walikufa. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, haya mambo ya hisia za kidini, nawaomba sana Serikali, hili jambo walichukue *serious* na lishughulikie kwa makini sana. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni suala zima la viashiria vya uvunjifu wa amani. Nimwambie jambo moja kubwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba, huu ni mwaka wa uchaguzi, iwapo Mwenyezi Mungu akijaalia kama *corona* ikipungua ninachosema kuna viashiria vya uvunjifu wa amani. Kwanza Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa na kawaida haitaki kupokea fomu za Wapinzani, hivyo ni viashiria vibaya vya uvunjifu wa amani. Imekuwa ni kawaida, hawapokei fomu zetu za upinzani ina maana kwamba hapa watu hawatokubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, vyombo kama hivi avielekeze ili tujue mapema. Hata hivyo, kubwa kuliko yote, kuna baadhi ya viongozi hawaguswi hata wakitoa kauli. Gazeti la Habari Leo tarehe 7 Machi, 2020 anasema wanaotaka CCM isitumie dola watasubiri sana, nafuu ya mwenye madaraka ni kutumia dola kubaki madarakani. Chama cha *KANU* kiliposhindwa kutumia dola hakikurudi madarakani. Huyo ni Katibu Mkuu wa CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba, wengine wakitoa matamko wanaitwa, wanahojiwa, wanaambiwa nyie ni wachochezi. Viongozi wa Upinzani wanapotoa maelezo yoyote wanaambiwa nyie ni wachochezi, Viongozi wangapi wa Upinzani wameambiwa ninyi ni wachochezi mnatakiwa kuhojiwa, mnaenda mahakamani lakini viongozi kama hawa wa chama dola hawahojiwi. Hii ni mbaya, mimi ni muumini wa ulinzi na usalama. Mambo kama haya si mambo mazuri hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea, kiashirio kingine ambacho kidogo nakiona kina tatizo ni mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, kama Mwenyezi Mungu akijaalia lakini niseme kwamba kumekuwa na tatizo la kuwekewa pingamizi na Tume ya Uchaguzi, baadaye ikaonekana kwamba hiyo pingamizi imefuata mkondo wake. Pingamizi ambazo hazina kichwa wala miguu zinahatarisha amani na utulivu na hasa hasa kwa Vyama vya Upinzani, watu wamekuwa

wakiwekewa pingamizi ambazo hazina kichwa wala miguu. Baadaye inakuwa ni vurugu, matokeo yake mtapiga watu, mtaua watu. Naomba niwaambie Tume ya Uchaguzi mara hii ina kazi kubwa, ichukue nafasi yake tuone kwamba tunakwendaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *corona*, jamani niwaambie jambo dogo, tarehe Mosi Aprili, 2020, Serikali ilitangaza wagonjwa 20; tarehe 6 Aprili, wakatangaza 24, tofauti ya wanen; tarehe 10 Aprili, wagonjwa 32, wakaongezeka nane; tarehe 14 Aprili wagonjwa 53; tarehe 15 Aprili wagonjwa 83; tarehe 16 Aprili wagonjwa 94; tarehe 17 Aprili, wagonjwa 147; tarehe 19 Aprili wagonjwa 170; tarehe 20 Aprili wagonjwa 254; tarehe 21 na 22 wagonjwa 284, hivi ni nani jamani ataona suala hili ni jepesi jepesi tu? Tanzania nawaambieni tunaelekea kubaya kwenye *corona*, ni lazima tuwe na mkakati wa ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru umesema tuchukue tahadhari, nami naungana na wewe kabisa tuchukue tahadhari ya ziada vinginevyo hili gonjwa Tanzania itashinda Kenya, hivi ni viashiria vibaya sana. *Corona* hivi sasa kila ukienda mitaani huko baadhi ya mikoa inasema kwamba mgonjwa akitoka Dar es Salaam akifika mkoaa mwingine anaambiwa hapana, wewe usikanyage utabakia karantini. Nimesikia Mkuu wa Mkoa wa Rukwa jana akitangaza, sasa nawaambia Serikali, suala la *corona*, tuna Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, fedha zipo za kutosha, tuna fedha za kigeni za kutosha, wananchi ni wanyonge, tusiwaache wao wenywewe peke yao wanapambana na *corona*, Serikali iweke mkono wake sasa wakati ndiyo huu kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kwenye fedha za kigeni, huu ndiyo wakati wake sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana kwa Mheshimiwa Jenista, hii ni kazi, wakati huu ni wakati mgumu kweli kweli, ukienda mitaani huko ni shughuli. Leo naambiwa taarifa kwamba kwenye Hospitali ya Amana kuna wagonjwa wametoroka, kwenye mitandao imetolewa hiyo na

naambiwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mheshimiwa Sophia amethibitisha, wamekwenda wapi? Wamekwenda mitaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini suala la *corona* lisifanyiwe mzaha. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, ulimtaja mtu wa mwisho ukasema Lusinde atakuwa mtu wa mwisho, lakini wakati umesema hotuba yetu haitasomwa ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ulitoa maelezo kwamba tuandae mtu ambaye attachangia zile dakika zetu za ambazo umetupa mwenyewe na kiti kimetupa. Sasa tulikuwa tumeshamuandaa Heche na tumekupa taarifa hapa kwamba Mheshimiwa Heche ndiye atakayechangia. Sasa tunaomba kama kuna uwezekano Mheshimiwa Heche aweze kuchangia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ili taarifa zikae vizuri uwiano wa wachangiaji saba ilikuwa CCM, mmoja CHADEMA, *CUF* mmoja; mtagundua hapa ameshachangia Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Esther Matiko nilikuwa nimemwita na upande wa *CUF* pia nimewapa muda wangu, mnaona ni Wabunge wawili waliochangia. Kwa hiyo hakuna mtu yejote ambaye ameibiwa hapo muda wake.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, naomba ukae. Mheshimiwa Waziri Dkt. Kigwangalla ulikuwa umesimama na nilikuwa sijakuona.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi kwenye Serikali ni *Care Taker Minister* wa Afya, bahati mbaya sijawaona wenzangu hapa lakini nimeona upotoshaji ukiendelea kuhusu janga la *Corona* na

nikasema siwezi kukaa hapa naendelea kushuhudia upotoshaji ukiendelea bila kutoa taarifa kwa umma.

**NAIBU SPIKA:** Sawa basi Mheshimiwa Waziri kama ni hivyo nitakupa nafasi ya kuchangia.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Sawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nipate tu mwongozo wako kuhusu msemaji aliyeppita pale ambapo kunakuwa aidha ni bahati mbaya ama kwa makusudi, tunapochanganya tafsiri ya maneno. Kamnukuu Katibu Mkuu wa CCM akisema kutumia dola, tafsiri ya neno dola au neno dola limetoholewa kutokana na neno la kiarabu *alduwlar* na tafsiri na sifa ya neno hili ni mambo matatu. Dola kwa mujibu wa lugha kiarabu ambapo neno *alduwlar* limetoholewa, ndiyo tunalotumia sisi katika Kiswahili, ni nchi, taifa, ni utaratibu wa kisiasa wa jamii katika fulani. Sifa ya dola ni mambo matatu; eneo, taifa na mamlaka ya watu, hizi ndio sifa za dola. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa msemaji anatafisiri neno dola kama vyombo nya dola. Katibu Mkuu wa CCM hajasema kutumia vyombo nya dola, kasema kutumia dola na dola ina sifa tatu. Kwa hiyo, nilitaka mwongozo wako ama kama Mheshimiwa Mbunge atasema kwamba alikuwa anamaanisha kwamba Katibu Mkuu alisema natumia dola ambayo sifa yake ni watu na taifa na ndiyo chama cha siasa au mfumo wa jamii ya kuishi. Kwa hiyo, CCM inatumia watu, taifa na inatumia mfumo wa jamii hiyo katika kuishi ili kuendelea kutawala. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Mwongozo huu pia nitautolea maelezo mwisho wa siku yetu ya leo. Mheshimiwa Livingstone Lusinde atafuatiwa na Mheshimiwa Masauni mtoa hoja ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mungu sana kunipa wasaa huu wa kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa namna ya kipekee, nikushukuru wewe mwenyewe Naibu Spika, Masoud acha gazeti kwanza jitulize, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kusema maneno machache. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe pole Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kaka yangu Mheshimiwa Boniface kwa kufiwa na baba yake mzazi mzee Boniface Simbachawene Mwatanguluyala, kwa majina yake matatu namtaja hapa. Vilevile nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge ambaye Mwenyenzi Mungu amemwita mbele ya haki. Mwenyenzi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana Watendaji Wakuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Waziri, Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Masauni, Katibu Mkuu pamoja na makamanda wa vyombo vyya ulinzi wa na usalama waliopo katika Wizara hii, Kamishna Dkt. Anna P. Makakala, amedhihirisha kwamba wanawake wanaweza. Aidha, nimpongeza AGP Simon Sirro kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za Jeshi la Polisi ni tofauti na kazi za hoteli. Kazi za hoteli zinafahamika, kusubiri wateja na mambo mengine lakini Jeshi la Polisi kwa nafasi yake kubwa linafanya kazi za operesheni. Kwa hiyo, naomba Serikali iwapatie vitendea kazi vyta kisasa zaidi Jeshi la Polisi ili kazi zao za operesheni ziwe nyepesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Jeshi la Polisi linahitaji kamera katika majiji yote makubwa, zifungwe kwenye *center zote*. Si lazima wawe wanatafuta mwizi kwa njia hii wanayotumia, kamera zinaweza kuwasaidia kupiga picha wakati wao hawapo na baadaye waki-*trace* wanaona kumbe kuna tukio limetokea sehemu fulani sisi

hatukuliona. Hiyo itawarahisishia sana Jeshi la Polisi katika mambo ya uchunguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia Jiji la Dodoma linavyokua kwa kasi, tumpongeze sana Kamanda wa Polisi wa Mkoa Dodoma Muroto anafanya kazi nzuri sana. Muroto anatakiwa aongezewe magari, *OCD* wa mjini hapa hana gari, Wilaya ya Chamwino ambapo anatoka Rais mtupatatie walau pikipiki kila tarafa ili wale polisi wa kitarafa waweze kupata muunganiko wa haraka pale yanapotekea matukio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuomba gari ya doria barabara ya Iringa – Dodoma, Wabunge wengi wanapita njia hiyo lakini hakuna kituo kikubwa cha Polis wala gari la polisi. Ajali nyingi zikitokea polisi wanapanda lori mpaka aje kufika saa ngapi, anakuta pale kama mtu amepoteza maisha yake kwa sababu ya kukaa muda mrefu sana na hii kweli haileti picha nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli maneno mengi sana yamezungumza, wengi sana wamempongeza Mheshimiwa Rais na mimi nampongeza kwa hotuba yake nzuri lakini kwa msimamo alioutoa kwa taifa hilli. Taifa la Tanzania haliwezi kufungia wananchi wake Mheshimiwa Rais amesema. Hii imedhihirisha kwamba kweli Rais wanyonge wa nchi hii anawajua. Kuna watu ukiwafungia saa mbili tu hawafi tena kwa *Corona* bali wanaanza kufa kwa njaa. Nchi yetu ina watafutaji wengi ambao wanatoka asubuhi kwenda kutafuta maisha akirudi ndiyo watoto wanakula. *Big-upsana* Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Rais nashauri Jeshi la Polisi liimarishwe kwa kupewa vitendea kazi. Mimi mara zote nasema ukitaka polisi wafanye kazi vizuri wewe fuata sheria, tii sheria bila shuruti utaona polisi wanafanya kazi yao sawasawa. Kuna maneno mengi yamesemwa sana asubuhi ya leo na wazungumzaji waliochangia lakini namuona Mheshimiwa Lema ameondoka nilitaka nimsaidie kidogo, huwezi kuelewa nini

wanataka. Mheshimiwa Lema amezungumza maneno mazuri sana kwamba roho ya mtu mmoja, namnukuu hapa vizuri na wao wenyewe wapo, roho ya mtu mmoja haiwezi kufanishwa na fedha, amesema Lema hapa halafu anawalaumu polisi kwa kutawanya watu nane wa CHADEMA. Sasa roho nane polisi kwenda kuziokoa dhidi ya *Corona* ni kosa? Unaweza kuona hauwezi kuelewa hawa watu wanataka kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema roho moja ni ya muhimu sana kuliko fedha lakini anawalaumu jeshi la polisi jana kuwatawanya walipokuwa kwenye hatari ya kupata *Corona*. Sasa unaweza usielewe wanachotaka ni kitu gani? Kwa sababu pale walipokuwepo ofisi ni ndogo, haina hewa ya kutosha, hawakuwa kwenye eneo la Bunge, walikuwa wapo uchochoroni huko ndani ndani, nitakupeleka siku moja, unapita kwa mama mmoja anauza vitumbua ndiyo kuna ofisi yenyewe hiyo. Kweli Kiongozi wa Upinzani apelekwe kule?

Mheshimiwa Naibu Spika, Polisi wakasema hapana, hapa mnaweza kupata maambukizi, kwanza kipimo kile cha kupimia kama kile cha mlangoni hakipo sasa wangepimwaje hao watu nane? Polisi wakasema hapana jamani, kwa hiyo, tunashauri eneo hili msifanyie kikao kwa sababu hali ya hewa yenyewe hairuhusu. Leo tena anakuja kuwalaumu polisi badala ya kuwashukuru polisi, kazi waliyoifanya jana polisi ndiyo ya ulinzi wa raia na mali zao. Pale walikuwa wanalinda raia, tusiwalaumi polisi katika kila hoja wakati mwininge tuwapongeze. Je, maambukizi yangepata roho nane Lema anasemaje sasa? Pale amesema roho moja ni ya muhimu lakini roho anataka nane zipotee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi CCM tumepewa dhamana ya kulinda roho za watu wote hatuangalii huyu mtu yupo chama gani? Siyo kazi yetu sisi. Nataka niwaambie ndugu zangu wa Upinzani mtego mnaotaka kuutega, fikira zenu mnafikiri mtanasa panya lakini nawahakikishia mtanasa nyoka. Hamtanasa panya kwa sababu huo mtego mnaoutega utawanasa wenyewe. Ndugu zangu sisi tumekuwa tukiongoza na siku zote Rais anasema maendeleo hayana chama, anasema ugonjwa huu hauna chama, kaka

yangu Simbachawene wewe katika Wizara yako pamoja na vyombo vyako simamieni haki.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba alipokuwa anachangia Lema pia aliwasemea maaskari wetu kwamba wakati waenda kuzuia *press* ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa walikuwa hawajavaa barakoa lakini pia walikuwa wamekaa kwenye gari polisi wengi kana kwamba tatizo lililopo sasa hivi hili la Corona ingekuwa ni rahisi sana wao kuweza kuambukizana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hata anapochangia ndugu yangu Lusinde akumbuke pia hilo Lema alilizungumzia. Kwa hiyo, hakuzungumzia *negative* tu kwa polisi pia alikuwa anazungumzia kwa maana ya kuwasaidia wanapoenda kukamata au kuzuia pia nao wajihadhari wavae barakoa na pia wasikae kwenye msongamano. Nilikuwa nampa taarifa tu ajaribu kukumbuka na hilo.

**NAIBU SPAKA:** Mheshimiwa Livingstone Lusinde, unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa ya Mbunge anayemaliza muda wake na kwa kweli anabidi kutumia Bunge hili kwa ajili ya kuaga, ni mionganini wa Wabunge ambao nawataka waage kwa sababu inawezekana uchaguzi utakapokuja hawatakuwemo, mmojawapo ni huyu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Wizara ya Mambo ya Ndani tumesema hapa kwamba ni kulinda watu na mali zao. Kwa hiyo, kazi yake ni kuhakikisha kwamba watu wote

wanakuwa salama bila kuangalia huyu mtu yupo chama gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi hapa wamezungumza kuhusu *NIDA*. Ni kweli kabisa Waheshimiwa Wabunge tumesema vizuri na kwa uchungu mkubwa kwamba *NIDA* kuna matatizo ya hapa na pale. *NIDA* wanapata wakati mgumu kwenye mikoa ya pembezoni kwa sababu vilevile hata ulaghai wa baadhi ya watu wa nchi za jirani kuomba vitambulisho vyetu nao upo, tusikatae Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi tumemuona Waziri wa Ardhi hapa Mheshimiwa Lukuvi anamuuliza mtu maswali anataka ardhi hawezি hata kujibu Balozi wake nani, anatoka wapi, mwisho wake akakamatwa pale kumbe siyo raia wa Tanzania. Kwa hiyo, lazima tukubali kwamba na sisi wenyewe tuwasaidie *NIDA* katika uchambuzi ili waweze kuwatekelezea haki zao Watanzania lakini na wageni nao waweze kuwabaini kwa sababu tuko Watanzania baadhi yetu na sisi tunatunza wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kilimo tunaona vibarua wanavushwa kutoka Burundi bila utaratibu wanakuja kulima matokeo yake wanahamia wanakuwa Watanzania na wanaomba vitambulisho vyya kupigia kura. Kwa hiyo, ingekuwa vyema mkakati wa pamoja uwekwe kati ya wanasiasa, viongozi wa Serikali ya Vijiji na Mitaa kuwabaini wageni wanaokuja kutuchafulia sifa inayochelewesha *NIDA* kufanya kazi yao kwa sababu tunawakamata wageni wengi sana.

Mimi sipendi Watanzania wanyanyasike eti kwa sababu ya maumbile au vitu vingine lakini tungependa Watanzania hao hao kwa kutumia mfumo wetu, sisi tuna mpaka nyumba kumi, kuwabaini wageni kwa urahisi, hii itasaidia sana watu wa *NIDA* kufanya kazi zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwingine amezaliwa mpakani ye ye Mtanzania ndugu yake yuko ng'ambo

anataka na ndugu yake wa ng'ambo apate kitambulisho na hiyo inatuchanganya vilevile. Lazima tuwe wazi kwamba jamani mimi ni Mtanzania, huyu ni ndugu yangu lakini yeye ni raia wa nchi nyininge, mbona hiyo ipo. Kwa hiyo, tusipokuwa wazi kusaidia Serikali katika kuwatambua wahamiaji haramu ambao wako pembezoni tutaifanya *NIDA* ifanye kazi kubwa sana katika kutoa *passport* na hivyo tutachelewa kupata vitambulisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo tunawaomba *NIDA* muongeze speed, mipakani mmesema kuna changamoto maalumu, hivi na katikati ya nchi nako kuna changamoto gani? Maana tunaangalia Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma bado kuna watu wanalia vitambulisho. Hapo sasa ndiyo tunaposema *NIDA* ongezeni speed, hizi namba peke yake mnazosema watu wanapewa, kama namba ipo kwa nini kitambulisho kisifuate namba? Maana watu wameshaandikishwa, namba tayari zinatoka, ukibonyeza kwenye mtando unapata namba, tabu iko wapi kupata kitambulisho? Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unajibu tunaomba utuambie hivi kwa nini namba mimi napata halafu kitambulisho sipati? Tukiweza kuupata majibu hayo yatatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kazi nzuri mnayofanya, tumeona ujambazi umepungua kwa kiwango kikubwa sana. Hata hivyo, tunaomba sana kwa Jiji la Dodoma ambako utapeli sasa umekuwa sehemu yake, unajua tumepata Jiji tumepata vitu vizuri lakini vilevile na uhalifu wa kimataifa nao umeongezeka Dodoma. Sasa hivi hata vioo vyaa magari vinavunjwa watu wanaiba pochi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba uwezo wa Jeshi letu la Polisi hasa katika vifaa uongezwe ili polisi wawe na vifaa vyaa kisasa. Polisi anapokwenda kwa mhalifu awe amesheheni. Siyo anaenda polisi anamwambia mhalifu toka, mhalifu anabisha, haiwezekani. Polisi akiwa amesheheni vifaa akimwambia mhalifu toka nje mwenyewe ananywea anatoka na anatii sheria bila shuruti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

## **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Ndugu Simbachawene na pia nimpe pole kwa kufiwa na baba yake mzazi, sote njia yetu ni moja, nimpongeze pia Naibu Waziri Ndugu Masauni, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi nijielekeze kwenye mchango.

Mheshiwa Naibu Spika, Wilaya ya Uvinza haina gari la *operations*, imepokea gari la kubeba mahabusu na vifaa, sote tunatambua Jimbo hili kijiografia ni kubwa na linapakanu na nchi za DRC na Burundi, uhalifu upo lakini pia matukio mbalimbali hadi tunavyoongea wana gari bovu walilopewa mkoani wakati Wilaya ikianzishwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu, tuletewe gari haraka kabla ya Uchaguzi Mkuu.

Mheshiwa Naibu Spika, pili, Gereza la Ilagala Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea gereza alitoa agizo la kugawiwa wananchi ekari 3,500 kati ya ekari 10,500 ili wananchi wapate maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ombi, tangu agizo hilo la Waziri Mkuu hakuna kilichotekelizwa, tunaomba Wizara isimamie utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Wilaya ya Uvinza, Jimbo la Kigoma Kusini ni mionganoni mwa Wilaya ambazo wananchi wake hawajapata vitambulisho vya *NIDA*, tunaomba Wizara isimamie zoezi la utolewaji vitambulisho kwa Mkoa mzima wa Kigoma kwani tatizo kubwa ni uhamiaji kupewa zoezi la uhakiki wa uraia wakati kila kijiji kina Kamati

za Ulinzi na Usalama. Kwa nini Uhamiaji wasikasimishe madaraka kwa Kamati hizo ili zoezi hili liwe jepesi kwani Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji ndio wanao wajua kina nani ni raia na kina nani sio raia.

Mheshiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo zoezi litakuwa jepesi, watoa huduma wa vitambulisho vya NIDA Mkoa wa Kigoma tuletewe wa kutosha kwani mkoa una majimbo nane na jiografia yake sio rafiki.

Mheshiwa Naibu Spika, mwisho Wilaya ya Uvinza ni mpya, hakuna jengo la Makao Makuu ya Polisi Wilaya, hakuna nyumba za watumishi, hakuna vitendea kazi kama pikipiki, hivyo tunaomba wapate pikipiki angalau kumi ili waweze kufanya doria kwenye vijiji vyenye miundombinu korofi.

Mheshiwa Naibu Spika, mwisho naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi kubwa inayofanywa na majeshi yetu, naomba kutilia mkazo mambo kadhaa ili yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Kitengo cha Upelelezi katika Jeshi la Polisi kiimashwe kwani kimekuwa ndiyo chanzo cha mrundikano wa mahabusu kwenye magereza yetu. Hii imetokana ama na uchache wa kutokuwa na weledi wa kutosha jambo linalopelekea kesi kuchukua muda mrefu na hatimaye kutupiliwa mbali.

Mheshiwa Naibu Spika, pili, watuhumiwa wa makosa madogo madogo watumikie adhabu zao wakiwa nje ya magereza na yale makosa yanayodhaminika, basi watuhumiwa wadhaminiwe na waendelee kusikiliza mashauri wakiwa nje ya mahabusu.

Mheshiwa Naibu Spika, tatu, kumekuwa na vitendo visivyo vya kitaaluma katika kutimiza majukumu yao kwa baadhi ya maaskari magereza hali inayopelekea matatizo na hata maafa kwa wafungwa kutokana na kuadhibiwa na maaskari hao.

Mheshiwa Naibu Spika, mfano tukio la tarehe 22/02/2020 katika Gereza la Nansio Wilayani Ukerewe ambapo mfungwa mmoja alifariki dunia na mwingine kuumizwa vibaya kutokana na kipigo kutoka kwa maaskari wa gereza hilo.

Mheshiwa Naibu Spika, nne, kwa kuwa lengo letu ni kufanya magereza yetu yajitosheleze kwa chakula, basi Magereza yaliyo na rasilimali ardhi yasaidiwe ili maeneo yatumike kama dhamana ili wapate mikopo kama mtaji wa uzalishaji kwenye maeneo yao.

Mheshiwa Naibu Spika, tano, mkwamo uliopo katika zoezi la upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa upate ufumbuzi ili mateso wanayopata wananchi katika kufuatilia na kupata vitambulisho hivyo yaishe.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, wewe binafsi Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya usalama wa raia hasa kurudisha uwabikaji kazini iliopelekea kupungua kwa uhalifu. Pia kwa kusimamia vizuri, rushwa na upendeleo umepungua kwa kiasi kikubwa kupelekea wananchi kushiriki kikamilifu shughuli za ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mbalizi, Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, askari bado wanaendelea kufanya kazi katika mazingira magumu kwa kukosa majengo ya Kituo cha Polisi na kuendelea kutumia jengo dogo liliokuwa *Police Post* kuhudumia Kijiji cha Mbalizi. Ni vigumu sana kwa Wilaya yenye askari 156 kufanya kazi kwenye hiki kibanda kidogo na ukichukilia kinahudumia wakazi karibu 500,000. Hii ni changamoto ya kiafya na pia kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali itoe kwa haraka bajeti ya ujenzi wa Kituo cha Mbalizi ya shilingi milioni 50 iliyokuwa imetengwa mwaka 2019/2020. Kwa vile katika ujenzi huu, wananchi wamejitoa kwa kiasi kikubwa, kiasi hiki kitachochaea kumalizia ujenzi wa maeneo muhimu ya kituo na kuwezesha huduma kuhamia kwenye majengo mapya ya kituo hiki. Hatua hii ni muhimu kwa askari na wateja wao hasa kipindi hiki tunapopambana na janga la *corona virus (Covid-19)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa huruma yake na mimi kuniwezesha kuwepo mahali hapa na kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2020/2021. Hotuba hii inakwenda kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020 kama ilivyoelekeza hasa kuhakikisha usalama wa raia na mali zao unaendelea kuwa wa uhakika. Kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kumpongeza Waziri pamoja na jopo lake lote kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza kuchangia kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoendelea kufanya kwa kuhakikisha majeshi yote ambayo yapo chini ya Wizara yana hali nzuri na utayari katika utekelezaji wa majukumu yao. Hata hivyo Jeshi letu la Polisi limekuwa likifanya kazi kwa ukaribu sana na wananchi na kupelekea matokea chanya, ila ielevweke kuwa uhiari wa umma kufuata agizo la polisi na kutoa ushirikiano, unatokana na uaminifu wake kwa Jeshi la Polisi kutokana na mfumo wa uwajibikaji wa polisi unaoaminika. Hivyo, naishauri Serikali kuwa ni budi kutambua umuhimu wa uwajibikaji wa polisi kwa kuleta sio tu, utawala bora wa sheria na haki, lakini pia kujenga uaminifu wa umma kwa polisi. Kuimarisha mfumo wa uadilifu na uwajibikaji wa Jeshi la Polisi, hii hukusudia kujenga ufanisi wa polisi na uaminifu wa umma kwa polisi, hali kadhalika uwajibikaji na usimamizi wa polisi ndiyo kiini cha utawala wa demokrasia ambaeo ni muhimu katika kuleta utawala wa sheria na kurejesha imani ya umma kwa jeshi la polisi, vilevile kukuza na kuendeleza uwazi, maadili na haki za binadamu mionganoni mwa Jeshi la Polisi na kujenga uhusiano mzuri kati ya polisi na umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kufuatia uwanda mpana wa dhana ya uwajibikaji wa polisi, miundo ya kisheria madhubuti ambayo huundwa Barani Afrika na kwengineko duniani ni utaratibu mzuri na wenye tija kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa muhtasari wa mambo muhimu yanayohusu mfumo wa uwazi katika Jeshi la Polisi kama ushauri kwa Serikali yangu na kutilia mkazo vipengele vilivyosahaaulika vya uwajibikaji ndani ya jeshi na mamlaka huru ya kiraia ya usimamizi wa polisi nchini kwetu. Sheria ya Kimataifa huunda misingi ya mifumo ya uwajibikaji ambapo dhana kuu muhimu ni haki ya kupata ufumbuzi. Hivyo, Serikali haina budi kutengeneza mwongozo utakaowezesha umma kupata suluhu kipindi haki zao za msingi zinapokiukwa, kwa mfano kuhakikisha mtu anapata ufumbuzi thabiti ambaeo uhuru au haki zake zitakuwa zimekiukwa licha ya kuwa ukiukwaji huo umefanywa na mtu wa mamlaka, kuhakikisha mtu anayetoa madai ya ufumbuzi

huo anapatiwa haki yake kupitia mahakama, utawala au mamlaka ya kisheria au mamlaka yoyote ilioainishwa na sheria za nchi ili kuhakikisha ufumbuzi wa kimahakama na kuhakikisha mamlaka zenyu uwezo zinazingatia utekelezaji wa ufumbuzi huo kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uadilifu ni jambo zuri sana katika kila sekta hapa nchini kwetu, kutokuwa mwadilifu ni kiini cha uhalifu hasa ukizingatia Jeshi letu la Polisi lina wajibu wa kuhakikisha askari wote wanakua waadilifu ili kulinda maadili na kiapo walichoapa.

Natoa pongezi kwa Jeshi letu la Polisi kwa kuhakikisha maadili ni sehemu muhimu na inatekelezwa kwa weledi mkubwa ili kulinda hadhi ya chombo hiki, lakini kumekuwa na changamoto ndogo ndogo kwa baadhi ya askari wetu wasiokuwa na weledi na waaminifu kwa kukiuka baadhi ya maadili na kuleta taswira mbaya kwa Jeshi letu, watu hawa wakibainika ni wajibu wa viongozi kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Jeshi letu la Polisi liendelee kupata ushirikiano wa karibu na raia, hapana shaka ni wajibu wao kufanya kazi kwa kufuata sheria, taratibu na maadili. Naishauri Serikali kuhakikisha wanawakumbusha wajibu wao askari wote ili kuondokana na ufanyaji kazi wa mazoea ambaao hauliletei Jeshi letu la Polisi sifa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limejitahidi kwa namna moja kufanya shughuli zake kwa wakati na kwa umakini sana, ila kuna changamoto mbalimbali zimekuwa zikijitokeza kwa baadhi ya maeneo kwa wananchi kulalamika namna ya utendaji wa baadhi ya askari wetu, suala la kubambikiwa kesi limepungua lakini bado lipo kwa baadhi ya maeneo, kunyimwa dhamana kwa baadhi ya makosa ambayo ni ya kawaida ilhali dhamana iko wazi yamekuwa ni malalamiko toka kwa wananchi, ucheleweshaji wa uchunguzi na kupelekea mtuhumiwa kukaa mahabusu kwa muda mrefu ni tatizo ambalo wananchi wanakutana nayo mara kwa mara.

Naishauri Serikali hasa katika suala zima la uchunguzi wa kesi, kuhakikisha kabla ya ukamataji basi wawe wamejiridhisha vya kutosha ndipo wafuate utaratibu wa kukamata na kufungua mashtaka, hii itasaidia kesi nydingi kwenda na kumalizika kwa wakati, tumeshuhudia mara kadhaa kesi zikiahirishwa mahakamani kwa sababu tu ya uchunguzi kutokukamilika, kufanya hivi kutasaidia kupunguza kero ambayo wananchi wamekuwa wakikutana nazo. Suala la ubambikiaji wa makosa, ni vyema askari yejote anayekutwa na kosa la kumbambikia raia kesi achukuliwe hatua kali za kisheria na kufutwa kazi na kufunguliwa mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia sasa tunakabiliana na janga zito la ugonjwa wa Corona (*Covid-19*), janga hili bado halijapatiwa ufumbuzi wala tiba, kutokana na aina ya maambukizi ya ugonjwa huu, naomba kuishauri Serikali kuchukua hatua za haraka hasa katika magereza yetu yote nchi nzima, tahadhari kwa kuепuka mirundikano katika magereza kwa wafungwa na mahabusu, hii itasaidia kuwakinga na aina yoyote ya maambukizi kama ikitokea ugonjwa huu ukafika huko. Aidha, naipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za haraka za kuzuia wananchi kwenda kutembelea ndugu zao katika magereza yote nchi nzima, hatua hii itasaidia kuепusha maambukizi ya aina yoyote yanayoweza kutoka nje na kupelekwa ndani, tukizingatia na mrundikano wa wafungwa katika magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua juhudini kubwa zinazochukuliwa na Serikali hasa kuhakikisha Idara ya Uhamiaji inatekeleza majukumu yake ipasavyo, kuhakikisha miundombinu inaimarishwa mara kwa mara kuendana na wakati hasa katika dunia ya leo ambayo teknolojia imetawala, hatua ya kufanya maombi ya *passport* kwa njia ya kieletroniki ni hatua nzuri na itasaidia kupunguza msongamano katika Ofisi za Uhamiaji. Naipongeza Serikali juu ya mafanikio hayo, pia napenda kuishauri Serikali kuendelea kuzifanyia kazi changamoto zilizopo ili kuboresha huduma na utendaji wa Maofisa wa Uhamiaji, aidha, kuwaboreshea miundombinu ili kuwawezesha kufanya

majukumu yao kwa urahisi, hasa katika kukabiliana na wahamiaji haramu, kama tujuavyo nasi kama nchi tumekuwa tukipokea wahamiaji haramu toka maeneo mbalimbali, baadhi ya wananchi wasiokuwa waaminifu na wazalendo kwa nchi yao wamekuwa wakiwapa ushirikiano wahamiaji hao huku wakijua wanavunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuchukua baadhi ya hatua kama kufanya misako na ukaguzi wa maeneo mbalimbali ikiwamo nyumba za kulala wageni na katika vyombo vyya usafiri pamoja na udhibiti wa mipaka kati ya Tanzania na nchi za jirani. Misako na udhibiti huo utasaidia kukamatwa kwa wahamiaji katika maeno mbalimbali hasa wengi wao wakiwa wanaitumia Tanzania kama njia ya kwenda katika mataifa mbalimbali hususani yale ya Kusini mwa Afrika kwa lengo la kusaka maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishatangulia kusema hapo awali, kwa kiasi kikubwa wanaowasafirisha wahamiaji hawa wanatajwa kushirikiana na Watanzania wasiokuwa waaminifu, wanaolenga kujipatia kipato pasi kujali usalama wa Taifa lao. Lakini kwa uzalendo wa hali ya juu maofisa wetu wamekuwa wakifanya kazi kwa weledi mkubwa na kuwabaini watu hao na kuwafikisha katika vyombo vyya sheria. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Maofisa wa Uhamiaji kwa uzalendo mkubwa hasa kuhakikisha wageni wanafuata taratibu na sheria kuingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu la Zimamoto linaendelea kufanya kazi katika viwango vizuri tofauti na hapo awali, tumeshuhudia sasa majanga ya moto yanapotokea basi mara moja Jeshi la Zimamoto linapopata taarifa linafika eneo la tukio kwa wakati ingawa kuna changamoto ya miundombinu kwa baadhi ya maeneo yamekuwa hayafikiki.

Naiomba Serikali kuongeza idadi ya magari kwa Jeshi la Zimamoto ili kusaidia kuyasambaza mikoani kwa wingi, tukiwa na magari ya kutosha tutaweza kukabiliana na majanga ya moto pindi yatakapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunga mkono juhudzi za Mheshimiwa Rais wetu John Pombe Joseph Magufuli, na mimi nikiwa mdau mkubwa hasa katika maendeleo, nimechangia mara kwa mara Jeshi letu la Polisi hasa Jimboni kwangu kwa kuzingatia umuhimu wa majukumu yao ya kila siku na changamoto wanazokabiliana nazo, nimejenga baadhi ya Vituo vya Polisi na vingine viko katika hatua za mwisho kukamilika, nimechangia vitu mbalimbali kulingana na mapungufu yaliyopo wakati husika, kwani nimekuwa karibu sana na uongozi wa Polisi Wilaya, tumekuwa tukishirikiana mara kwa mara na pale panapotokea jambo lolote basi hawasiti kunishirikisha, naweza sema sisi Wanakibaha Vijijini tuko vizuri, wananchi na Jeshi la Polisi wana ushirikiano mzuri na matukio ya kihalifu yamepungua.

Naiomba Serikali kutuangalia hasa katika changamoto ambazo bado tunakabiliana nazo, nyumba za askari, vitendea kazi kama usafiri na kadhalika vinahitajika ili kuwawezesha askari wetu kufanya doria eneo kubwa zaidi na kufika kwenye matukio kwa wakati, aidha, suala la nyumba litasaidia kuwatoa askari wetu huko maeneo mbalimbali wanakoishi na kuwaweka sehemu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri. Nawapongeza sana kwa jinsi walivyoweza kudhibiti ajali za barabarani. Hii imesaidia kuokoa maisha ya Watanzania walio wengi. Kwa kuwa ajali nyingi zinatokana na pikipiki, napendekeza madereva wa pikipiki wasiofuta sheria wachukuliwe hatua kali, ukaguzi wa leseni zao ufanyike mara kwa mara na elimu iendelee kutolewa juu ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa mikakati yao ya kuhakikisha walengwa wanajilisha na kujitosheleza kwenye vyakula. Kwa sababu magereza ziko kila Mkoa, kila Mkoa utenge eneo la kutosha ili wafungwa

hawa walime, wajitosheleze kwenye chakula, wauze ziada ili kupata fedha za kuchangia shughuli nyingine nhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NIDA*; utoaji vitambulisho imekuwa shida kwa baadhi ya watu. Baada ya kujaza fomu, kama utaonekana uraia wako una utata kidogo au Maafisa wa Uhamiaji wakiwa na maswali fulani fulani, inabidi mwananchi awafuate Maafisa Wilayani. Wote tunajua kuwa wapo Watanzania amba ni maskini au wazee si rahisi kwao kupata nauli za kuwa wanakwenda Wilayani kila wakihitajika.

Kwa kuwa wanaowafahamu wakazi wa eneo kama ni Watanzania au laa, wako huko vijijini, hivyo Maafisa wa Uhamiaji na wa *NIDA* wawafuate wananchi huko huko vijijini badala ya kuwasumbua kwenda Wilayani. Tunaomba zoezi hili likamilike mapema kwani watu wamefungiwa simu zao na hawana mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kadri nchi yetu inavyoendelea kupata maendeleo, tunajenga majengo makubwa na marefu, ninaomba bajeti ya Wizara hii iongezwe ili Idara ya Zimamoto waweze kununua magari na mitambo mikubwa ya kuweza kuzima moto kwenye nyumba ndefu zenyen ghorofa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia pia nimpongeze Waziri kwa kazi kubwa anayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa taarifa kuwa Wilaya mpya kama Mkalamu wanayo majengo ya Wilaya ya Polisi ambayo hayajaamilika pamoja na fedha nyingi kuwekwa. Ni lini maboma haya yatakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wilaya hizo zina changamoto ya makazi ya Polisi. Wizara ina mpango upi wa kimkakati utakaoweza kutatua tatizo hill?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya Wizara muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuwasilisha kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza ni kuhusu vitendea kazi katika Jeshi la Polisi. Naipongeza Serikali kwa juhudhi kubwa inayochukua ya kuboresha jeshi hili. Lakini bado katika suala la vitendea kazi hasa usafiri hajawa ya kuridhisha. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee kuchukua juhudhi ya kulipatia jeshi hili usafiri ili kuweza kumudu kazi zake katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali nimshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe makazi ya askari wetu katika Mikoa yote kama ilivyojenga nyumba bora na za kisasa zilizopo *Kilwa Road*, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali inunue magari ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya doria, pia kutumika kwa ajili ya kupeleka mahabusu mahakamani maana wakati mwininge mahabusu wanashindwa kuhudhuria mahakamani kwa sababu ya kukosa gari la kuapeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe maslahi ya askari wetu hususan mishahara yao maana kazi wanazofanya ni kubwa na wanazifanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe majengo ya magereza yetu sababu mengi ni machakavu, hivyo yaboreshwe kuwa ya kisasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itoe elimu ya kutosha kwa askari wa usalama barabarani kuondokana na tabia ya kubambikia makosa madereva kwa kutumia kipima mwendo yaani *torch*, mara nyingi wakikamata gari mfano basi la kampuni fulani wao hawaoneshi namba ya gari ya basi hilo ila kinachoonekana katika kamera ni jina la kampuni ya basi. Hili tatizo maana kuna kampuni inakuwa na mabasi zaidi ya kumi na yanapita njia hiyo hiyo kila baada ya nusu saa, hivyo *traffic* hao hutumia picha hiyo moja kukamata magari yote ya kampuni hiyo na kuwaandikia faini kwa uonevu. Nashauri tabia hiyo irekebishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwenye Kikosi cha Zimamoto, kuna mtindo wa kuwalazimisha wamiliki wa maduka kuweka vizima moto (*fire extinguisher*) ndani ya maduka yao, utaratibu huu hausaidii kuokoa mali za wananchi wakati janga la moto litakapotokea hususan nyakati za usiku maduka yamefungwa na mmiliki hayupo eneo la tukio. Nashauri baada ya kikosi hicho kuwalazimisha kuweka ndani, waweke nje kwenye *corridors* iwe rahisi kuokoa mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nashauri fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi hiyo.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo; awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kumkabidhi Wizara hii ngumu Mheshimiwa Simbachawene. Kwa kweli Mheshimiwa Rais ana maono ya hali ya juu maana

mimi namfahamu Mheshimiwa Simbachawene ni simba kweli kweli ambaye anajua namna ya kuwinda bila kupiga kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili ya kumkabidhi Waziri huyu mchapakazi, kwanza nimuombe Polisi Wilaya ya Namtumbo haina jengo lake la kutolea huduma. Aidha, jengo wananolitumia lipo ndani ya *road reserve* na hivyo linatakiwa libomolewe. Jengo hili ni la zamani na linavuja sana. Hebu Mheshimiwa Waziri George Simbachawene tujengee jengo la Polisi la Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ninayoitaka Mheshimiwa Waziri aipokee ni uhitaji wa magari ya Polisi kwa Vituo vya Polisi mbalimbali vya Wilaya ya Namtumbo hususan Kituo cha Polisi cha Lusewa ambacho kipo kilometra zaidi ya 100 kutoka Makao Makuu ya Wilaya na changamoto za mpakani ni nyingi. Tunaomba gari kwa kituo hiki na vingine vya Mkongo Gulioni, Namabengo na Namtumbo yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa utendaji mzuri sana, namwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwajaalia afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa nyumba za Maafisa Uhamiaji wanaofanya kazi katika mpaka Malawi na Tanzania eneo la Manda hawana nyumba za kuishi, ni vizuri Serikali iwajengee nyumba maafisa hawa ili wafanye kazi kwa *morale* zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maafisa Uhamiaji wanaofanya kazi katika mpaka huu wa Malawi na Tanzania eneo la Manda hawana usafiri, yaani gari na boti za kufanya *patrol*. Hivyo ni muhimu eneo hili la Manda wakapewa boti angalau moja na gari la *patrol*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukidhibiti wahamiaji haramu wanaopita kwenye maeneo ya nchi yetu kuelekea nchi nyingine kama Afrika ya Kusini kwa gharama kubwa, wakati nchi nyingine za jirani zimekuwa zikiruhusu wapite. Napendekeza tujaribu kuangalia uwezekano wa kuruhusu waweze kupita ili mradi hawatakuwa wanajihusisha na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano wa mahabusu na watuhumiwa kwenye Vituo vya Polisi, tatizo hili ni kubwa nchini. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mahakama waangalie uwezekano wa kutoa dhamana kwa makosa madogo madogo na kutoa hukumu za kifungo cha nje kuliko kupendelea kifungo cha ndani. Hii itasaidia kupunguza msongamano mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi ya Tarafa za Vijiiji Vituo vya Polisi ni chakavu sana, kwa mfano, Kituo cha Polisi cha Lupembe Wilaya ya Njombe ni chakavu sana jengo la kituo hiki lilikuwa ni zahanati na mwaka 1985 baada ya kuhamisha zahanati ndipo jengo hili likawa kituo cha polisi. Tunaomba Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha kwa ajili ya Kituo kipyaa cha Polisi. Pia eneo la Kata ya Mtwango halina Kituo cha Polisi lakini kuna benki na ni eneo lenye watu wengi. Huduma za kipolisi zinapatikana Makambako au Njombe Mjini ambako ni mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunilinda hadi leo hii tunapofikisha miaka mitano ya uhai wa Bunge letu, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu ndugu zetu Watanzania wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, viongozi mbalimbali na wananchi waliotangulia mbele za haki, tuendelee kuliombea Taifa kutokana na janga hili la Corona linalotikisa dunia nzima kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kumpongeza sana

Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Samia Suluhu Hasan, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri mkuu, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge letu na waandamizi wote Serikalini kwa jinsi walivyosimamia Serikali kutekeleza Ilani ya CCM 2015 - 2020. Kwa hakika tumeng'ara kitaifa mbele ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu kuishauri Serikali kuhusu Wizara hii. Kwanza, Serikali isimamie upunguzaji wa mahabusu katika magereza yetu nchini kwa kupunguza masharti yasiyo ya lazima kupata dhamana, kutathimini utendaji kazi wa Maafisa Upelelezi hususan ubabaishaji, urasimu na kutokuharakishwa kwa taarifa ya upelelezi unaofanywa na maafisa waliokaa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya huduma kwa Jeshi la Magereza na Polisi yatazamwe na kuwekwa vigezo kwa kuangalia vipaumbele vya umuhimu hususan vipaumbele vya bajeti zilizopitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye mapitio ya fursa za kiuchumi na uzalishaji kwa magereza yote nchini zilizoko kwenye nyanja za kilimo, ufugaji, viwanda na shughuli zingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hali ya makazi ya askari nchini ni mbaya kutokana na ukosefu wa nyumba, uchakavu, Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kuitia bajeti zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za maendeleo katika bajeti zetu za Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hususan Magereza na Polisi tutumie *force account* na nguvu kazi ya wafungwa ili kupata matokeo makubwa kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi mimi naona suala la kuwa na mahabusu ya polisi kila Wilaya nchini ni kuibebesha

Serikali yetu mzigo mkubwa usio na sababu kwa kuwa kutakuwa na wahalifu ambao watahudumiwa na Serikali kwa gharama kubwa hivyo tuangalie ikama ya Maafisa Upelelezi kwa ngazi ya Wilaya na kusimamia kikamilifu uwajibikaji wao wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto kubwa sana ya wafanyakazi wa Uhamiaji. Mfano Ngara wanahamishwa watano halafu wanaletwa wawili. Hivyo tunaomba Uhamiaji watuongezee wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna changamoto ya usafiri, Uhamiaji Wilaya ya Ngara hawana gari ya kufanya doria. Tunaomba uhamiaji Ngara tupate gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngara tuna changamoto ya gari ya magereza, hatuna gari ya kupeleka mahabusu kwenye kesi zao. Hivyo tunaomba gari lipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba za askari hazitoshi na zilizopo ni chakavu sana, hazifai katika Mkoa wetu wa Kagera na askari wengi wanaishi mitaani. Mfano imetokea dharura hadi polisi afike kwenye eneo inakuwa ni balaa tayari.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais ambaye ni Jemedari Mkuu. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika na wewe mwenyewe Naibu Spika kwa uongozi mzuri kwenye Bunge letu tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu na maombi ni kuimarisha ujenzi wa Vituo vya Polisi na hasa katika Mkoa wangu wa Morogoro. Serikali yangu imefanya mambo mazuri na makubwa, naomba iendelee hivyo hivyo, chini ya Mheshimiwa Waziri Simbachawene.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa sasa ulinzi umeimarika sana na mfano mzuri ni katika Msitu wa Biharamulo, hapo miaka ya nyuma wasafiri walikuwa wanasingidikizwa na polisi kwenye mabasi na kwenye magari madogo, lakini kwa sasa mambo ya kusindikizwa hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tatizo la vitambulisho vya *NIDA* bado ni tatizo. Ni vyema jambo hili likafanyiwe kazi. Ni vyema kila Mtanzania akawa na kitambulisho chake kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa haya machache naomba yafanyiwe kazi na Serikali yangu sikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na kuendelea kunikinga na janga hili la Corona. Pili, naomba kukupongeza wewe Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, Katibu wa Bunge, pamoja na watumishi wote wa Bunge kwa kuendelea kuliendesha Bunge hili kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote katika Wizara hii kwa namna wanavyosimamia usalama na amani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo hapo juu sasa naomba nianze mchango wangu kwa kuishauri Serikali kwa mambo yafuatayo; nikianza na makazi ya maaskari polisi. Kumekuwa na uhaba mkubwa sana wa

nyumba za maaskari nchini sambamba na ofisi za maaskari hao hapa nchini. Maaskari wengi nchini wanakaa au kupanga uraiani. Mfano katika Wilaya ya Liwale yenyé Tarafa tatu na Kata ishirini hajawahi kuwa na jengo la Kituo cha Polisi wala nyumba za watumishi. Wilaya hii ina umri wa miaka 45, lakini ziko Wilaya mpya tayari zina majengo hayo niliyoyasema. Je, Mheshimiwa Waziri atawapa lini Wanaliwale huduma hii muhimu kwa usalama wao?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Magereza; pamoja na kwamba Serikali kufanya vizuri sana katika kuwajengea makazi bora maaskari wa idara hii lakini bado kuna magereza kadhaa nchini hazina majengo wala ofisi za maaskari wake. Mfano Magereza ya Liwale; magereza hii imeasisiwa tangu mwaka 1982, magereza hii bado ina jengo la tope ambalo limezungukwa na uwa (*fence*) ya miti. Hata hivyo eneo liliopojengwa gereza hili bado haliljalipwa fidia kwa wenye mashamba hadi leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri awaeleze Wanaliwale ni lini wananchi wale watalipwa fidia ya mashamba yao? Je, ni lini gereza lile litapata majengo ya kisasa yenyé hadhi ya magereza nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho vya *NIDA*; changamoto kubwa katika taasisi hii ni upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa. Je, Vitambulisho vya Taifa ni mradi? Na kama ni mradi je, mradi huu utaisha lini na utaligarimu Taifa kiasi gani? Changamoto nydingine katika hili ni uhaba wa watumishi hasa katika Wilaya yangu ya Liwale kuna uhaba mkubwa sana wa watumishi wa idara hii jambo linalosababisha hadi leo kukosa vitambulisho, kwani hata namba za hivyo vitambuliso havipatikani katika Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho mimi niombe Wizara hii kuendelea na kufanya kazi kwa weledi hasa Idara ya Polisi na uhamiaji, kwani bado wako watumishi wa idara hizi wanaendeleza tabia ya njoo kesho, njoo kesho, katika hili naiomba Wizara kuongeza udhibiti kwa hao watumishi

wachache wanaotaka kuichafua Serikali yetu. Vilevile katika Jeshi la Polisi wapo maaskari wanawabambikia kesi raia wema na kuwaomba rushwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa juhudzi zake kubwa zinazofanywa kuitia sekta hii muhimu sana ya kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika harakati kubwa zinazofanywa na taasisi hii niombe sana Serikali kuiongezea bajeti ya kutosha ili waendelee kufanya kazi zao kwa urahisi zaidi. Mara nydingi sana wamekuwa na upungufu wa mafuta ya ufatiliaji pale inapotokea dharura, lakini pia wamekuwa na uchache wa vitendea kazi vinavyowawezesha kufika haraka kwenye matukio. Pia wamekuwa na malalamiko ya fedha wanazodai ambazo wameshazitumikia kuchelewa kulipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha uchaguzi na matukio mengine ya kutuliza ghasia ili kuimarisha amani kwa wananchi wamekuwa wakilazimika kufanya kazi usiku na mchana kulinda amani ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki cha kujikinga na maambukizi ya virusi vinavyosababisha homa kali ya mapafu - Corona, wamekuwa wanafanyakazi kubwa sana katika nchi hii kuwasaidia wananchi kuendelea kudhibiti maambukizi ya Corona. Pamoja na hali hiyo wanayoendelea nayo katika kipindi hiki wanahitaji kupewa mavazi maalum ya kujikinga na maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la fedha pia linahitajika na kuongeza ununuzi wa madawa kwa ajili ya

askari hawa ambao wanapambana na walioambukizwa wagonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa madawa kwa ajili yao itawasaidia kuwa na uhuru zaidi wa kuendelea kufanya kazi na wanaendelea nazo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ulimwengu unapita katika changamoto ya virusi vya Corona, ni lazima vyombo vya ulinzi na usalama viandaliwe kwani pamoja na matatizo ya afya lakini kuna matatizo ya kiuchumi na kijamii yanayosababisha umaskini mkubwa na umaskini njaa na mtu mwenye njaa ni mtu mwenye hasira, hivyo Serikali ilione hili kama ni tatizo na kutatta.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya madereva bajaji na bodaboda bado wanateseka na askari wasio waaminifu kuwakamata kiholela na kudai rushwa ndogo kwao, je, Serikali hii inachukua hatua gani kuwasaidia vijana hawa ambao wanajitafutia maisha yao kwa hali ngumu katika awamu hii ya tano ambayo umaskini umekithiri na Serikali imeshindwa kuajiri vijana?

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri machache yafuatayo kwenye hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pasi za kusafiria za *EAC* zitolewe Makao Makuu ya Wilaya za mpakani na isichukue muda mrefu kwa mwombaji kupata kama anastahili kuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa Vitambulisho vya *NIDA* vinachukua muda mrefu mno kupatikana, Wizara waje na mfumo wa kuharakisha zoezi la ku-issue vitambulisho vya *NIDA* kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Polisi Wilayani Longido wana shida kubwa kwa suala la matengenezo ya magari yao mawili tu walijonayo na baya zaidi hata hayana matairi na mara nyingine mafuta, hivyo naomba Waziri awape kipaumbele Wilaya ya Longido kwani ni eneo nyeti la mpakani na ni muhimu magari yetu ya doria yakawa mazima na yawe na mafuta na matairi wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kwa suala la Corona, naomba Wizara iwape haki ya dhamana mahabusu wote ambao kesi zao sio za matukio ya kihaini ili watoke na kwa njia hiyo tupunguze msongamano magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Longido tuna uhaba mkubwa wa nyumba za maaskari, lakini sita, katika Kituo cha Kamwanga, kituo cha polisi Kipyta tulicho jenga kwa nguvu ya wananchi, kinahitaji msaada wa kukimalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba na mwisho wananchi wa Kata ya Mundarara nao wameanzisha ujenzi wa Kituo cha Polisi na ni eneo nyeti lenye Migodi ya Ruby na kituo hicho pia kinahitaji msaada wa Serikali kuwaunga mkono wananchi kumalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, dakika tano, Mheshimiwa Masauni ajiandae.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpe pole kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene kwa kumpoteza mzazi wetu. Kwa kuwa nina dakika chache niende moja kwa moja kwenye hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nataka kufafanua ni kwamba tupo kwenye kipindi cha janga kubwa la kidunia ambalo bahati mbaya sana halijui mipaka, *social status*, kabilia au rangi. Unaweza ukalifananisha janga hili

pengine na vita. Katika mazingira kama haya utulivu wa viongozi lakini pia wa wananchi unahitajika sana. Kwa msingi huo, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa uongozi thabitii kwenye kipindi hiki kigumu ambacho nchi yetu pamoja na dunia nzima inapitia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema napongeza? Watu wengi wangetamani, huwa naona sana kwenye *group* la Wabunge *tweets* za Mheshimiwa Lema akilalamika juu ya mambo mengi, mojawapo kubwa ni kwamba kwa nini sisi hatujafanya *lockdown*. Rais wetu aliona mbele, hakuwa anafanya kazi ya kuzima moto huku amejifunga kitamba cheusi usoni, alikuwa anaona mbele kwamba nini kitatokea. Kwa sababu Rais wetu ni Rais wa wanyonge na anayafahamu maisha halisi ya watu wa kipato cha chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya *lockdown* ingefaa sana kwenye nchi zilizoendelea ambazo watu wake wana uelewa mkubwa, *literacy rate* ni kubwa, uwezo wa kiuchumi ni mkubwa, hauwezi kulinganisha na watu wetu sisi. Sehemu kubwa ya Watanzania walioko kwenye miji yetu inayochipukia ikiwepo Jimbo la Arusha la Mheshimiwa Lema ni watu ambaao wanaishi kwa kufanya kazi leo, analisha familia na wazazi wake kwa kufanya kazi leo, atoe jasho leo, ale leo na familia yake. Ukifanya mikakati ya *lockdown* huku umejifunga kitambaa cheusi usoni watu wa aina hii unawaambia nini? Unatengeneza *safety net* ipi kwamba wataishije na familia zao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Rais wetu aliangalia kabla ya janga, kipindi cha janga na baada ya janga, kabla hatujafika. Ndiyo maana akatoa mwongozo kwamba tusiende huko lazima tuangalie maskini wa Tanzania ambaao ndiyo asilimia kubwa. Vinginevyo maskini wetu badala ya kufa kwa *Corona* wangekufa aidha kwa kupigwa na polisi, ama na vyombo vyaya ulinzi kwa sababu watakuwa wamevunja misingi ya *lockdown*, ama wangekufa kwa njaa ndani ya nyumba zao kama tungeenda kwenye *lockdown*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa mikakati iliyowekwa na Serikali imezaa matunda kwa kiasi kikubwa. Shirika la Afya Duniani lilitoa tathimini yake likasema ifikapo katikati ya mwezi Aprili takribani wiki moja iliyopita 15 Aprili, 2020 tungengekuwa tumefikisha idadi ya wagonjwa 1,000 na kwamba itakapofika mwezi Mei katikati, tarehe 15 mwezi ujao, wiki tatu kuanzia sasa, tutakuwa tumefikisha idadi ya *cases* zipatazo 10,000. Tarehe 14 tulikuwa hatujafika *cases* hata 100. Huu ni ushahidi kwamba mikakati iliyowekwa na inayotekelizwa na Serikali na vyombo vyake mbalimbali inafanya kazi. Hilo tu inatosha kwa sababu tulikadiriwa kwamba kufikia katikati ya Aprili tungefika 1,000 hatukuwa tumefika hata 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo watu katika kipindi hiki cha taharuki cha janga kubwa kama hili tuwe wamoja, tupo vitani, tusibeze wala kudharau jitihada ambazo zinafanywa na wenzetu. Hata kama hatuko madarakani lakini *Corona* kama nilivyosema awali haichagui, uwe CCM au CHADEMA itakupa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sasa Serikali toka wiki mbili zilizopita inafanya mikakati ya kuimarisha *contact tracing*, namna ya kuwafuatilia watu ambao wameathirika na ule mzunguko wao wote. Pili, inafanya mikakati ya kuongeza mavazi ya kujikinga (*PPEs*) kwa wataalamu wetu walioko mstari wa mbele kwenye sekta ya afya. Hiyo ndiyo mikakati ambayo tunaamini itatusaidia kuimarisha mapambano dhidi ya *Corona virus*. Mkakati wa mwisho ni kuimarisha mifumo na miundo ya kupima watu ambao wameathirika lakini pia kutoa tiba kwa wale ambao watakuwa *critical*. Hii ni mikakati ambayo tunaamini itatuvusha salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Masauni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ingawa lazima nikiri kwamba sikuwa natambua kwamba ratiba imebadilika bado nilikuwa nadhani kwamba pengine bajeti yetu ingechukua siku mbili, hata hivyo nakushukuru kwa fursa hiyo. Lakini kabla sijachangia chochote naomba nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya Ulinzi na Usalama nchini kwa kuendelea kuwa na imani na mimi katika nafasi hii ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kumshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Waziri Mkuu, vilevile kwa jinsi ambavyo na wao wanawenza kufanya kazi zao vizuri na kutupa sisi ushirikiano pale unapostahiki. Nitoe shukrani zangu vilevile kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Simbachawene kwa kweli Mheshimiwa Waziri Simbachawene amekuja kwa muda mfupi tumefanya kazi nae kwa muda mfupi lakini ni aina ya Waziri ambaye ananipa ushirikiano mkubwa sana. Namshukuru sana na katika kipindi kifupi ambacho tumefanya kazi mimi na yeze tunaendelea vizuri pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wote wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi mbalimbali na wafanyakazi wenzetu pamoja na Makamanda wote nchi nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Mkwajuni kwa kunistahimilia kutokana na majukumu haya yanasaababisha wakati mwingine kukosa muda wa kutosha kukaa jimboni lakini ninaamini kabisa kwa ushirikiano wao tumefanya mambo makubwa sana ya kutosha miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maana kwa kusema mwisho kwa maana ya umuhimu lakini niishukuru sana familia yangu kwa jinsi ambavyo na wenyewe wanani pangu ya

kutekeleza majukumu yangu haya ya kitaifa hususan mke wangu, watoto wangu pamoja na familia yangu yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo sasa naomba niende katika hoja, najua hoja ni nyngi na muda unaweza kuwa usitoshe lakini nitajitahidi kuzijibu kwa kadri itakavyowezekana. Kwanza kabisa nataka nizungumzie kuna jambo moja ambalo limekuwa kwa kweli linanisikitisha sana. Mara nyngi tumekuwa tukisikia hoja hasa kutoka upande wa pili ambazo zinaelekeza lawama kwa jeshi letu la polisi. Kinachonishangaza zaidi leo kwamba imefika wakati sasa kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanaona jeshi letu la polisi kupewa nyenzo za kufanya kazi basi ni *issue*. Nilitaraja kwamba Wabunge hawa ama sisi ambao tunawakilisha tungakuwa mstari wa mbele kwanza kwa kuliunga mkono jeshi letu la polisi kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inafanya ya kusimamia usalama wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, sisi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wanafanya wa upande huu kuwa ndiyo wasemaji wao pale inapobidi kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais za kuleta mapinduzi ama maboresho makubwa hususan ya vitendea kazi na mazingira yao ya kufanya kazi.

Ninyi ni mashahidi juu ya kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya katika miaka mitano iliyopita ya kuimarisha vyombo hivi. Leo katika hotuba Mheshimiwa Waziri amezungumza mambo mengi sana na bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge wengi wanajua juu ya maboresho katika mazingira yao ya kuishi, katika vitendea kazi na kadhalika haya ndiyo mambo ambayo nadhani yalikuwa ni ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza zaidi ni kwamba juu ya kebehi, lawama hizi za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzetu humu lakini leo akitokea mbunge akinyukuliwa kidogo anakimbilia polisi. Ndiyo ile hoja ambayo imezungumzwa ya yule mtu ambaye anasemekana

amepatwa matatizo kule Zanzibar lawama zinapelekwa polisi kinyume, chake ilitakiwa polisi wapongezwe baada ya wananchi wale kuchukua hatua ya kumjeruhi yule raia. Askari polisi walifanya uchunguzi na kuwashikilia watuhumiwa na case yao sasa ipo katika hatua za mwisho. Lakini badala ya kupongeza jeshi la polisi kwa kazi nzuri inayofanywa leo lawama zinapelekwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge mimi nimebahatiwa kuwepo katika wizara hii kwa takribani miaka mitano sasa, nafahamu juu ya kazi na mazingira ambayo jeshi letu la polisi linafanya katika kusimamia usalama wa nchi hii. Siyo haki na si sahihi kulipaka matope na kuliletea lawama jeshi la polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba hakuna changamoto na ndiyo maana hata hotuba hii ambayo tumewasilisha leo hapa mezani imezungumzia juu ya hatua ambayo Serikali imefanya na itaendelea kuzifanya katika kuhakikisha pale zinapotokea changamoto zinazogusa baadhi ya askari wetu hatua zinachukuliwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatusemi kama askari hawa ni malaika lakini hapa hata inapokuja katika hoja siyo tu hizi za uhalifu wa kawaida, hata katika masuala ya usalama barabarani. Leo Waheshimiwa Wabunge hapa wanalalamika baadhi yao wanasema kwamba askari wa jeshi la polisi wa usalama barabarani wengine wanajificha, lakini sijasikia kupongeza juu ya kupungua kwa ajali na vifo, matukio ya ajali kwa zaidi ya asilimia 26 katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Sijasikia juu ya kupungua kwa watu waliofariki kwa ajali kwa zaidi ya asilimia 11, juu ya majeruhi kwa zaidi ya asilimia 19.3, hayo hayasemwi. Lakini haya yamefanikiwa kwasababu ya hizo hizo mbinu ambazo jeshi letu la polisi linatumia kwa mazingira tuliyokuwa nayo kwasababu wahalifu wanatumia mbinu na askari wetu wa usalama barabarani wataendelea kutumia mbinu mbadala kuhakikisha kwamba wanaendelea kuokoa maisha ya watanzania wasiendelee kupotea kwa ajali za barabarani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niliona nilizungumze hilo kwa sababu ni jambo ambalo niliona kwamba lina msingi sana kwa upande wa jeshi la polisi. Kuna mambo mengi ambayo tunayazungumza sasa hivi tuna janga la Corona, askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu leo tunapopambana kuhakikisha tunapunguza mahabusu na wafungwa katika magereza yetu. Lakini askari hawa hawa ndiyo wanalinda wale wafungwa, askari hawa hawa ndiyo wanalinda mahabusu na wenyewe ni binadamu, na wenyewe ni binadamu ikiwa wanafanya kazi hii kwa niaba ya usalama wa raia wa nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka nilizungumze ambalo lilitzungumza na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na hali ya raia na hasa wahamiaji haramu katika mipaka yetu. Bahati nzuri nilipata kutembelea kwa mara nyingine tena katika mikoa iliyopo mipakani muda mfupi uliopita nadhani kama wiki chache zilizopita. Nilitembelea katika maeneo huku ya Kagera, Kigoma, na jambo ambalo naweza kulizungumza kwa ufupi juu ya *concern* ya Waheshimiwa Wabunge. Kwamba lazima tutambue kwamba mazingira ya mipaka yetu, mikoa ambayo iko mipakani ina changamoto kubwa sana. Mikoa hii imepakana na nchi ambazo zilikuwa zina changamoto sana za kiusalama kwa hiyo lazima vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vifanye kazi ya ziada katika kuhakikisha kwamba usalama wa raia wanaoishi maeneo yale unaweza kukidhiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana nao katika hoja moja na ambayo tuli-address jambo hili na leo nataka nilipongeze sana Jeshi la Uhamiaji. Hivi tunavyozungumza jana nilizungumza na Kamishna wa Mipaka juu ya matatizo ya Corona lakini yuko vijijini huko mipakani anashughulikia haya maelekezo ambayo tuliyatoa. Moja la msingi ambalo nasema nikubaliane nalo kwamba lazima na kitu ambacho tunakifanya sasa hivi tunahakikisha kwamba tuwe na nambari ama takwimu za uhakika kuhusiana na idadi ya wakimbizi, wahamiaji haramu na raia halali ambao wanaoishi kwenye mipaka ili kila mmoja apewe haki ambayo anastahili.

Anayestahili kupewa haki yake ya kiraia kwa maana ya kitambulisho cha *NIDA* aweze kupata ambaye ni mhamiaji haramu basi sheria za uhamiaji haramu zinajulikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tukaendelea kukaa na watu katika mipaka na maswali yasiyokuwa na majibu. Kwa hiyo, haya ni maelekezo ambayo tumeyatoa na kazi hii inaendelea vizuri naamini kabisa muda siyo mrefu changamoto hii ambayo Waheshimiwa Wabunge hasa Mheshimiwa Oliver na Mheshimiwa Vuma ameizungumza itaweza kuwa imepatiwa ufumbuzi wa kudumu. Lakini nakubaliana nao kwamba hili jambo tumeliona na tumelifanya kazi kwa hatua kubwa. Hata hivyo waendelee kunga mkono vyombo vyetu hasa askari wa uhamiaji. Pale linapokuja suala la kuhakikisha kwamba tunawahoji wale wote ambao tuna mashaka nao ni Jambo la msingi sana na ni jambo muhimu kwa usalama wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohakikisha na muda najua kengele imelia nisiingie katika hoja nydingine nikawa sitoitendea haki, naomba niishie hapo mengine yatakayojitokeza basi nadhani tutayajibu baadaye. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mtoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru wewe mwenyewe kwa kusimamia mjadala huu lakini pia niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na niwashukuru Waheshimiwa Naibu Mawaziri ambao wamepata fursa ya kuchangia hoja hii kama sehemu ya kunisaidia katika kutoa ufanuzi wa Serikali na msimamo wa Serikali katika baadhi ya maeneo waliyoyazungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu za kipekee nizipeleke kwa wachangiaji wote, baadhi ya maeneo ambayo wameyashauri tumeyasikia na wapo waliochangia kwa kusema ni 15 na wengine wamechangia kwa maandishi

nipende kwa niaba ya wizara niwashukuru sana. Maeneo kadhaa ambayo nitapata fursa ya kuyafafanua, lakini niseme tu michango yote Waheshimiwa Wabunge ambayo mmechangia ile yenyewe nia ya kujenga wizara inaichukua na tutafanya kama sehemu ya kufanya kazi ama kuleta marekebisho kwa kadri ya maoni na mapendeleko na fursa ya Serikali kadri ya fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Katika bajeti ya mwaka huu mtaona kuna ongezeko kidogo na hili limetokana na maeneo ambayo yana mapungufu katika Taasisi ambazo zinasimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili moja ambalo limezungumzwa na wachangaiji wengi akiwemo Mheshimiwa Semguruka kuhusiana na *NIDA* na wengine wengi ambao wamechangia katika eneo hili. Changamoto kubwa iliyosemwa hapa ni namna ya kufanya utambuzi wa watu wanaostahili kusajilliwa na kupewa uraia, kupewa vitambulisho vya utaifa. Vitambulisho hivi vya Taifa ndio vinavyo-*define* uraia wa muhusika na kwa hivyo tunapochuja na kufanya usajili wa watu hawa lazima tuwe makini sana na hasa maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, pamoja na kazi hii kwamba imefanywa na pengine imekuwa na changamoto hapa na pale lakini jamani uraia si jambo la kulichezea. Uraia ni jambo la msingi na linaambatana na haki za uraia huo, anapopewa uraia mtu ambaye si raia Jambo hili linaweza likaleta shida na hasa katika eneo la usalama wa Taifa letu. Ni kweli kwamba kuna muingiliano mkubwa na mnafahamu katika maeneo mengi ya mipaka ya nchi yetu ni mipaka ilio wazi na kwa hivyo udhibiti na uhakiki wa watu kutokana na ule muingiliano ni jambo gumu sana. Tutaendelea kuwa makini lakini pia kupunguza changamoto zinazojitokeza kwa wale wanaopata usumbufu lakini hatuepukiki kuwa na msimamo wa kuhakikisha kwamba wanaopata vitambulisho hivi ni Watanzania wenye haki ya kupata vitambulisho vyenye. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ilipojitokeza na tulikutana kwenye kamati na nilipata ushauri wa kamati. Kamati ya Ulinzi

na Usalama tulishauriana na ikapelekeea wizara kutoa maelekezo kwa wenzetu waliopo kule kwa maana ya *NIDA* na Uhamiaji na kwamba wasifanye ile kazi kule peke yao lazima washirikiane na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Na kwa mujibu wa Sheria ile ya Vitambulisho vya Taifa imeeleza wazi juu ya mahusiano haya, kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kwa hivyo bado ushauri mnaotoa Waheshimwa Wabunge uko vilevile hata kwa mujibu wa Sheria. Kwamba lazima Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Serikali za Vijiji zishiriki katika kuwabaini wale ambao wana sifa za kupata uraia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa hivyo nitumie bunge hili kutoa maelekezo haya kwa Watumishi wa *NIDA* na Uhamiaji ambao wapo kule katika timu moja ya kuhakiki na kusajili watu hawa ambao wanastahili kupewa Vitambulisho vya Taifa washirikishe Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopo kule Vijijini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imeulizwa hapa juu ya namba kupatikana na baadaye vitambulisho vinakuwa havipatikani. Kutolewa kwa Kitambulisho (*hard copy*) ya kitambulisho ni sehemu ya mwisho kabisa katika utoaji wa vitambulisho na ni sehemu ndogo sana. Lakini sehemu muhimu ni kufanya uchambuzi na kubainisha ili uweze kusajiliwa na kupata namba ya usajili, namba ya kitambulisho. Ile ndio mchakato wake ni mkubwa na ni mchakato ambao unazingatia *consultations* nyingi lakini unaambatana na maswali na ndio maana tukishamaliza kazi hiyo ya uchambuzi huo, ya usajili huo, ya utambulisho huo, sasa kazi inayobaki ni ya vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nipongeze *NIDA* kwamba wamejitahidi sana kwa sababu wamefanya utambuzi wa watu wengi sana. Eneo lililobaki ni la vitambulisho ambalo hatukufanya vizuri kwasababu tumetoa vitambulisho milioni sita tu na ushee na wakati tumeweza kutambua watu zaidi ya milioni 17. Hii ilitokana na changamoto za mashine kushindwa kufanya kazi vizuri, lakini mashine tumeshazinunua nataka niwahakikishie Watanzania

kwamba tutakapoanza mwishoni mwa mwezi huu kutoa vitambulisho tutakuwa na *speed* nzuri na Watanzania karibu wote watapata vitambulisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, imejitokeza jambo la mkanganyiko kati ya usajili wa utelewaji wa Vitambulisho vya Taifa au kupewa namba na usajili wa simu. Usajili wa kupewa Vitambulisho vya Taifa Sheria yetu inasema kwamba tusajili watu wanaoishia miaka 18 kwenda juu, chini ya 18 hapana. Lakini umiliki wa simu unamillikiwa na watu wenye umri chini ya miaka 18, hatuna Sheria inayokataza.

Kwa hiyo, nadhani kuna mahala hatuendi sawa, maswali mengi tunayojobu hapa nadhani itapaswa yajibiwe na *TCRA* na kwa hivyo kwa kuwa Serikali ni moja tutajaribu kuangalia namna ya kufanya. Nadhani jambo hili tulilifanya bila kuwa na angalizo hili, kwamba ndio maana utakuta waliosajiliwa kwenye simu wako milioni 37 lakini utambuzi wa Watanzania ni milioni 27 kama *target* ambayo tulikuwa tumetarajia kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Mamlaka ya kutoa Takwimu ambayo tunapaswa kwa watu hawa tutakaowapata ni milioni 27 tu. Kwa hiyo, nadhani kuna kitu hapa hakijakaa sawa tutajaribu kukiweka sawa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi hapa na mdahalo mkubwa ulikuwa kwenye eneo la Covid 19, Corona. Sisi kama wizara tumejjipanga kuhakikisha kwamba tunalinda Magereza ili wasiathirike kwasababu ugonjwa huu ukiingia magerezani tutapata shida kubwa. Lakini pia tunawalinda Watumishi wetu wakiwemo polisi kwa kuwapatia vifaa nya kujikinga na Corona na tunashirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba vifaa hivi vinapatikana mapema iwezekanavyo ili hata kama Askari wanapokwenda kufanya ukamataji au kufanya shughuli nyingine waweze kuwa na vifaa hivi. Lakini pia corona ni janga la dunia na *pandemics* hizi zimekuwa nyingi duniani pengine mkanganyiko uliopo hapa ni kwamba wengine tunaitizama kama ni sehemu ya kwamba maisha yamefika mwisho basi kila kitu kisiendelee tujifungie ndani, tutakufa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa msimamo wake kwa ufanuzi aliota jana kwamba *pandemics* hizi, kwa mfano kulikuwa kuna *pandemic* ilikuwa inaitwa *the black death* ambayo ilikuwa mwaka 1346 mpaka mwaka 1353 iliua watu kati ya milioni 75 mpaka milioni 200. Ilikuwa inatokana na Kirusi kilichokuwa kinaitwa *Bubonic plague*, na maisha yaliendelea na mpaka leo tupo. Lakini imekuwepo kwa *pandemic* nyingine ambayo ilikuwa inaitwa *plague of Justinian* ambayo ilitokea kati ya mwaka 1541 hadi mwaka 1542 iliua watu milioni 26. Leo hii watu waliokufa hawajafika hata laki mbili wako laki moja na themanini na nne. Hatuwezi kusema tujifungie ndani tutakufa kwa sababu watu wanahitaji kuishi, wanahitaji kula, wanahitaji kufanya shughuli zao na ndio maana Mheshimiwa Rais anatusisiza kwamba tutumie kinga zote ikibidi hata zile za mbinu mbadala. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikibidi hata dawa zetu za asili na Wizara ya Afya wameagizwa kwamba wajaribu kusimamia hili jambo kwa sababu tuna Idara ya Tiba Mbadala kuhakikisha kwamba Watanzania wengi tunajokoa na hii. Lakini unamuona Mheshimiwa Rais anaendelea kusisitiza kwamba ni lazima tuangalie wale waliozidiwa ndio tuwapeleke hospitali. Kwa hiyo, ipo haja ya kuendelea kutafakari na kuona namna gani tunaweza tukashughulika huku tukiwa tunafanya kazi, tusipofanya kazi tutakufa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona watu wanakwenda wameambiwa watawagawia vyakula, watafanya nini lakini kinachotokea sasa ni muingiliano na mgusano ambaunapelekeea ugonjwa sasa unaweza ukaharibu kabisa hata maambukizi yakazidi kabisa katika nchi hizo na siwezi kuzitaja kwasababu za Kidiplomasia lakini walioamua hivyo wamefeli na sisi Tanzania tuko salama sana kutokana na msimamo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yamezungumziwa masuala ya majengo ujenzi wa Vituo vya Polisi, ujenzi wa nyumba za

wafanyakazi katika majeshi ya Polisi na Magereza, jambo hili tunalifanya sana. Katika bajeti yetu hii tumezingatia hilo na tumekubaliana kwamba katika fedha zitakazopatikana, Magereza yako maboma mengi, Jeshi la Polisi lazima tuhakikisha kwamba tunayamalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiasi kikubwa utaona kwamba katika kipindi cha miaka hii mitano ya Serikali ya Serikali ya Awamu ya Tano miradi mingi sana imefanyika katika Wizara hii. Karibu kila mahali Mheshimiwa Rais amepeleka pesa kidogo kidogo na hata wakati mwininge ukifanya tathmini unaweza ukakuta katika miaka hii mitano tumefanya kazi kubwa katika sekte hii ya eneo la Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Sekta hizi za Polisi na Magereza kuliko wakati mwininge wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo ambayo yalikuwa hajawahi kuguswa kwa mradi wowote toka tulivyoachiwa na wakoloni, lakini sasa yameguswa. Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivi na kuhakikisha kwamba tunaboresha maisha ya Askari wetu na sehemu za kufanya kazi Askari wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi la kisasa ni jambo la muhimu. Napenda kuchukua ushauri kwamba sasa tuwe na Jeshi la Polisi la kisasa.

Katika hali ya mazingira ya sasa hata uhalifu unaofanyika ni wa kisasa zaidi. Unapokuwa na Askari ambao hawana usasa na wanatumia akili za kizamani na mbinu za kizamani bila kutumia vifaa vya kisasa vya kiteknolojia, nadhani udhibiti wa uhalifu utakuwa mgumu. Kwa hiyo, naungana nanyi wote mliotushauri na kwamba Serikali inajitahidi kufanya *transformation* hiyo na tutahakikisha kwamba tunaweka hata hizo *camera* kupunguza na kuona matukio yanapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo ambayo zimebekwa *camera* kuna *improvement* kubwa, hata kwenye mabenki na maeneo mengine. Tutajaribu kufanya hivyo hata

kwenye miji yetu ikiwemo na Dodoma ambayo uhalifu unakua kwa kasi kidogo, lakini tutajitahidi kuudhibiti. Nawapongeza sana Askari Polisi wa Mkoa wa Dodoma, wanajitahidi sana kufanya hivyo na Mikoa mingine mikubwa wanajitahidi kufanya hivyo. Nampongeza sana *IGP* kwa sababu anafanya kazi nzuri. Tuendelee kukaza kwa sababu mabadiliko haya ya kiuchumi pia yanaweza kusababisha uhalifu kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa vitendea kazi kama upungufu wa magari, ni jambo ambalo tumejitahidi sana miaka miwili tu iliopita na tunaendelea na huo mradi wa magari 700, tumeendelea kuingiza na Serikali ilitoa pesa, lakini tuseme tu kwamba bado hayatoshi. Tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunatafuta namna nyingine mbadala ili kuongeza magari na ikibidi kwenye vituo vidogo kupeleka pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhamiaji mipakani; nimesema hili pamoja na *NIDA*. Tuwapongeze tu kwamba wanafanya kazi nzuri, lakini lazima tuhakikishe kwamba tunadhibiti na kuhakikisha kwamba uraia unatoa kwa mtu mwenye sifa ya kupewa uraia kwa mujibu wa Sheria ya Uraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza kujitegemea kwa chakula, hili mmelisemea na ninawashukuru. Wamejipanga na wametuletea taarifa kwamba watahakikisha kwamba wanajitegemea kwa chakula. Tutaenda *gradually*, hatuwezi kwa mara moja tukatimiza kwa Magereza yote lakini wengine wanaweza kuwalisha wengine na pale tutakaposhindwa, basi tutajua namna ya kufanya, lakini itasaidia kuokoa fedha na kufanya nguvu kazi ile isipotee kama tulivyosema kwenye hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Ulinzi Binafsi, sheria ile Mheshimiwa Almas ipo katika mchakato wa mwisho kabisa. Ni bahati mbaya tu kwamba hili ni Bunge la mwisho, lakini tulikuwa kwenye mchakato wa mwisho kabisa. Nataka nikuhakikishie kwamba kwa wale watakojaliwa kurudi, mimi

nina hakika nitarudi, tutakuja kushiriki wote kumalizia kuitunga sheria hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na bodaboda Vituo vya Polisi; Waheshimiwa Wabunge bodaboda zimeongeza na nyingine zimekuwa ni vitendea kazi vya kiuhalifu sana. Uhalifu sasa haufanywi kwa kutumia magari, bali unafanywa kwa kutumia bodaboda. Wanapokurupushwa na Polisi hukimbia na kuziacha, ndiyo maana mnazikuta zimelundikwa mle kwenye Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtu yejote au Mbunge yejote ambaye ana kesi mahususi kwamba bodaboda wake akiwa na kosa la kawaida, bodaboda yake imezuiliwa, naomba atuone lakini tusi-*generalize* kwamba bodaboda zilizojaa kwenye Vituo vya Polisi basi ziko pale kimakosa, ziachiwe hapana. Hivi ni vidhibiti na ni ushauri kwa wallotenda makosa na kesi ziko Mahakamani na wengine wamekilimbia na hawajulikani waliko. Sasa kuna utaratibu wa namna ya ku-*dispose* hivi vitu kisheria. Kwa hiyo, tusichukulie tu kwa ujumla, lakini kama kuna mtu ana kesi mahususi, ailete tutaishughulikia kwa namna ilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kudhibiti mwendokasi wa magari barabarani na Askari wale wa barabara wanaopiga picha; malalamiko haya ni makubwa na kusema kweli mara nyingi mimi mwenyewe nimeyapokea, kwamba mtu amezidisha *speed* 52 mahali ambapo tunasema *speed* 50 unakuta mvutano ni mkubwa na Askari wetu na wenyewe unakuta wana msimamo mkali, unamkuta naye dereva anayeendesa wanarushiana maneno. Wakati mwingine ni *approach* tu. Mheshimiwa Kanali Mstaafu amesema madereva wetu wanapaswa kuwa na hekima na uadirifu na kufanya kazi kwa uaminifu na siyo kwa dharau. Haya mambo tukiyasema pande zote kama Wawakilishi wa Wananchi, kuzingatia na kufuata sheria bila kulazimishwa ni jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ukimkuta Askari ukiwa umezidisha *speed* mbili; badala ya 50, ni 52 ukamwambia

samahani bwana; lakini mtu anasema mimi ni *speed* mbili tu, halafu unanikamata! Ndiyo mambo yanayopelekea sasa wanakaziana. Mnajua hao ni vijana, wana nguvu. Hawa vijana wakianza kubishana, wote ni vijana inakuwa shida. Sisi wote hapa tunapita barabarani huko na ukiongea na Askari vizuri wanakuwa ni waungwana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani tufanye kazi yetu kwa pande zote; sisi tunaosimamia Askari wetu tutawaambia wawe waadilifu na wawe na busara katika kufanya maamuzi haya, kwa sababu haya ni maisha, wakati mwingine mtu kajisahau kapitiliza kidogo. Wakati mwingine unammulika halafu wanampa *reading* ya uongo; na yenye we hayo yanajitokeza. Pia wakati mwingine wanatumia simu katika kupiga picha; na yenye we yanajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitumie Bunge lako Tukufu kumwagiza /GP atoe maelekezo maalum juu ya udhibiti wa mwendo wa barabarani kwa sababu yanayofanyika yanasa babisha fujo. Ziko *recording* za picha kwa *camera* za simu, hii haikubaliki, kwa sababu tuna kifaa mahususi ambacho wote tutakiamini. Kwa sababu simu yako hiyo, huyu Nokia, huyu ana *iphone*, huyu *Sumsung*, tunaaminianaje kwamba ni kitendea kazi ambacho tumekipitisha kisheria? Hii haikubaliki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna kupiga picha halafu ile *image* inasogezwa, kwa sababu aliyekupiga amekupima ama unakwenda au unarudi, hapa pana hitaji msimamo wa kisheria. Kama kuna sheria tulioitunga inaruhusu hivyo, sawa; lakini kama hatuna sheria tulioitunga inaruhusu, hiyo mbinu haikubaliki kwa sababu inasema uongo na inawasingizia wengine na ndiyo maana ubishi unakuwa barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naagiza tu picha zinazopigwa kwa kujificha; hivi kwa nini tujifiche? Maana barabarani tupo kila siku, nasi ndiyo madereva. Hakuna sababu ya kujificha. *Speed* ziko barabarani mle, tuendelee kuongeza elimu zaidi kwa madereva wetu, tuendelee

kuongeza wapate uelewa na kufuata alama za barabarani, lakini kushitukizana tutasababisha ajali. Maana saa nyingi unakuta Askari anatokea hivi, mpaka ye ye mwenyewe anaweza akagongwa sasa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa hili, nawaagizaa tu Jeshi la Polisi usalama barabarani kuwa na mbinu za kistaarabu za kusimamia sharia. Nchi hii ni yetu sote, nchi hii kila mtu anastahili kupata raha na furaha. Kwa hiyo, ni lazima tusimamie sharia; siyo kwa nia ya kukomoana, bali kwa nia ya kujenga ustaarabu na ustawi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yamesemwa mengi na niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu na hotuba yetu ilikuwa ni ndefu, timesoma kwa kifupi mambo mengi ambayo mlikuwa mnayasema, majibu yake yamo kwenye hotuba yetu mnawenza mkaipata mle. Vinginevyo, niyachukue yote ambayo hatukuyajibu tukayajibu kwa nyakati nyingine katika ufanuzi wa kawaida. Itoshe tu kusema nawashukuruni sana kwa kutuunga mkono na kutushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wizara yangu napenda nimshukuru Spika, nikushukuru na wewe kwa kusimamia hoja yetu hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. Ahsanteni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa kwa kawaida kama mnavyojua, baada ya mabadiliko kidogo, kuna watu wameomba hapa ufanuzi kuhusu hii hoja. Mheshimiwa Joram Hongoli.

## **HOJA ZA KISERA**

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa nafasi, jambo langu ni dogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kujua Serikali ina mkakati gani wa kujenga Vituo vya Polisi kwenye maeneo au Tarafa zile ambazo kwa muda mrefu zimekuwa hazina Vituo vya Polisi na maeneo hayo kuna huduma muhimu kama benki na vitu vingine ambavyo vinahitaji ulinzi wa Jeshi la Polisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hilo tu, nataka ufanuzi kwamba nini mkakati wa Serikali kuhakikisha maeneo haya yanakuwa na Vituo vya Polisi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ujenzi wa Vituo vya Polisi, kuna njia mbalimbali ambazo tunazitumia. Moja ni utaratibu wa kwenye bajeti ambapo Mheshimiwa Mbunge ni shahidi hata mwaka huu tumetenga fedha hizo kwa ajili ya umalizaji wa Kituo cha Mbalizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo hichi cha Mbalizi kilijengwa kwa jitihada kubwa za wananchi pamoja na viongozi wanaohusika. Kwa hiyo, hiyo vilevile ni njia nydingine. Kuna maeneo mengi ambayo kuna Vituo vya Polisi, tumeona jitihada za wadau mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge wakianzisha michakato mbalimbali ya ujenzi wa vituo, halafu baadaye Serikali inaingia kumalizia kama ambavyo tunatarija kufanya katika bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikshie tu kwamba mipango ya Serikali ya kujenga vituo vya wilaya tunatambua juu ya changamoto hizo siyo tu katiika vituo vya wilaya, lakini hata baadhi mikoa mipyä kuna mingine bado haina hata Ofisi za Mikoa za Ma-RPC.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jutihada hizo zipo, pale ambapo bajeti itakaa vizuri, tutajenga katika Mikoa yote na Wilaya zote, lakini kwa sasa hivi tunapokea vilevile na michango ya wadau mbalimbali na viongozi mbalimbali wa kisiasa watakaokuwa tayari kushirikiana na Seriakli katika kukabiliana na changamoto hii ya upungufu wa Vituo vyta Polisi nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud ufanuzi. Sasa kwa sababu mko Masoud wengi, inabidi utajwe Masoud kikamilifu. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo mimi mwenyewe mzee, yule kule kijana kijana kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nilitaka tu kupata ufanuzi, sina haja ya shilingi ya Mheshimiwa Waziri, najua shilingi yake ina kazi nydingine. Nataka kupata ufanuzi kuhusu ule muda wa ukomo wa upelelezi sambamba na lile giza nene, kitu ambacho tunakiongelea muda mrefu juu ya sakata au giza nene la Mashehe wetu wale wa Kiislamu waliokaa muda wa miaka nane kama mahabusu, wakati mwaka 2019 tulipata taarifa kwamba *email* zao ziko hapa na pale. Kwa hiyo, nataka kupata ufanuzi zaidi wa kisheria ukoje? Maana yake na muda umekuwa mrefu na hatuoni ufanuzi wa aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufanuzi.

**NAIBU SPIKA:** Namwona Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesimama, lakini hili jambo kimsingi ni jambo muhususi, ni jambo linalohusu watu fulani, siyo jambo la kisera. Hoja zinazotoka kwenye mshahara wa Waziri ni zile zinazohusu sera. Kwa kuwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ulisimama, labda nikupe hiyo fursa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nitapenda kumrejesha Mheshimiwa Mbunge aliyeomba ufanuzi kwenye ufanuzi nilioutoa siku

ya kikao cha bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, tulieleza vizuri kwamba kabla ya hapo palikuwepo na changamoto za kiutaratibu zilizohitaji kuwekewa mfumo mahususi wa kisheria. Hatua hiyo ilishafanyika. Kwa hiyo, zile hatua mahususi za kiutaratibu wa kisheria zipo tayari na kwamba mashtaka kuhusu watu hawa yataanza muda siyo mrefu baada ya hapa. Ahsante. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Nilikuwa naomba ufanuzi kwenye suala la hati za kusafiria (*passport*). Kumekuwa na utaratibu ambapo mwananchi popote alipo anaweza akapeleka maombi yake kuomba hati ya kusafiria, lakini kuna tatizo kidogo kwa upande wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar kwa maana kwamba Watanzania wenyе asili ya Bara wakiomba hati za kusafiria kule mchakato unaanza, lakini unapofikia hatua ya mwisho wanaambiwa waje huku Bara, lakini wakati wanafika hatua hiyo tayari watakuwa wameshafanya mpaka malipo na wakija huku Bara wanaanza upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitaka tupate ufanuzi, kwa nini jambo hilli linatokea na hii ni nchi moja na huko Mikoani kote taratibu zinafanyika hivyo? Kwa nini hawa Watanzania wanaoishi kule wakiomba, lazima waambiwe waje huku Bara na wakati mwingine wameshalipa, wanalazimika kulipa kwa mara ya pili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Shangazi kwa swali lake. Nami nilishalisikia na *of course* lina ufafafuzi wake, lakini kwa namna lilivyo na kwa *complication* hii namwomba tu Mheshimiwa Shangazi, acha tulichukue, tutalifanyia kazi ili kama kweli kuna hilo tatizo la kwamba mtu ukishafanya

process kule, ukaimaliza na kulipia halafu ukija huku tena unaanza na moja, tulione kwa namna lilivyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nipate ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba tunavyozungumzia ufanisi wa kazi za Jeshi la Polisi ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha za bajeti ambazo tunazitenga kwa ajili ya shughuli za maendeleo zinakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeonekana katika bajeti hii fedha ambayo ilitengwa ilikuwa ni shilingi bilioni 31.9 lakini fedha ambayo imetoka kwenda shughuli za maendeleo ni shillingi bilioni 7.9 peke yake ambayo karibuni ni asilimia 24 tu. Sasa changamoto ziko nyangi sana kwenye Jeshi la Polisi na inawezekana ikawa ni sababu kubwa ya Jeshi la Polisi kushindwa kutekeleza majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hizo fedha katika bajeti ya mwaka huu kabla hatujamaliza muda zitakuwa zimeshatoka kwenda kufanya kazi hizo au ndiyo imeshatoka hivyo hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ufanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba fedha zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya maendeleo zilikuwa ni *thirty one point nine billion* na zilizotoka ni *seven point nine, which is like twenty four percent* na tumeweza kufanya shughuli zetu. Kwa muda huu uliobaki pia tunaweza tukabahatika tukazipata na tukizipata zitafanya zile shughuli ambazo zilikuwa zimepangwa kwa sababu bado tunao muda kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hii *Corona* na mambo mengine nadhani Mheshimiwa Mbunge *you must*

*be reasonable enough* kuona kwamba kwa sasa mambo ni magumu na kwa hiyo, sisi kama Wizara tumeweza kutimiza majukumu yetu kwa kiwango ambacho tumeweza na kama zikitoka, basi *inshallah* tutafanya majukumu yetu kwa muda huu uliobaki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza naomba nilipongeze Jeshi la Polisi kwa jana kuzuia na kuokoa Waandishi wa Habari ambaao walikuwa wanaenda kukutana na kiongozi ambaye alitoka karantini hivi karibuni. Tunafahamu Wabunge tuna fursa nyingi na tuna *exemption* nyingi. Kifungu cha 83 (a) na (b) cha Sheria ya Magereza Na. 34 ya mwaka 1967 kinazuia mtu yeoyote kusogea eneo la Magareza ama kuanzia eneo la mita 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka ufanuzi kujua sisi Wabunge tunaruhusiwa kusogea maeneo hayo ya Magereza au kuingia muda wowote kwa maana ya kifungu hiki hakituhusu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ufanuzi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ufanuzi wa swali liliolizwa na Mheshimiwa Mlinga. Ni kweli kwamba kifungu cha 83 (a) na (b) cha Sheria ya Magereza kinalifanya eneo la Magereza na hasa gereza kuwa *smart area* na *high security area*; na kwa hiyo, unapokwenda pale ni ama unapelekwa kwa nia ya kipelekwa Magereza kama mahabusu au mfungwa au unakwenda kwa shughuli nyingine zenyenye kibali maalum. Sasa kama unakwenda pale kwa namna ya tofauti lazima utakutana na taratibu za ulinzi wa Magereza ambazo zitachukuliwa.

Sasa kama unakwenda pale kwa namna ya tofauti lazima utakutana na taratibu za ulinzi wa Magereza ambazo zikichukuliwa na kwa sababu nimesema ni *high security area*

basi zinaweza zikawa kidogo zina uzito. Kwa hiyo nimfahamishe tu Mheshimiwa Mlinga kwamba ukipenda kwenda haya, lakini hatua kali zitachukuliwa kwa sababu mpaka uwe unajulikana unakwenda kufanya kitu gani.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto.....	Sh. 35,099,519,000
Fungu 28 - Jeshi la Polisi.....	Sh. 562,497,260,000
Fungu 29 - Jeshi la Magereza.....	Sh. 186,661,298,000
Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya	
Ndani ya Nchi.....	Sh. 20,140,032,000
Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.....	Sh. 59,336,322,000

#### **MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto.....	Sh. 3,500,000,000
Fungu 28 Jeshi la Polisi.....	Sh. 2,034,050,000
Fungu 29 - Jeshi la Magereza.....	Sh. 14,590,000,000
Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya	
Ndani ya Nchi.....	Sh. 10,861,812,000
Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji.....	Sh. 4,450,000,000

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa taratibu zetu hizi mpya tumefika mwisho wa mjadala, lakini pia bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani imepitishwa. Nilikuwa naangalia kura hapa, kura nydingi zimesema ndiyo. (*Makofii*)

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge waliopiga kura za ndiyo wameshinda na hivyo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi yamepitishwa rasmi na Bunge.

Pamoja na hayo nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Wabunge wengi wamesifia hapa, kazi nzuri inayofanywa na nyle kama Wizara na vyombo vyote vilivyo chini ya Wizara hii. Changamoto zilizosemwa pia haziwezi kukosekana lakini ni muhimu kuzifanyia kazi. Kwa hiyo mimi niwapongeze sana kwa hatua hii ambayo Bunge inawaamini kwamba mnaweza kwenda kutekeleza bajeti hii, ambayo mmeiomba.

Pia niwaombe kama Mheshimiwa Waziri ulivyosema, yale mapendekezo yaliyotolewa kwa ajili ya kuboresha hapa na pale basi ni vizuri yafanyiwe kazi. Umetuambia vyema kwamba umewasikia Wabunge wakisema, lakini Waheshimiwa Wabunge pia tuishukuru Kamati ambayo imefanya kazi kwa niaba yetu sisi sote. Wametoa mawazo mazuri ambayo yameisaidia Wizara kwenye mambo mbalimbali ambayo wameyazungumza hapa. Kwa hiyo tunawashukuru Kamati yetu kwa kazi nzuri na Wajumbe wote, na Wabunge wote ambao wamepata fursa ya kuchangia. Tunaamini kwamba nchi yetu itasonga mbele kwenye hili eneo ambalo Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi analisimamia. (*Makofii*)

Pamoja na hayo Waheshimiwa Wabunge, kuna miongozo miwili ilikuwa imeombwa hapa. Nitazungumza kwa kifupi mambo matatu: la kwanza ni mwongozo wa Mheshimiwa Mashauri Mashimba Ndaki ambaye alikuwa ameomba mwongozo kuhusu mchango uliotolewa na Mheshimiwa Lema. Kama hili jambo kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 68(7) alikuwa ameomba Mwongozo akitaka kujuu kama hili jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi.

Sasa hilo jambo aliloliombea mwongozo katika mchango wa Mheshimiwa Lema wakati akichangia katika kusema kwake kuna eneo alisema na nitalinukuu hilo eneo alisema:

*"Najiuliza hivi wakiambukizwa Polisi leo, na tunakwenda kwenye hali mbaya ya uchumi, utalii sasa hivi*

*ni asilimia sifuri, TANAPA na KINAPA kwa siku walikuwa wanatengeneza zaidi ya bilioni moja. Leo Kamati ya Bajeti imesema hawatengenezi milioni nane kwa siku”.*

Akaendelea na maneno mengine hapo. Kwa hivyo haya maneno aliyoyazungumza Mheshimiwa Lema hasa hii sehemu ya mwisho kwamba Kamati ya Bajeti imesema hawatengenezi milioni nane kwa siku ndio yaliyoombewa mwongozo na Mheshimiwa Mashauri Mashimba Ndaki. Kwamba je yanaruhusiwa na yeye kwa maelezo yake anasema Kamati yake hajatoa hiyo tathmini kuhusu utendaji kazi ama kuhusu mapato katika hili eneo la TANAPA na KINAPA.

Kwa muktadha huo, hilo jambo kwa sababu ameomba mwongozo haliruhusiwi. Kwa sababu haliruhusiwi basi ili taarifa ya Mheshimiwa Lema ikae vizuri kwenye kumbukumbu za Bunge ni hiyo sehemu tu ya sentensi inayozungumzia Kamati ya Bajeti, itaondoka kwa sababu Kamati ya Bajeti hajasema hayo maneno.

Mwongozo mwingine nimeombwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kuhusu matumizi ya neno Dola na kwamba Katibu Mkuu wa CCM amezungumziwa hapa ndani na mchango uliotolewa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim kwamba Mheshimwia Dkt. Bashiru alizungumza kwamba CCM itatumia Dola kubaki madarakani.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza lazima tuelewe matumizi yetu ya vyombo vya habari na sisi kama Viongozi tukichukua haya ambayo wenzetu wanatuhabarisha lazima usome habari nzima. Yapo mambo ambayo tunaweza tukavilaumu vyombo vya habari, lakini yapo mambo ambayo vyombo vya habari vinahitaji viseme kwa namna fulani ili chombo chake kinunuliwe au kisikilizwe. Ukitisema kinunuliwe kwa maana ya gazeti, ukisema kisikilizwe basi ni kile chombo kinachosikika. Kwa hivyo yeye atachukua sentensi moja ataiweka hiyo na wewe ukaamua kuichukua hiyo bila muktadha wa ilizungumzwa vipi, unakuwa unaleta changamoto kwa sababu pia haiyumkiniki chombo cha

habari kitaweka kichwa cha habari cha muktadha mzima, kinaweka neno ili wewe ukafuatilie hiyo habari.

Waheshimiwa Wabunge, bahati nzuri gazeti hilo hilo alilokuwa akilitazama pale Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim la Habari Leo la Siku ya Jumamosi, tarehe 7 Machi, 2020. Ukisoma taarifa yenye utagundua kwamba ufanuzi ultolewa pale pale wala hakukuwa na haja ya mtu kueleza kwamba pengine Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Dkt. Bashiru kasema atatumia Dola kubaki madarakani, kwa sababu maelezo yaliyoko kwenye gazeti hilo hilo yanaeleza wazi alisema kitu gani na pia alimaanisha nini.

Sasa niwasomee sehemu ndogo tu, inayotoa ufanuzi kwenye gazeti hili hili, inasema hivi: *Alisema watu wanaweza wasielewe falsafa ya kutumia Dola kubaki madarakani, allifanua kuwa kusimamia rasilmali, kusimamia matumizi ya kodi na makusanyo, utekelezaji wa miradi, ujenzi wa Vituo vya Afya, Elimu bure, ndio matumizi sahihi ya Dola na ana uhakika wa kushinda uchaguzi mwaka huu na atatumia Dola sawa sawa*". (*Makofii*)

Maana yake ni hii, Waheshimiwa Wabunge sitaki kurejea maelezo marefu aliyojatao Mheshimiwa Bashe kwa maana ya neno Dola. Tunaposema Serikali ya CCM na haya maneno huwa tunayatumia sana kwa kifupi, ni kwamba hii Serikali ndio iliyopigiwa kura ama ahadi zake ndizo ambazo wananchi wameziamini kwa miaka hiyo mitano.

Kwa hiyo ukisema sasa hivi Serikali inakusanya kodi maana yake ni Serikali ya CCM; ukisema Serikali inajenga kitu gani, ni Serikali ya CCM; ukisema umeme huko vijijini, ni Serikali ya CCM. Kwa hiyo akisema atatumia Dola maana yake Serikali ile iliyopo madarakani kwa kuwa ni Serikali ya CCM inatekeleza yale ambayo wananchi walihidiwa na kwa namna hiyo hiyo wananchi hawatashindwa kuiamini tena, kwa kuwa imetekeliza waliyoahidi. (*Makofii*)

Kwa hiyo nawashauri Waheshimiwa Wabunge, tusifikie mahali ambapo tutataka kuwarushia mpira kila

wakati Wanahabari, sisi wenyewe tuangalie muktadha kwa sababu mwanahabari anatafuta maneno ambayo Waingereza wanaita *catchphrase* ili aweze kufanya hiyo kazi yake ya habari.

Jambo la mwisho Waheshimiwa Wabunge, tumezungumza sana kuhusu *corona* na Mheshimiwa Rais alishatoa mwongozo. Mimi nimwombe Mheshimiwa Kigwangwalla kwa sababu ndio yupo hapa, lakini pia Mheshimiwa Waziri wasichoke kuendelea kutoa elimu kwa sababu yanapotokea mambo kama haya yanaonesha namna ambavyo bado tunahitaji elimu iendelee kutolewa kila wakati. Kwa hiyo tusichoke kuendelea kutoa elimu na Mheshimiwa Rais ametoa mwongozo mzuri, naamini tukitembea katika mwongozo wa Mheshimiwa Rais, tutaweza kutoa maelezo mazuri zaidi kwa wananchi na wataelewa. Naamini wameshaelewa na wanaendelea kuyafanya kazi, ndio maana hata yale mabaya sana yanayosemwa watu wanayasubiri lakini naamini hayatotokea, naamini hivyo. (*Makof!*)

Kwa hivyo pengine tu kwa kumalizia ni kwamba *corona* ipo na ni halisi, tujihadhari, lakini tusitishwe na pia tusitishane sisi wenyewe. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwatakie kila la kheri Mheshimiwa Simbachawene na Wizara nzima kwenye utekelezaji wa hii Bajeti na naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho saa nane mchana.

Jambo lingine kesho itakuwa ni Bajeti ya Wizara ya Elimu, kwa sababu Wizara ya Mambo ya Ndani tumehitimisha leo. Nadhani tumelewana vizuri Waheshimiwa Wabunge, kesho Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa nane mchana.

*(Saa 12.11 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 24 Aprili, 2020, Saa Nane Mchana)*